ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13.Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
22. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
23. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
24. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
25. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
26. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
27. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la mwanakwerekwe
28. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
29. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
30. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
31. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
32. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake

34. Mhe. Asha Abdalla Mussa - Jimbo la Kiwengwa
35. Mhe. Bahati Khamis Kombo - Jimbo la Chambani
36. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Jimbo la Wawi
38. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Nafasi za Wanawake
39. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Shaurimoyo
40. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo
41. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni
43. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje
44. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe
45. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini
46. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo
47. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani
48. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando
49 Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu
50. Mhe. Mihayo Juma N'hunga - Jimbo la Mwera
51. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni
52. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile
53. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
54. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
55. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
56. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
57. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
58. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
59. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
61. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
62. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
63. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
64. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
65. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake
66. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
67. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
69. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu

70. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
72. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
74. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Jimbo la Micheweni
75. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
77. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
78. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
79. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
80. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
83. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Kumi na Saba – Tarehe 13 Juni, 2016

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika (Mgeni Hassan Juma) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Bwana Yesu asifiwe, *assalam alaykum.*

Wajumbe: *Waalaykum salaam.*

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: *Ramadhani Kariim.*

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha mezani hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kuweka hati mezani ya maoni ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya Baraza la Wawakilishi, kuhusu hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, baada ya kusimama kwa mguu moja kwenye Kanuni ya 63, nakuja kwenye Kanuni ya 43, kuhusu kauli za serikali.

Mhe. Naibu Spika: Umesema Kanuni ya 63 au 43?

Mhe Jaku Hashim Ayoub: Ni Kanuni ya 63, ndio iliyonisababisha nisimame hapa, lakini hoja yangu nataka kauli ya serikali Nam. 43.

Mhe. Naibu Spika: Sasa unasemaje?

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Eeh! Kuna jambo tokea jana Mhe. Naibu Spika, na juzi limetokea kuchukuliwa ng'ombe Kwarara/Fuoni ni jambo la kusikitisha na nilisema humu ndani kuna milango mitatu ya kuingilia; uchaguliwe na wananchi, uteuzi wa Mhe. Rais au viti maalum. Mhe. Naibu Spika, ng'ombe wanachukuliwa Kwarara na wengine hata ndio miungu yao majumbani mwao wanachukuliwa. Nataka kauli ya serikali ndio utaratibu ulioagizwa huo?

Mhe. Naibu Spika: Sasa anayehusika na masuala hayo Mheshimiwa, hayupo, wacha afike ataweza kutoa maelezo kuhusiana na suala hilo, lakini anayehusika hayupo sasa hivi, sawa Mhe. Waziri, ana shughuli nyengine anafanya baada ya hapo atakuja kutoa maelezo. Tumefahamiana?

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, najua serikali inafanya kazi kama *team work*, ndio maneno yao siku zote yupo Waziri wa BLM, hapa anaweza kutoa kauli, yupo na Naibu Waziri wa Afya na mawaziri wengine wapo.

Mhe Naibu Spika: Sawa, sawa lakini…

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya ku-*respond*.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba ukisoma Kanuni ya 43 inaitaka serikali kama vile ambavyo Mhe. Mjumbe, ameeleza, lakini ningemuomba tu mjumbe ashuke kidogo kwenye Kanuni ya 44 inaelekeza utaratibu mzuri tu wa serikali namna ya kuweza kutoa kauli. Kwa hiyo, nimuombe tu Mhe. Mjumbe, *concern* yake serikali tumeisikia na sisi kama serikali atupe muda kwa mujibu wa Kanuni ya 44, tutatengeneza utaratibu maalum kama ingekuwa jambo la kuja kusema. Lakini kwa kuwa jambo lenyewe limekwisha kufanyiwa kazi na kinachopaswa kufanyika ni kile ambacho Mjumbe analalamikia, basi nimuombe Mhe. Mjumbe, atengeneze utaratibu wa kuihoji serikali ili serikali tuweze kumpatia majibu kama vile ambavyo yeye angependa.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante nakushukuru Mhe. Waziri, lakini hata hivyo kanuni hiyo hiyo ambayo Mhe. Mwakilishi, ameizungumza Kanuni ya 43, fasili ya (2) inasema:

"Kauli za aina hiyo zinaweza kutolewa kwa idhini ya Spika, katika wakati unaofaa kufuatana na mpangilio wa shughuli ambazo umewekwa na Kanuni ya 27".

Sasa kwa mustakabali huo ningemuomba sana Mheshimiwa, asubiri kama nilivyosema mwanzo, asubiri ili tuweze kumpata Mhe. Waziri na atumie utaratibu huo wa namna gani ya kuweza kupata taarifa, hivi hivi hatuwezi kuendelea na kauli hiyo. Nashukuru.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2016/2017 – Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, leo hii tunatarajia kuimaliza Wizara ya Elimu na majina ambayo yameletwa hapa mpaka sasa hivi ni majina 26, kwa hiyo. ningewaomba sana na leo hii tutatoa nafasi zaidi kwa wale ambao hawajawahi kuchangia kama ameleta jina lake mbele. Tutatoa nafasi kwa wengine ambao wamechangia lakini wamechangia kwa muda na huu ndio utaratibu wa Mabunge mengine ili kuwapa nafasi wajumbe wote waweze kuchangia katika wizara mbali mbali. Naomba sana tuelewane kwa hilo.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wajumbe, naomba nitataja majina ambao watachangia na wala sasa hivi sitaki kifungu wala kanuni yoyote, nimepewa mamlaka ya kuweza kutoa maamuzi, na tutafata utaratibu ambao tumejipangia kwamba ni afadhali tufanye hivyo ili tuhakikishe na wengine wanapata nafasi, kwa sababu na wengine ni wawakilishi wa wananchi vile vile, wenzetu wengine ni wawakilishi wa wananchi. Kwa hiyo, naomba tukae sawa waheshimiwa, tukiachie kiti kifanye kazi yake vizuri. Nashukuru sana.

Sasa Waheshimiwa Wajumbe, naomba nimtaje mchangiaji wa mwanzo kabisa.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana, mimi kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia afya njema na kuwajaalia viongozi wote tukakutana kwa uzima na vile vile, nitaomba kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Naibu Spika, mimi ningeanza na suala la kujenga skuli za ghorofa mjini. Mhe. Naibu Spika, nafahamu kwamba serikali ina lengo zuri la kujenga skuli ambazo ni za ghorofa ndani ya mji, lakini tukiangalia vile vile mashamba skuli zao ziko taabani. Sasa serikali sijui imeangalia vigezo gani vya kufurahisha watu wa mjini wajengewe ghorofa, lakini wale wanaoishi shamba wabakie na mabanda yale yale ya zamani ambayo hata sakafu hamna ndani. Mhe. Naibu Spika, ningemuomba sana Mhe. Waziri wa Elimu hili suala ambalo la kujengwa skuli za ghorofa mjini lifikiriwe ili wale wananchi wa vijijini kule majimboni kwetu wenye skuli mbovu za zamani ambazo hazijawahi hata kukarabatiwa zile ndio zishughulikiwe mwanzo halafu ndio zijengwe hizo ghorofa.

Mhe. Naibu Spika, mimi nafurahi sana mjini wapate ghorofa na baadhi ya sehemu wapate ghorofa, lakini tukisema kwamba tufanye maghorofa tu mjini lakini huku shamba wasijengwe na wakawekewa hali nzuri skuli zile zile walizokuwa nazo. Maana yake mpaka hivi sasa skuli ziko taabani, hazina madirisha, mabati yanavuju na ikinyesha mvua wanaroa ndani, hawana pakukaa, madeski hawana, sasa itakuwaje serikali ifikirie kujenga maghorofa mjini wakati skuli za mjini ni nzuri, waache kumaliza za shamba halafu ndio waingie Mjini.

Mhe. Waziri, ningekuomba sana mngewatizama kwanza watu waliokuwa wanyonge wa mashamba wakarekebishiwa skuli zao pamoja na matatizo yote waliyokuwa nayo halafu ndio muangalie mjini, kila siku mjini, mjini, watu wa shamba wanaangaliwa muda gani. Kwa hiyo, ningekuomba sana Mhe. Waziri, ungekaa na wizara yako mkaangalie hili wazo la kujenga skuli za ghorofa mjini sio vibaya, ni suala zuri kwa sababu wananchi ni wengi, lakini vile vile na shamba wananchi ni wengi na wako katika hali mbaya.

Mhe. Naibu Spika, hali inasikitisha sana ya majimbo yote ya shamba, kwani maeneo yote ya shamba Unguja na Pemba, skuli ziko taabani, yaani sijui hata nizifananishe na mabanda ya mifugo gani ya wanyama. Yaani mle ndani hata kama hao wanyama saa nyengine hawafugiki kwa hali iliyokuwepo. Kwa hiyo, ningekuomba sana Mhe. Waziri, hili suala la kujengwa skuli za ghorofa kwanza wizara yako ikasimamisha na ikaangalie kwanza hali iliyokuwepo shamba na vijijini warekebishiwe hali zao zikawa nzuri halafu ndio mkaitafuta mjini kujenga maghorofa, sio mnaanza mjini watu wa shamba mnawasahau. Mimi kwenye mchango wangu skuli ulikuwa ni huo.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, nitaenda kwenye suala la elimu. Mhe. Naibu Spika, nafahamu kwamba Wizara ya Elimu inatambua kuwepo kwa Chuo cha

Kiislamu ndani ya Zanzibar na inatoa walimu kusomesha mashuleni dini ya Kiislamu pamoja na Kiarabu, lakini chakusikitisha zaidi wizara haiwatambui walimu wa vyuo. Walimu wa vyuo wa dini wamewekwa chini sana japokuwa inatambua Chuo cha Kiislamu cha Zanzibar na inasomesha wanafunzi mambo ya dini, lakini walimu wa vyuo wametupwa. Mimi ninachomuomba Waziri wa Elimu na wizara yake na hawa walimu wapewe *priority* kama walivyopewa walimu wa skuli nao wawe wanathaminika kila siku wasikae chini tu. Kwa kuwa serikali chuo hiki inakitambua, kwa nini na walimu wa vyuo wasitambulikane wakapewa na wao mishahara, wakapewa na vitu vyengine kama wanazopata walimu wa skuli? Kwa sababu elimu ya duniani ni elimu hii ya dini pia, yaani "dini na dunia".

Kwa hiyo, lazima wafikiriwe hawa tusikae tu tukajisahau sana tukabeba tu walimu wengine, lakini wa chuo tukawasahau. Mimi namuomba sana Mhe. Waziri, aje anijibu vizuri tu vipi atakuja kufanya katika mambo yake yote kuhakikisha kwamba hawa walimu wa chuo wanathaminika na wanakubwa na serikali.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, nitakwenda kwenye walimu ambao wanafanya kazi kwa muda mrefu, lakini wengine hawajaajiriwa wanafanya kazi ya kujitolewa kwa muda zaidi ya miaka nane wengine mpaka kumi na mpaka leo hawajaajiriwa. Lakini inatokezea kwamba kuna watu wanaingia ndani ya mwaka tu wanapewa ajira mbio mbio. Sasa hii inaonekana kwamba kuna uwenyeji unapita ama umaarufu unapita, lakini mimi ninachoomba wizara yake ajitahidi kadri ya uwezo wake ahakikishe hakuna ubaguzi na wala habaguliwi, wapewe *priority*, watu wanasomesha miaka kumi hawajaajiriwa mpaka leo wanajitolea.

Hili suala linasikitisha sana na hawa walimu kwa ushahidi wapo wengi na vile vile na yeye mwenyewe naamini kwenye ziara yake ameyaona haya matatizo. Kwa hiyo, ningeomba sana walimu ni watu muhimu sana, walimu wa chuo, walimu wa skuli ni watu muhimu na ni wazee namba mbili, kwani wanalea watoto kwa kadri inavyowezekana.

Mhe. Naibu Spika, sisi tukaa majumbani lakini watoto wetu wanasomeshwa, walimu ndio wana-*take care* kwa wale watoto, sisi hatuna wasi wasi, lakini leo cha ajabu walimu wanawekewa mazonge, hawathaminiki walimu wote kwa ujumla, sio wa skuli wala sio wa vyuo wote, wametupwa tupwa kwa njia yoyote ile. Sasa ningemuomba Mhe. Waziri wa Elimu, ajitahidi sana kukaa na hawa walimu wakatatua matatizo yao hasa wale waliokuwa hawana ajira kwa

muda mrefu, na wale wenye matatizo yao labda ya mambo madogo madogo, vile vile, ajitahidi awatatulie ili waendelee na kazi zao vizuri.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitajitahidi nichangie kidogo kidogo kwa sababu nina mada nyingi na wenzangu wapate kama ulivyosema. Sasa nitakwenda kwenye suala la wanafunzi.

Mhe. Naibu Spika, skuli za Zanzibar karibu asilimia 60 za shamba wanafunzi wanakaa chini hawana madeski ya kukalia. Wanakaa chini ambapo hata saruji wenyewe ina mashimo, wale wazee walioko kule ni wanyonge, masikini, hawana uwezo wanajitahidi kununua unifomu za kuwavalisha watoto wao vizuri, lakini matokeo yake zinachanika na zinaingia uchafu kwa sababu wizara haijakaa ikaamua vizuri kuwatilia *plaster* na kuwawekea mambo mengine. Kwa hiyo, mimi ningeishauri wizara kama haina uwezo wa madeski basi wawanulie japo mabusati kwanza.

Mhe. Naibu Spika, namwambia Mhe. Waziri wa Elimu, mimi kwenye jimbo langu nipo tayari kushirikiana na wizara yako kununua mabusati pamoja na wizara yako inunue ili tuhakikishe yale madarasa yaliyokuwa hayana madeski yawekwe mabusati kwa muda mpaka watakapoletewa madeski ili wasikae chini. Watoto imefikia hatari wamekuwa hawathaminiwi, binadamu sisi, sio kama wanyama lazima tuwathamini hata kama serikali haina pesa isimamishe kujenga maghorofa mjini ya elimu, badala yake ikaweka mabusati na madeski, madarasa ya kusomea yanavuja, mashimo matupu ndani, yaani mwalimu hana sehemu ya kukaa.

Kwa hiyo, mimi ningekuomba sana Mhe. Waziri, mimi binafsi Mwakilishi wa Jimbo la Chaani nipo tayari kutoa ushirikiano na wizara yako kununua japo mabusati ili wanafunzi wasikae chini bila ya kuchafua unifomu zao nao wakajihisi nao wamethaminiwa. Kweli serikali haina pesa ya madeski lakini hata kukunua busati ndio haina pesa!

Mhe. Naibu Spika, mimi ningeomba sana Mhe. Waziri, mkalifikiria hili na ikachukuliwa hatua haraka iwezekanavyo. Vile vile, nataka uje unipe kauli ni lini utasaidiana na mimi kuhakikisha kununua mabusati kwa sehemu ya mwano kwenda kuwapelekea wananchi wangu wa Jimbo la Chaani wakapata kukaa kwenye mabusati badala ya kukaa kwenye mashimo.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitakwenda na suala la wazee ambao wanawatuma watoto wakati wa skuli kwenye mifugo, kuwafanyisha biashara pamoja na wale wanaowatumika mambo ya kuuza njugu na maandazi wakati wanafunzi wale

wanatakiwa kusoma. Mhe. Waziri wa Elimu, ningekuomba sana ukafanya kadri iwezekanavyo kwenye wizara yako ukawaita hawa wazee au ukakamata hawa watoto na wazee wao ukahakikisha kwamba hili suala unalisimamisha kwa sababu watoto wale wanataka elimu, watoto wadogo wanapewa ng'ombe wakabebe maji, wanapewa biashara wakauze samaki wakati suala la elimu ni muhimu kwa dunia ya sasa hivi.

Yale masomo ya miaka ya nyuma aliyefika *form four* mwaka wa nyuma sio *form four* ya sasa hivi, masomo yanabadilika kila siku, ndio maana tukaambiwa elimu haina mwisho. Maana ya kwamba elimu haina mwisho kwa sababu elimu kila siku inabadilika, hizo *computers* zilizotoka mwanzo sasa hivi ziko *failure* zimeingia *computers* mpya, hao wenye *PhD* za zamani na *PhD* ya sasa hivi kuna mambo yamebadilika, ndio maana tukaambiwa elimu haina mwisho haina kikomo, mtu mpaka anakuwa mzee anazoma tu kwa maana hiyo.

Mheshimiwa, ningekuomba sana hawa wanafunzi wote wanaotumwa badala ya kusoma wazee wao wanawatuma kufanya biashara, wazee wale wakakamatwa wakapewa masharti maalum kuliko kuwatuma watoto kwenye masuala ya kubeba maji, kwenda kuuza maji kwa ng'ombe, kupanda punda wakati kunatakiwa elimu, elimu ndio itakayokwenda kuwafaa baadae, itafika hatua miaka ya sasa hivi sawa kuna uwenyeji lakini itafika hatua kutakuwa uwenyeji hakuna tena atatizamwa mtu na elimu yake aliyokuwa nayo ndiyo apate kazi, na hili linaonyesha dhahiri sasa hivi sehemu yoyote unayokwenda kuomba kazi hupewi tu kwa uwenyeji uwenyeji, utaambiwa kwanza una elimu gani, una *certificates* gani ulizosoma ndio upate ile na kazi zote zinazotangwa sasa hivi zinatangazwa kwa mujibu wa elimu ya yule mtu.

Mhe. Naibu Spika, mimi ningeomba sana kwa Mhe. Waziri, hii Wizara yake iko *very sensitive* kwa dunia ya sasa hivi kwa sababu ni mambo ya elimu, ningekuomba sana na Wizara yako mkaangalia hili suala vizuri, masuala haya ya shule mkawapelekea mabusati kwanza badala ya madeski kwa sababu naamini Serikali kupeleka madeski kwa pamoja Zanzibar nzima na Pemba hamuna uwezo kwa sasa hivi. Ningeomba sana mununuwe mabusati na mimi niko tayari kushirikiana na nyinyi Wizara ya Elimu kuwapa mabusati ya Jimbo langu kwanza halafu tukawaletea madeski.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, ningemshauri Mhe. Waziri, akamuombe Mhe Rais Dkt. Ali Mohammed Shein afanye harambee ya kuita matajiri na wafanyabiashara na watu wanaopenda elimu na Wawakilishi vile vile tukahudhuria ikafanywa harambee ya kuchangisha pesa ya madeksi. Mimi ningemuomba sana Mhe. Waziri, hili kamuombe sana hili Mhe. Rais wetu wa

Zanzibar, tunampenda sana na tunajuwa ni mtu wa kazi, tusifanye tu harambee nyengine za kuchangisha changisha mambo mengine, tufanye harambee ya madeski kama wanavyofanya Bara tuone mfano. Mkuu wa Mkoa keshakusanya madeski tele kule Dar-es-Salaam, na kwa nini sisi tusifanye harambee hiyo. Mimi nipo tayari kushiriki kwenye harambe hiyo na sisi Wawakilishi sote tuwemo, Wabunge sote pamoja na Wafanyabiashara wote.

Mhe. Naibu Spika, mimi michango yangu kwa uchache ni hiyo na naikubali hii hotuba yake kwa asilimia 90, asilimia kumi atakapokuja kunitolea maelezo kamili niliyompa nitakuja kuendelea naye. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Nadir, sasa mchangiaji wetu mwengine atakuwa ni Mhe. Mohammedrazza, baada ya Mhe. Mohammedrazza, atafuata Mhe. Asha Abdalla Mussa, baada ya Mhe. Asha Abdalla Mussa atafuta Mhe. Mihayo Juma Nunga.

Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohammedali:Mhe. Naibu Spika, wa Baraza la Wawakilishi. Awali ya yote kwanza napenda kuchukuwa nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutupa pumzi hizi kwa kuweza kufika hapa leo kuja kuchangia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Naibu Spika, mimi nichukuwe nafasi hii kumshukuru Mhe. Waziri na wasaidizi wake wote kwa kuweza kuwasilisha hotuba hii nzuri yenye usikivu, hekma na busara. Mhe. Naibu Spika, nimpongeze Mhe. Waziri, kwa dhati kabisa kwa mwezi huu wa Ramadhani, alipokuja kuanza hotuba yake mbele ya Baraza hili, mbele ya Wazanzibari alianza kwa kusema napenda nimnukuu "*Bismillahi Rahmani Rahhim*" kwa maana ya mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na kuneemesha neema ndogo ndogo.

Sasa Mhe. Waziri, dada angu Mhe. Waziri wa Elimu, hili ni Baraza na ningelipenda kutoa nasaha zangu kwa kwako wewe binafsi ukiwa mdogo wangu, mimi kaka yako uweo na hekma, busara na usikivu na jambo ambalo ulikuwa hulijui au hulifahamu ni bora kila mtu anayesimama umjibu kwa kusema kwamba nipeni muda, mimi bado mchanga nimeingia kwenye Baraza angalau mnipe mwaka mmoja.

Mhe. Naibu Spika, Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar imeshafanya mambo mengi sana nchi hii, elimu, barabara, umeme, maji na mambo yote katika kuwaletea maendeleo na tulifanya Mapinduzi hii kuwaletea wananchi maendeleo bila ya kujali rangi, kabila, dini.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri, nikuombe; Mwenyezi Mungu alipomleta Mtume wetu (*S.A.W*) alimwambia ikra (soma), sasa Mhe.Waziri wa Elimu, Mhe. Naibu Spika, hebu utakapokuja katika kufanya *winding up* katika Baraza lako hili na kwa sababu umeanza kwa jina la Mungu, hebu tuambie Mhe. Waziri wa Elimu, katika maskuli yetu yote ya Unguja na Pemba ni madeski mangapi yanahitajika na gharama zake ngapi na kila deski inasimama kiasi gani, yaani uje utuambie.

Mhe. Naibu Spika, mimi naamini kama nilivyosema Serikali yetu imeshafanya mengi, naamini uongozi bora wa Rais wa Rais Dkt. Shein na Makamo wa Pili wa Rais Balozi Seif Ali Iddi, na sisi tuliokuwepo ambao wenye uchungu na nchi, uwezo tunao, nia tunayo, na tutafanikisha jambo hili. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, Waziri wa Elimu, tafadhali sana utakapokuja utuambie ni madeski mangapi yanayohitajika. Siku nyengine kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu kwa uwezo wa Rais wetu mpendwa Dkt. Shein na kwa uwezo wa Wazanzibari waliokuwa nje na ndani tukalifanikisha suala hili, lakini utupe *statistics* zilizokuwa na uhakika, madeski elfu thalathini, elfu arubaini, elfu hamsini, ili hawa watoto wetu tuwaweze kuwaweka katika hali nzuri. Na Mhe. Naibu Spika, nasema kwa mwezi huu wa Ramadhan, ninavyomjua Dkt. Shein na Balozi Seif Ali Idd na uongozi mzima wa Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar, *inshallah* kwa uwezo wake kabla hatujaingia awamu nyengine ya nane jambo hili nafikiri itakuwa historia kwa Zanzibar, *inshallah* Mungu atusaidie na atupe nguvu ya kufanya hivyo.

Mhe. Naibu Spika, nimuombe Mhe. Waziri wa Elimu, kwamba ahadi za Rais, ninaweza nikasema katika majimbo mbali mbali ni mengi, sasa nikuombe Mhe. Waziri wa Elimu, kwamba kuna sera ilitoka kwamba, wananchi wachangie maskuli Unguja na Pemba katika kuweka ukifika wakati wa mapaa Serikali itabeba majukumu hayo. Ninaweza kuthubutu kusema mbali na Jimbo langu la Uzini, lakini bado kuna majimbo mengine kwa miaka nenda rudi yale mapaa yamekaa kama yanakaliwa na kunguru na ndege.

Sasa Mhe. Naibu Spika, nimwambie tu Mhe. Waziri wa Elimu, namuheshimu sana dada yangu na najuwa ni mtoto wa komandoo, yaani msikivu kwamba, Pagali pale miaka minne iliyopita Mhe. Rais kaja, katoa ahadi ya kumaliza paa. Mhe. Naibu Spika, huyu ni Rais wa nchi, unaposema Rais ni Rais. Sasa ninajua yeye kaja hapa ni mara yake ya kwanza kwenye Baraza, lakini hawa watendaji naona wamemuona kama Rais kauli yake ya kawaida, sasa nawambia watendaji kama hawawezi waache watuachie sisi nchi hii, lakini haiwezi kauli ya Rais wa nchi hii ikafanywa kama kitambara, hawa watendaji wote

wanaohusika wamerejea wale wale, Rais katoa kauli Pagali miaka minne mapaa tu, Rais wa nchi!

Mhe. Naibu Spika, hapa niliuliza mwaka jana mwaka juzi kaambiwa mwaka jana, hawa watendaji wana nia kweli ya kuwasaidia hawa Mawaziri. Maana yake Mheshimiwa, nataka Serikali lazima sasa hivi Mawaziri hawa tuwasaidie sana, kwa sababu huu mtandao ni mkubwa humu ndani katika Mawizara mbali mbali, sasa lazima sisi wananchi. Mhe Naibu Spika, sisi tumekuja hapa kwa niaba ya wananchi, mimi nimekuja hapa na kiti changu hichi cha Uzini kupitia Chama cha Mapinduzi, na sisi sote hapa, hata Rais wetu Dkt. Shein kaingia Ikulu kwa nguvu za wananchi, *alhamdullillahi*, Rais Dkt. Shein pale yupo pale kwa niaba ya wananchi kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi na humu sote asilimia 95 tunatekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Sasa Mhe. Naibu Spika, ninachoomba sasa, nimuombe Waziri wa Elilmu, ahadi zote za Rais, maana Rais huyu anateremka kilima, apande kilima, sasa hatuwezi akaja akaondoka tukaacha magofu. Sasa watuambie Wizara ya Elimu kwamba bwana hizi kauli za Rais kwa mfano Pagali aje aseme tu hapa bwana Razza, hee! huyu Rais kauli yake katoa sisi hatuwezi kuitekeleza, *wallahi*, kesho nitaifanya kazi hiyo, aje aseme humu ndani. Huyu Rais mnampeleka Rais kila sehemu, anatoa ahadi miaka minne mitano, yaani mategemeo yetu sisi ni wananchi. Kwa hiyo, Mhe. Naibu Spika, nasema yale kwa sababu tumefika wakati kuna ahadi nyingi za Rais, kuna ahadi nyingi za Makamo wa Pili wa Rais, na hawa wanazungumza kwa niaba ya wananchi, hawazungumzi kwa niaba ya kikundi.

Kwa hiyo, ningelimuomba Mhe. Waziri wa Elimu, Mhe. Naibu Spika, kwamba tunamuhitaji bado na *in shaa Allah* Mungu akinijaalia ampe uhai na nguvu, Mungu akimjaalia leo ameingia kwenye viti maalum, miaka mitano tutampeleka Jimboni, najuwa kutakuwa na neema kubwa sana Wizara ya Elimu.

Mhe. Naibu Spika, lakini ninachotaka Mheshimiwa, kina mama wanaweza Mhe. Naibu Spika, mimi nakuhakikishia kina mama wanaweza na nataka kumwambia Mhe. Waziri wa Elimu, lugha moja aikamate, aseme kila kitu *you can, you can, you* can, *in shaa Allah* Mungu atampeleka mbali. Lakini kwa kuwa nimemwambia hivyo, kaanza kwa *bismilllahi* ni jambo kubwa sana. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, mimi nimwambie tu na vile vile, kuna suala la Kiboje, ni matumaini yangu yanatekelezwa.

Mhe. Naibu Spika, lakini vile vile nimwambie mbali nilosema kwa Wazanzibari wote kutaka kujua madeski yanayohitajika, lakini kwa kuanzia mimi kwangu Uzini niko tayari kushirikiana na Wizara ya Elimu, maana yake mtu huwasha taa nyumbani halafu huwasha taa nje, nashukuru wananchi wa Uzini, niko tayari kushirikiana na Waziri wa Elimu kwa vyovyote vile kumaliza tatizo la madeski kwa Jimbo la Uzini, kama wao wana milioni kumi na mimi nina milioni, wao wana milioni hamsini, mimi nina milioni hamsini, tunataka watoto wa Jimbo la Uzini wote wamekaa kwenye madeski na niko tayari na skuli zote.

Mhe. Spika, Mhe.Waziri, ninataka nikwambie tu kwamba katika Jimbo langu, maana mtu huulizwa umelifanyia nini Jimbo, mimi Jimbo la Uzini Mhe. Waziri, kwa sababu najuwa hawawezi kukupa kumbukumbu hiyo watendaji wako, nimejenga skuli ya kisasa kuanzia *foundation* Pagali ambayo Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein alikuja akaifunguwa, nikiwa kama Muwakilishi wa Jimbo la Uzini. Isitoshe hapo, nimekwenda Miwani nimefunguwa skuli ya kisasa Miwani *from foundation* mpaka kumaliza ilikuja kufunguliwa na Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar mzee wangu Balozi Seif Ali Iddi.

Mhe. Naibu Spika, Mhe.Waziri, tujaribu tukae pamoja, hili ni letu, Serikali yetu hai hoi. Maana yake Serikali Mhe. Naibu Spika, kinachopata ndiyo kinachotumia, sasa ni lazima *we have to understand.* Lakini Mhe. Waziri wa Elimu, changamoto ya Wawakilishi hawa ni mengi mkaa na maiti haachi kulia lia, sasa hapa sote wananchi tumekuja kwako, nataka uwe mvumilivu, jambo usilolijua, jambo ambalo unaliona gumu waambie wenzako, ndugu zako, dada zako, kaka zako, wazee wako, jamani nipeni muda hili mimi kwangu kwa sasa hivi kilichokuwepo nipeni muda nitakwenda kwa Rais. Nakuomba sana sana Mhe. Waziri wa Elimu, huu ndio ustaarabu, hakuna maana katika mwezi huu wa Ramadhan kila akaja kibabe, suala halipo, mchanganyiko, hakuna nini, kwa hivyo, nafikiri hii kwa mwezi huu mtukufu wa Ramadhani itatusaidia sana.

Mhe. Waziri wa Elimu, kupitia Mhe. Naibu Spika, nikushukuru sana sana, nasema tena nenda kafanye *home-work* uje utuambie madeski ya nchi nzima mahitaji ni mangapi na thamani yake ngapi na kampuni gani. Maana sasa hivi Mhe. Waziri wa Elimu, tuwe wazi, tuwe wazi katika kutekeleza, mtandao mkubwa, unaweza ukaitisha *tender* hapa hiyo *tender* ikawa ghali kuliko hawa *individual people* na nafikiri biashara hii tuwape sasa Wazanzibari, wapo. Kwa hiyo, Mhe. Waziri wa Elmu, ninachokuomba kwamba katika mazingira yote haya ahadi za Rais Mhe. Waziri wa Elimu, hilo halina mjadala katika Baraza hili, tunaongozwa na Rais wetu wa CCM, kwa hivyo, kama kuna watendaji

wako hawataki kuzitambua wa Wizara ya Elimu, hawa watendaji wako, hawataki kuzitambua ahadi za Rais Dkt.Shein, watuachie wenyewe, wasubiri hao watakapokuja kuipata Serikali yao, lakini hawawezi kufika hapa Mhe. Waziri, wakakudanganya.

Mhe. Naibu Spika, nakushauri Mhe. Waziri wa Elimu, kuna tabia ya watendaji huanza kukupa maneno ya kutupa tupa tu humu ndani, Mhe. Waziri, utakuwa na heshima yako, bora uwe na heshima yako, lakini kama jambo hulijui nenda kwenye *site*, mimi Mheshimiwa, hata ukiniambia twenzetu Pagali tutakwenda pale, yaani mabati mia mbili tu *astahfirullahi*, haizidi hata milioni tano, *inallillahi wainnailayhi rajiuun*..

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri wa Elimu, kwakwambia mtu kwamba skuli hii haikaliki nenda kaitizame, lakini usipewe neno na watendaji wako ukaja chini ukaja kuzungumza kitu sicho, sasa kwa kweli hili ni jambo kubwa sana. Kwa hiyo, Mhe. Naibu Spika, niwaombeni Wawakilishi wote tuvumiliane, tujadiliane, ili kukijenga Chama chetu kilichokuwa kimetupa nguvu hapa na mtazamo wa wananchi wote ni Baraza la Wawakilishi, mimi ninasema mwenyewe kwa mwenyewe, kwa hivyo, sasa hivi tuonyeshe kwamba tunaweza kuitekeleza ahadi zote za kuwatumikia wananchi wananchi.

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana nashukuru, ahsante sana Mhe. Waziri, wa Elimu kwa hotuba yako.

Mhe. Naibu Spika: Mchangiaji wetu anayefuata ni Mhe. Asha Abdalla Mussa, samahani, baadae Mhe. Mihayo, naona simuoni, lakini kama itakuwa Mhe. Mihayo, hayupo nitampa nafasi Mhe. Ame Haji Ali, baada ya Mhe. Ame Haji Ali, atakuja Mhe. Mwantatu Mbaraka, wajitayarishe hao.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia Wizara hii ya Elimu. Mhe. Naibu Spika, kwanza na mimi nimpongeze Mhe. Waziri, pamoja na watendaji wake wote kwa kuandaa kitabu hichi cha hotuba ambayo ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka huu wa fedha 2016/2017. Mhe.Naibu Spika, kutokana na muda na wachangiaji kuwa wengi na mimi nitachukuwa muda mchache sana kuzungumzia mammo haya yafuatayo.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitaanza kuchangia kuhusu suala zima la uwajibikaji kwa walimu pamoja na wanafunzi. Mhe. Naibu Spika, tunafahamu kwamba watoto wetu wanapata elimu na elimu bila ya walimu basi hawawezi kupata elimu bora.

Mhe. Naibu Spika, uwajibikaji wa walimu katika mahudhurio wakati mwengine katika maeneo mengine yanakuwa ni madogo.Utakuta wanafunzi wapo tu mitaani wanaradha, ukiuliza walimu hawapo wa kusomesha, hususan katika maeneo yetu ya vijijini.

Mhe. Naibu Spika, kuna baadhi ya walimu wengine wanatoka maeneo mbali mbali, lakini kufika katika eneo la skuli muda unakuwa mkubwa, kipindi chake kiko saa mbili basi skuli anafika saa sita na ikifika saa saba na nuzu mwalimu anaondoka. Mhe. Waziri, suala hili naomba ulitizame kwa kina kwa sababu mwanafunzi unapofika wakati wa kufanya mitihani yake anashindwa kufanya mtihani kwa sababu somo lile halifahamu na hajawahi kufundishwa hata mara moja.

Mhe. Naibu Spika, lakini kuna baadhi ya walimu wengine wanaacha kusomesha masomo waliyopangiwa wanaenda kuhutubia siasa ndani ya madarasa. Mhe. Waziri, haya masuala yapo na ya uhakika na tunauhakika nayo. Kuna baadhi ya walimu kazi yao kusomesha siasa katika madarasa. Tunakuomba Mhe. Waziri, ulifuatilie kwa kina ili waweze kuwajibishwa walimu hawa.

Mhe. Naibu Spika, lakini kuna masuala ya posho la nauli ya walimu. Walimu wetu wengi wanatoka sehemu mbali mbali wanafata kazi zao katika vijiji, yaani anaweza kutoka mjini lakini anasomesha Matemwe, lakini ikifika wakati wa kulipwa posho lake halipati ipasavyo na kuna malalamiko walimu wengi sasa hivi inaweza ikafika miezi sita hawajapewa maposho yao ya nauli. Tunaomba Mhe. Waziri, ufuatilie kwa kina, hivi kuna walimu baadhi yao walitaka kufuata moja kwa moja, lakini wametuomba tuwasemee katika Baraza.

Mhe. Naibu Spika, kuna ukosefu wa walimu wa sayansi, naomba wizara hii ipange mkakati maalum ili iweze kuajiri walimu wa sayansi na wafike katika maeneo mbali mbali katika skuli zetu, ili wanafunzi waliofaulu masomo ya sayansi basi waweze kuendelezwa na wao waweze kuja kutusaidia baadae.

Mhe. Naibu Spika, kuna kesi nyingi zinajitokeza kwa wanafunzi wetu ambao wengine wako karibu na mitihani, lakini wengine utakuta mwanafunzi yuko darasa la tano au la sita, ni mwanafunzo mdogo lakini anachukua ujauzito na baadae wazazi wanamuozesha mtoto yule anakatishwa masomo. Namuomba sana Mhe. Waziri, tuwaige wenzetu wa Tanzania Bara tufuate ile elimu ya kwamba, mwanafunzi yeyote hata akikutikana mjamzito basi aweze kuendelea na masomo yake.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala jengine nimuombe Mhe. Waziri, kuna vituo vimeanzishwa vya "Tucheze Tujifunze".Vituo hivi viko katika maeneo mbali mbali, katika jimbo langu la Kiwengwa kuna vituo vinane, lakini cha kusikitisha kuna walimu ambao wanajitolea kuwasomesha watoto wetu, walimu hao mwaka wa pili sasa hawajapewa sabuni zao. Namuomba Mhe. Waziri, ashirikiane na wenzake ili waone walimu hawa wanapewa sabuni zao. Kwa sababu wengine imefikia pahala wanasema kwamba, waume zao wanasema wasipopewa mishahara mwezi huu basi wasiende tena kusomesha watoto. Mhe. Waziri, namuomba achukue suala hili ili tuone kwamba watoto wetu na wao wanapata elimu ya maandalizi.

Mhe. Naibu Spika, naliomba suala jengine la mwisho au nipendekeze kwenye wizara hii. Kwa kuwa sasa hivi vijana wengi hawana maadili na hawajui historia yao ya Zanzibar, napendekeza kwamba somo la Historia lirejeshwe skuli. Mhe. Waziri, namuomba sana na ninapendekeza somo hili lirejeshwe skuli ili wanafunzi waweze kufahamu wapi tulikotoka, wapi tulipo na wapi tunakokwenda.

Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa muda huu, lakini pia nasema niungane na wenzangu kwa kuwa watu wengi hawajachangia na wizara hii ina watu wengi na kila mtu ana jukumu la kuwatetea wanafunzi pamoja na walimu wetu walioko katika majimbo yetu. Nikushukuru sana na mimi naungana na wenzangu kwa kuunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja, ahsante.

Mhe. Ame Haji Ali: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniamsha asubuhi hii nikiwa katika hali ya uzima na salama. Kwa kuanza mchango wangu kwanza natanguliza kumshukuru Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, pamoja na watendaji wake wote kwa mashirikiano makubwa sana waliotupa wakati kamati yangu inapitia hotuba hii.

Kwa hiyo, kwa kuwa mimi nilikuwa miongoni mwa walioipitia hotuba hii natanguliza kusema kwamba, naiunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Hata hivyo, kutakuwa kuna maeneo ambayo nami niongezee kati ya yale ambayo tumeyaona katika kuipitia hotuba hii. La kwanza, niende moja kwa moja katika upungufu wa walimu. Eneo hili ni eneo ambalo linahitaji litizamwe kwa jicho la huruma, tulipokuwa tunapitia hotuba waziri na watendaji wake walitwambia kwamba mwaka uliopita 2015/2016 waliomba walimu 942, lakini kwa masikitiko makubwa mwaka mzima walipata walimu 90.

Sasa mimi niiombe sana serikali hasa kupitia watu wa utumishi, jamani tuliangalie jambo hili kwa upana na ukubwa wake. Kwa sababu tutalaumu matokeo kuwa mabaya kumbe wanaoyafanya matokeo haya yawe mazuri hatujawapa nafasi ya kuwaajiri. Kwa hiyo, mimi nawaomba sana wa utumishi wawatizame kwa jicho la huruma watu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa sababu naona pia katika mwaka huu wamerejesha hesabu hiyo, basi angalau kutoka 900 wapate japo 300 ili walimu hao waje wakawasaidie watoto wetu kule maskulini.

Eneo la pili ambalo nataka kulitizama kwa leo kutokana na muda italazimika niende haraka haraka ni eneo la mikopo hasa kwa hawa wanafuzni wetu wa elimu ya juu. Mhe. Naibu Spika, eneo hili nalo niiombe sana serikali, kwa kuwa Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango yupo pale niwaombe sana, watoto wetu hawa wanaosoma katika elimu ya juu wanapata tabu sana katika maeneo wanayosoma.

Hivi karibuni tulikuwa tuna mazungumzo na wanafunzi wa Vyuo Vikuu waliopo Zanzibar katika kamati yangu, Mheshimiwa, ukiwasikiliza yale masikitiko yao na matendo yanayotokana na kukosa mikopo hii kwa wakati kama wazazi inasikitisha sana. Sasa mimi niiombe serikali kwa dhati kabisa Mhe. Waziri wa Fedha, yupo pale anatusikia tujitahidi kadri tuwezavyo hii mikopo watiliwe hawa wizara ili wanafunzi waipate kwa wakati ili nao waendeleze kile ambacho wamekusudia kukiendeleza nacho ni kutafuta elimu bora.

Mhe. Naibu Spika, niende haraka katika michango yangu, lakini eneo jengine ambalo nataka nilisemee leo ni hili ambalo Mhe. Waziri, aliingiza katika hotuba yake akasema kwamba, katika mwaka huu wa fedha anakusudia kumaliza madarasa 120 yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi. Mimi nasema haya madarasa ni kidogo sana, kwa sababu wananchi wamehamasika na wako tayari kujitolea kujenga na wanahitaji madarasa yao yamalize, lakini tunakubaliana kwamba hiyo ndiyo hali halisi ya uchumi wa nchi yetu, lakini tujitahidi pia kutafuta vipaumbele katika kumaliza.

Mheshimiwa wa jimbo la Chaani aliposema alisema tusizame mjini, mashamba pia turudi tutizame. Sasa Mhe. Waziri, kwa heshima sana mimi binafsi namuomba kwamba skuli yangu ya Bwereu ikamaliziwe. Wale wananchi wamefanya juhudi kubwa, lile banda limekwisha kwa muda mrefu sasa, namuomba sana katika 120 mimi yangu madarasa manne wala sio mengi sana. Kwa hiyo, tumaliziwe pale ili tuone kwamba zile jitihada ambazo wamefanya wale wananchi pale tumewasaidia.

Eneo jengine ambalo nataka kulichangia ni eneo la matokeo mabaya ya mitihani hasa katika wilaya zetu. Mhe. Naibu Spika, wilaya inayoongoza kwa matokeo mabaya ni ya Kaskazini "A", kwa bahati mbaya sana nafasi zetu miaka yote ni ya tisa, tukitoka ya tisa inakuwa ya kumi. Ni matokeo mabaya sana, mimi binafsi nimekuwa nikijaribu kuangalia sababu zinazotupelekea matokeo haya kuwa mabaya ni nini, hivi watoto hawataki kusoma au nini ambacho kinapelekea hivi. Lakini baadhi ya mambo ambayo nimeyagundua ni haya ambayo nitayasema kwa mawazo yangu.

Jambo la kwanza, ni hili la upungufu wa walimu. Katika eneo ambalo linaongoza kwa upungufu mkubwa wa walimu ni Wilaya ya Kaskazini "A", nimejitahidi kujaribu kupitia skuli nyingi zilizo katika eneo lile lakini nimeona upungufu wa walimu ni mkubwa sana na kinachofanyika ni kwamba wizara inajitahidi kuleta walimu Kaskazini. Lakini Mheshimiwa, mwalimu anaweza akaja wiki moja na haimalizi anaondoka na hakuna sababu. Kwa hiyo, leo utakwenda kupokea mwalimu haijamaliza wiki utakapokwenda mwalimu mkuu anakwita anakwambia mwalimu yule kaondoka na sababu hazijulikani. Kwa hiyo, Mhe. Waziri, eneo hili liangaliwe kwa upana Kaskazini tuna upungufu mkubwa sana wa walimu na hiki ndicho kinachopelekea matokeo yetu mara nyingi yakawa mabaya.

Mhe. Naibu Spika, eneo jengine ambalo linapelekea matokeo kuwa mabaya ni walimu wetu kukosa sana maadili. Mhe. Naibu Spika, sasa badala ya kufanya kazi ya kusomesha elimu tulizowapangia walimu wanaingia madarasani kusomesha siasa, limekuwa ni jambo baya ambalo linawavunja moyo hata wazazi na ukiona mashirikiano yanakosekana miongoni mwa walimu na wazazi ni katika eneo hili.

Mhe. Waziri, namuomba sana ashushe timu yake katika maskuli waende wakakemee jambo hili, walimu wetu wasomeshe kama kazi ambayo wamepewa, sio wakasomeshe siasa, wakifika mahali wakiamua kuja katika siasa wasubiri wakati ukifika wa siasa waje majukwaani tunawasubiri kwa dhati kabisa, waache kazi ya kusomesha waje majukwaani tunawasubiri tutangaze siasa tuendelee mbele. Lakini kama tumewapa kazi ya utumishi basi kwanza watusomeshee watoto wetu ili yale tuliyokusudia yawe yana mafanikio.

Kwa hiyo, Mhe. Waziri, namuomba sana na timu yake eneo hili nalo lipewe kipaumbele na ashuke chini aangalie walimu wetu hawa wafanye kazi ile ambayo tumewapelekea kwa matokeo mazuri ya watoto wetu. Watoto hawa

wako tayari na wasikivu sana, lakini wanakosa uzalendo wa walimu kutoshughulikia.

Jambo jengine ambalo labda nimalizie tu kutokana na muda ni suala la Vyuo vya Amali. Mhe. Waziri, katika eneo la Vyuo vya Amali tunahitaji msukumo mkubwa sana, inawezekana wazazi au jamii yetu haijaifahamu hii dhana nzima ya elimu ya amali na ndio maana tunapata upungufu mkubwa wa wanafunzi na hata wale wanaokwenda wanakwenda kama kwa kulazimishwa hivi. Kwa hiyo, eneo hili tunahitaji turudi sasa chini tutoe taaluma na tuelekeze hasa maana ya hii elimu ya amali ni nini na ujasiria mali ni nini, ili wanafunzi wetu hawa tupunguze msongamano wa kusubiri ajira serikalini. Serikali hii haina uwezo wa kumuajiri kila mtu lakini tutie mkazo katika eneo hili.

Katika eneo hili pia tuendelee kutafuta wafadhili ili wale wanafunzi wanapomaliza mafunzo yao pale basi waanze kupata mitaji ya kuanzia kazi, hata kama kwa mikopo, lakini ni vyema wanapomaliza kujifunza pale wawe wameondoka pale na ujuzi lakini pia wawe wameondoka pale na mtaji ambao utawawezesha waanze kufanya kazi zile ambazo wamejifunza.Tukifanya hivi kwa jitihada hizi nadhani tutakuwa tumepunguza sana tatizo hili la kusubiri ajira serikalini.

Eneo la mwisho ambalo leo nataka kulichangia ni eneo la ukosefu wa vifaa. Wajumbe waliotangulia wamesema lakini Mhe. Waziri, nataka niseme kwamba upungufu wa vifaa maskulini ni mkubwa sana hasa madawati. Mimi nimepitia skuli nyingi lakini nitoe mfano mmoja tu mdogo Skuli yangu ya Nungwi nina madarasa 10 hamna dawati hata moja na nyengine hivyo hivyo. Sasa niiombe serikali kupitia zile taasisi ambazo zinatusaidia za binafsi na hata za serikali zijitahidi kulitizama eneo hili ili watusaidie madawati watoto wetu wanakaa chini sana kitu ambacho kinapunguza uwezo wao wa kujifunza vizuri.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa tuko wachangiaji wengi na mimi nimepata nafasi ya kupitia hotuba hii kabla, narudia tu kusema kwamba naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja na nawaomba wajumbe wote tuipitishe ili tuwape kazi watumishi wetu hawa wakaifanye kwa niaba yetu. Ahsante sana Mheshimiwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis: Mhe. Naibu Spika, ahsante na mimi kwa kunipa fursa hii asubuhi hii ya leo nikawa ni miongoni mwa wachangiaji wa hotuba hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu (*S.W*) ambaye ameniwezesha na kunipa pumzi za kuweza kusimama hapa. Lakini pili nimpongeze Mhe. Waziri, pamoja na Naibu Waziri na watendaji wake wote kwa kuweza kufanya kazi nzuri na hatimaye wakaweza kutuwasilishia hotuba hii katika Baraza letu hili.

Mhe. Naibu Spika, katika hotuba hii mimi nianze kuchangia kipengele cha Huduma za Maktaba. Maktaba zipo na zinaimarishwa kwa ajili kuwawezesha wanafunzi na watu wengine kuweza kujisomea na kupata taarifa mbali mbali ambazo zinawapatia uelewa wa mambo mbali mbali katika kufanya shughuli zao.

Mhe. Naibu Spika, hotuba hii ya Mhe. Waziri, ilieleza kuwa kuna jumla ya vitabu 3,826 cha masomo mbali mbali ambavyo vimesambazwa katika maktaba zetu hizi. Nimuombe Mhe. Waziri, katika hili aje anieleze katika vitabu hivi ni vitabu vingapi vya *Braille* ambavyo wanatumia wasiyoona vimesambazwa katika maktaba zetu ili na wanafunzi wale wenye mahitaji maalumu na wao waweze kufaidika na huduma hizi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, sasa nije katika programu ya elimu mjumuisho na stadi za maisha. Nianze na kipengele cha nne katika kitabu hiki ambacho kimezungumzia kwamba kuna vifaa vya kufundishia na kujifunza wenye mahitaji maalumu vilipatikana.

Mhe. Naibu Spika, ili mwanafunzi aweze kujifunza kunahitajika vifaa vya kutosha kama ni nyezo kuu za kumuwezesha kujifunza mtoto au mwanafunzi mwenye mahitaji maalum. Katika hotuba hii imeonesha kuwa vifaa hivi ambavyo vimeelezwa katika kifungu cha nne vimepatikana kutoka *ZANAB* ambayo ni Jumuiya inayojitegemea ya Walemavu Wasiyoona na kutoka *ZANTEL*, *ZANTEL* pia ni kampuni. Hapa nimuulize Mhe. Waziri, kwamba ni vifaa vingapi na vya aina gani ambavyo wizara yenyewe kama ndio yenye jukumu la kuhakikisha watu wote wanapata elimu sawa wameweza kununua kwa lengo la kuwaondoshea vikwazo wanafunzi wenye mahitaji maalum pamoja na walimu wao.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo nije katika vipaumbele vya wizara. Katika kitabu hiki miongoni mwa vipaumbele vya wizara kimeeleza kuwa kutajengwa skuli 10 za ghorofa na madarasa 120 yatakamilishwa. Kwa hili namuomba Mhe. Waziri, katika kujenga majengo haya kuzingatiwe mahitaji ya watu wenye ulemavu. Kwa sababu majengo mengi hivi sasa hata yale ya umma ambayo tunategemea serikali itasimamia ili kuwawezesha watu wote waweze

kuyatumia basi hayafikiki. Kwa hiyo, kwa hizi skuli ambazo zinajengwa tunategemea, kuna walimu wanaofundisha wenye ulemavu, lakini vile vile kuna wanafunzi wenye ulemavu watahitaji kuzitumia, basi hili suala la kuzingatia mazingira rafiki iwe ni kipaumbele katika wizara hii.*(Makofi)*

Miongoni mwa kuboresha hayo majengo mbali na ufikikaji wa majengo hayo kuweka mitelezo katika majengo hayo. Tunapoweka mtelezo tutamuwezesha hata yule mwenye kibaskeli chake cha magurudumu mawili akaweza kujiendesha mwenyewe bila ya kumtegemea mtu mwengine. Kwa hiyo, ataweza kuingia na kutoka katika majengo yale bila ya vikwazo vyovyote.

Lakini chengine ni milango inayojengwa katika majengo haya ambayo tunategemea hawa walimu wenye ulemavu na wanafunzi wenye ulemavu kutumia basi angalau tuifanye ni mipana ambayo itamuwezesha hata kama akiingia kwenda kujisaidia aende mwenyewe bila ya kutegemea mtu mwengine, kumpeleka na kama tunavyojua mazingira ya watu wenye ulemavu wengine wanakwenda kwa mikono.

Kwa hiyo, mlango utakapokuwa mpana ataweza kuingia na kifaa chake au baskeli yake mle ndani na mwenyewe akaweza kugeuza akafanya haja zake bila ya kutegemea msaada kwa mtu mwengine. Vyenginevyo, milango inapokuwa membamba mtu yule inabidi aweke kigari chake nje na aanze kutembea kwa mikono kuingia katika sehemu ya kwenda kujisaidia hali ambayo kwa mtu yeyote hawezi akaifanya isipokuwa anafanya tu kwa vile mazingira yamemplekea kufanya vile. *(Makofi)*

Lakini vile vile vyoo ambavyo vinajengwa katika majengo haya vizingatie kwamba kuna watu wenye ulemavu ambao wanahitaji vyoo maalum. Sio kila choo tu mtu anaweza akatumia. Kwa hivyo, nikuombe Mhe. Waziri, kwa unyenyekevu mkubwa ulichukulie hili na kwa vile nakuelewe naamini utalifanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, nije hapo hapo katika Elimu Mjuisho na *Study* za Maisha. Programu hii ya Elimu Mjumuisho ina lengo la kutoa Elimu Jumuishi kwa wote wakiwemo wenye mahitaji maalum.

Kwanza niipongeze wizara kwa kuweka au kwa kuanzisha kitengo hichi. Mhe. Naibu Spika, kuanzishwa kwa kitengo hichi wanafunzi wenye ulemavu pamoja na wazazi wao walifarajika sana wakaona kwamba sasa hivi kuna chombo ambacho tutaweza watu wenye ulemavu tukajivunia na tukapata ile elimu ambayo tunaikusudia kutoka na mazingira tofauti ambayo tulikuwa

tukikwazana nacho. Mhe. Naibu Spika, imani ikatupeleka kwamba Elimu Mjumuisho itakuwa ni mkombozi wetu.

Mhe. Naibu Spika, kiliponzishwa tu kitengo hichi kulikuwa na skuli ambazo zilikuwa kama skuli za majaribio. Skuli hizi zilitekeleza moja kwa moja programu hii, lakini hivi sasa skuli hizi kusema la ukweli mazingira yake hayaridhishi na ile elimu ambayo tulitegemea watu wenye ulemavu tuipate katika skuli ile haipatikani. Kusema ukweli skuli hizi zimetupwa hazipati zile huduma au vifaa vya kuwawezesha watu wenye ulemavu au wanafunzi wenye ulemavu waweze kujifunza vizuri.

Naiomba wizara kukiimairisha kitengo hichi cha Elimu Mjumuisho kwa sababu bado wanafunzi wenye ulemavu na wazazi wao wanailalamikia elimu hii kwa namna inavyotolewa. Mhe. Naibu Spika, kuna mifano hai kuna mwanafunzi mwenye ulemavu anasoma msingi anaweza akapata mwalimu wa kumsomesha ambaye ana uwezo, lakini anapokwenda Sekondari anakuwa hapati yule mwalimu na matokeo yake yule mwanafunzi anakwenda kule skuli kupeleka wenziwe na kurudi nyumbani. Kitendo ambacho kinavunja moyo na wanafunzi wenye ulemavu wanavujika moyo na kusindwa kuendelea na masomo na kukosa hii haki muhimu ya elimu.

Mhe. Naibu Spika, ombi langu kwa Mhe. Waziri, kukiongezea bajeti kitengo hiki ili kukiwezesha kufanya kazi zake kwa ufanisi na kuteleta maendeleo kwa wanafunzi wenye ulemavu. Lakini vile vile niiombe wizara ifanye jitihada za makusudi kuhakikisha wanapata walimu wenye sifa za kufundisha wanafunzi wenye ulemavu ili kuondha hiyo kero ambayo ipo hivi sasa.

Mhe. Naibu Spika, sasa nizungumzie hukusu Sera ya Elimu Mjumuisho. Imeelezwa katika kitabu hiki kwamba Sera ya Elimu Mjumuisho tayari imeshatayarishwa lakini inahitaji michango zaidi.Ombi langu ni kwamba inapopelekwa ili kuboreshwa hii sera au kujengwa ni vyema vikashirikishwa hizi jumuiya za watu wenye ulemavu ili na wao wakaweza kutoa michango yao ya kuweza kuiboresha au kuijenga sera hii.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na ukosefu wa walimu wa lugha za alama kitendo ambacho kinawasababishia wanafunzi wenye ulemavu wa uziwi kukosa hasa ile elimu inayotakikana. Niishauri wizara ishirikiane na Taasisi ya Elimu ya Juu kuanzisha elimu ya kiwango cha digirii ya elimu maalum pamoja na ukalimani wa lugha ya alama.

Baada ya michango hiyo na mimi niungane na wachangiaji waliotangulia kuunga mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri, kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Naibu Spika, na mimi niungane na wenzangu kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia afya na uzima, wengi walitamani kufika siku ya leo, lakini kwa matakwa yake *Subhana wataala* hawakufika na neema hiyo wametupa sisi tukaungana hapa ili kuendelea na majukumu yetu ya kawaida. Kwa hiyo, ni jambo la kushukuru.

Lakini pili nikushukuru Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii kuchangia hotuba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali ambayo ameiwasilisha na nampongeza waziri kwa uwasilishaji wake mzuri, kawasilisha kwa ufasaha, hii ndio raha ya kuwapa nafasi vijana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kwa kuthibitisha hilo hata Mhe. Rais wa Jamhuri anakubaliana na hilo, amewapa nafasi vijana wanamchapia kazi na yeye mwenyewe ana-*appreciate*.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuanzia naomba nizurungimzie suala la Elimu ya Juu na nitagusia *specific* katika huduma ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Mhe. Naibu Spika, kuna matatizo mengi katika mkopo wa SMZ ambao vijana wanaendelea na elimu zao wanakumbana na changamoto nyingi sana kiasi ya kwamba gurudumu la elimu ambalo wanajaaribu kulisukuma mbele linarudi nyumba.

Mhe. Naibu Spika, nina maoni ya wanafunzi hapa ambao wameniwasilishia niwafikishie kwa Mhe. Waziri, na ni mengi kabisa siwezi kusoma yote. Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba ninukuu machache na naomba uniruhusu baadae nimkabidhi hii karatasi Mhe. Waziri na kamati yake ama na timu yake ili waweze kukaa na kuyapitia na kuona watakuja na majibu gani. Lakini pia kuona watayafanyia kazi vipi changamoto hizi.

Mhe. Naibu Spika, haraka haraka naomba nisome changamoto ya kwanza kwa ruhusa yako naomba kunukuu:-

(1) Kutopewa pesa za kujikimu kama mkataba unavyoeleza kwani tokea tunaaza chuo mpaka leo hatujapewa pesa hizo kwa wakati na kwenye mkataba zimo.

(2) Changamoto ya pili kuulipia mkataba kwa kila mwaka wakati sisi ni masikini na kiwango cha kulipia mkataba huo kila mwaka ni kikubwa kwa mwanafunzi wameandika (elfu thalathini na tano).

(3) Wanafunzi hatushirikishwi ipasavyo katika bodi ili kuwaelezea changamoto zetu.

Mhe. Naibu Spika, kwa ku-*save* muda naomba nimalizie hapo. Lakini nitamkabidhi Mhe. Waziri, karatasi hii ili aone kwamba ni kiasi gani anazifanyia kazi changamoto hizi.

Mhe. Naibu Spika, mimi katika hili pamoja na kuwa nawazunguzia wanafunzi kwa ujumla, lakini *concern* yangu ipo katika wanafunzi wa kike. Mhe. Naibu Spika, huu mkopo unawaweka ndugu zetu katika njia panda. Mtoto wa kimasikini ametoka kwa kutoka Kizimkazi huko baba na mama wameshauza ngombe anakuja kusoma, lakini pia kile kidogo alichokipa huko anategemea mkopo wa SMZ utamuengezea katika elimu yake, lakini watoto wanakaa muda mrefu sana hawapati mikopo na hii inapelekea watoto wa kike kudhalilika, wanapita wakiomba, ataomba mara ya kwanza, ya pili, ya tatu, mara ya nne ataombwa yeye.

Mhe. Naibu Spika, mnatudhalilishia wanafunzi ama watoto wa kike ambao wako katika vyuo, na hili kuonesha kwamba hata halipewi kipaumbele katika wizara haijaonesha kabisa ni wanafunzi wangapi wa kike wamepata mikopo ya elimu ya juu na wala haijaonesha ni jumla ya wanafunzi wangapi wamepata mikopo. Kwa hiyo, mimi *concern* yangu namuomba Mhe. Waziri, akija hapa atuelezee hapa katika idadi ya mikopo waliyotoa ni asilimia ngapi na idadi ya wanafunzi wangapi wa kike wamepata mikopo hii.

Jengine Mhe. Naibu Spika, nalizungumzia hili kwa sababu nina wasi wasi kwamba kama ile dhamira ya serikali kutaka kuwasaidia wanafunzi hawa ni ya kweli. Kwa sababu Mhe. Naibu Spika, ukiangalia katika bajeti ya mwaka jana jumla ya wanafunzi ilikuwa ni asilimia 25, serikali ilitenga bilioni nane milioni mia mbili hamsini na tisa kwa ajili ya mikopo. Lakini mwaka huu ambapo asilimia imepanda imekuwa thalathini, lakini serikali imetenga bilioni sita milioni mia moja kumi na tisa na elfu tisini kwa ajili ya mikopo hii. Sasa nina wasi wasi *demand* imepanda lakini fungu la fedha limeshuka.

Mwaka jana ilipokuwa *demand* ndogo fungu limeweka kubwa, sasa nina wasi wasi kama kweli serikali ina dhamira ya kutimiza hili na naona kabisa bado watoto wa kike wanafunzi wataendelea kudhalilika. Mhe. Naibu Spika, watoto wa kike mahitaji mengi, kuna mambo mengi wanahitaji ambayo wakiwa hawapati hizi pesa za kujikimu basi inawapelekea kufanya mambo mengine ambayo hawakupaswa kufanya na baadae kuwapelekea kupata matatizo mengine na kushindwa kuendelea na elimu zao katika vyuo.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia katika hili naomba kupongeza sana wale ambao wamepata mikopo, kwa sababu ukusanyaji wa mikopo ama urejeshwaji wa mikopo inaonesha imepanda. Lakini pia nichukuwe fursa nitoe wito kwa wale ambao walipata kukopeshwa hizi pesa hazitolewi bure. Mhe. Naibu Spika, niwaombe sana wale wanaopata mikopo wachukuwe jitihada za kurudisha mikopo hii ili na wenzao wengine waendelee kunufaika na mfuko huu ama na mikopo hii ambayo inatolewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo naomba nizungumzie Elimu Mbadala na hapa nitagusia katika Programu ya Mafunzo ya Amali. Mhe. Naibu Spika, kwanza niipongeze serikali kwa kuona umuhimu wa vyuo hivi na nimeangalia uingizwaji wa pesa katika vyuo hivi umekuwa mzuri sana hadi kufikia asilimia 76. Pamoja na kwamba mara hii kumekuwa na upungufu kidogo wa uingizwaji wa fedha ambazo zimetengwa, lakini upungufu ule sifikirii kama utaathiri sana kwa sababu ni wa asilimia ndogo sana.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana wizara imekiri kwamba kuimarika kwa vyuo hivi ni kupunguza tatizo la ajira kwa vijana. Mhe. Naibu Spika, hivi sasa kuna wimbi kubwa la vijana ambao hawana ajira kuna wanaoishia kidato cha pili, cha nne na kuna pia wanaoishia kidato cha kumi na sita.

Mhe. Naibu Spika, vikosi haviwezi vikachukuwa watu wote ambao wanafeli, ama wanaishia masomo yao katika *level* ya chini. Hivyo, niombe serikali sana iendelee kuimarisha Vyuo vya Amali kwa sababu watakaokosa kuingia katika Vikosi ambapo siku hizi wananchi wamejengeka kwamba, ukifeli unakwenda vikosi na ndio maana siku hizi tunakuwa na askari ambao hawana adabu, adabu huko nje wanafanya wanavyotaka wao.

Sasa Mhe. Naiabu Spika, ku-*challenge* hili naomba sana serikali iimarishe Vyuo vya Amali ili kuona kwamba wale ambao wana-*drop out of school, at least* wanakuwa *covered* katika hivi Vyuo vya Amali.

Lakini jengine Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa serikali imekiri kwamba hivi Vyuo vya Amali vinasaidia sana kupunguza ajira na kwa kuwa hotuba ya Mhe. Waziri, amesema kwamba hivi sasa imeeleza kwamba viaashiria vya Programu hii moja ni kupunguza ukosefu wa ajira kwa vijana kutoka kiwango cha asilimia kumi na 19.6 kwa mwaka 2009 hadi kufikia asilimia 11.4 ifikapo 2017.

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri, akija kutoa maelekezo hapa anieleze, nilitaka kujua kwamba hivi sasa asilimia ni ngapi kabla ya kufikia

hiyo 2017 na Vyuo hivi na kwa mwaka jana vilisaidia kiasi gani kushusha ukosefu wa ajira kwa vijana katika nchi yetu.

Jengine Mhe. Naibu Spika, miradi ya Wizara ya Elimu. Kwa kweli katika hotuba ya Mhe. Waziri, miradi ya Wizara ay Elimu haikuelezewa sana, isipokuwa imeelezwa kidogo tu, yaani kama imetajwa ile miradi, lakini pia kuna jaduweli ambalo limeonesha tu uingizwaji wa fedha za miradi ile.

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nataka kujua kulikuwa na mradi wa kujenga Vyuo vya Amali, sina uhakika sana kama ulikuwa unafanywa na SMZ au na wafadhili. Lakini kuna mradi wa kujenga Vyuo vya Amali ilikuwa unafanywa katika kila mikoa, nilikuwa nataka kujua *progress* ya mradi huu umefikia wapi, ile dhamira ya serikali kuona kwamba Vyuo vya Amali vinasaidia kushusha ukosefu wa ajira kwa vijana inafikiwa.

Kwa hiyo, nataka kuomba Mhe. Waziri, akija anambie mradi ule umefikia vipi. Lakini pia kuna miradi mbali mbali ambayo ilikuwa inaendelea hivi sasa haijatajwa na wala haijaelezwa katika hotuba ya Mhe. Waziri, na wala katika majaduweli huku nimejaaribu kutizama hamna kitu. Kuna mradi wa TZ 2021 nilikuwa nataka kujua umefikia wapi.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo, najua kwamba serikali imejipanga kuletwa mswada wa SUZA. Lakini kulikuwa kuna kitu kimoja ambacho nilikuwa nataka kuomba kwamba, Chuo cha SUZA kianzishe Vitivo ama *Faculties* tofauti ili Vyuo vyengine kama vile Chuo cha Uongozi wa Feha na Chuo cha Maendeleo ya Utalii vibaki kama vilivyo. Kwa sababu Vyuo hivi Mhe. Naibu Spika, vimekuwa vikifanya vizuri na maendeleo yake mazuri. Kwa hivyo, hivi Vyuo tungeomba sana visiwekwe chini ya *umbrella* ya *SUZA* na badala yake vingeachwa kama vilivyo, *instead SUZA* ingeanzisha *faculties* nyengine ambazo ingeweza kuwa- ac*commodate* watu wa fani nyengine, ili tuwe na vyuo mbali mbali katika nchi yetu ambavyo vingeweza kutoa elimu kwa vijana wetu tofauti.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo nina mengi lakini mengine nitampelekea Mhe. Waziri, kwa maandishi, na nisema kwamba ninaunga mkono hotuba hii ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali. Lakini kama nilivyosema kuwa Mhe.Waziri, ninamuamini, ni kijana mwenzangu, tumetoka sote katika au ninasema tumeokwa katika tanuri la uongozi kwenye chama chetu. Kwa hivyo, ninamuaminia sana. Hivyo, si-*expect* akija hapa ani-*let down*.

Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Wanu Hafidh Ameir. Waheshimiwa, kabla ya kuendelea naomba kidogo tuwatambue wageni wetu waliofika hapa. Na wageni wenyewe ni wa Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy ambaye ni Mwakilishi wa Chaani.

Wageni wenyewe ni Bwana Ismail Saffu ambaye anatokea Uturuki, Bwana Al-Akuu kutoka Uturuki na Bwana Aley Hoja Haji kutoka Nungwi. Naomba msimame msalimie, kwa hivyo, *you are very welcome*. Ahsante sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea na wachangiaji wanaofuata ni Mhe. Ali Khamis Bakar, baadae atapata nafasi Mhe. Rashid Makame Shamsi, baada ya hapo atakuja Mhe. Zaina Abdalla Salum na anayefuata mwengine ni Mhe. Said Omar Said.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipa nafasi kuweza kuchangia machache. Na mimi niungane na wenzangu kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha siku ya leo tukakutana hapa tukiwa wazima na pia atujaalie saumu zetu zetu *makbul, inshaallah.*

Mhe. Naibu Spika, mimi mchangu wangu leo nitaanzia kwenye sekta yetu hii ya madarasa haya tuliyoanzisha ya TUTU. Mimi kwanza niishukuru wizara kwa kuliona hili jambo ikaweza kulianzisha ni jambo zuri. Na niwashukuru tu watendaji wa sekta hii ya elimu kuona kwamba kule majumbani kwetu wale watoto wetu hawakai tu na kurandaranda ovyo, jambo ambalo ndiyo humo humo huweza kupatikana baadhi ya wengine wakabakwa na wengine ikabidi wakakosa haki zao za msingi.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea nimshukuru Mhe. Waziri, kwamba niishukuru wizara yake kwa kuliona hili jambo lina umuhimu, kuwa ilisema Sera ya Elimu ya Lazima kuanzia tokea maandalizi. Mimi kwenye masuala haya ya tucheze tujifunze nimeshawahi kuwa mwalimu. Nilipata elimu hii ambayo baada tu ya wizara kuanzisha hii sekta, nilipata mafunzo haya pale Dodeani kule Kisiwani Pemba kwa fulani. Kwa hivyo, ninalifahamu vyema suala hili la elimu ya watoto.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, mimi mchango wangu niishukuru tena wizara kwa kuwasaidia walimu hawa, kwa sababu pale mimi ambapo niliiachia hii nafasi nikaendelea kubakia na majukumu mengine, posho lao walimu lilikuwa elfu ishirini. Kama sasa hivi imefikia elfu thalathini, *inshaallah* nina imani kama

wizara itawaongezea. Lakini ni vyema kuwasemea na kuona kwamba na wao wanajisikia raha kama walivyo walimu wengine. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba elimu ndiyo kila kitu, ndiyo msingi wa maisha wa mwanadamu na bila ya elimu haiwezekani mtu akawa binadamu kamili. Utakuwa upo tu utaishi kama mnyama. Hivyo, ni vyema Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri, walimu wetu wa vituo hivi vya Tucheze Tujifunze nao wakaonekana kwamba mishahara yao kwa kusema ukweli ni midogo, waongezewe. Ifikie alau kiwango fulani kwa sababu ndiyo serikali imesema itawaongezea wafanyakazi kwenye habari zao za mishahara kwamba kutoka kima cha chini na kupanda juu zaidi. Kwa hivyo, na wao hawa ijapo hayo hayo maposho wanayopewa yaongezwe baada ya hizi shilingi thalathini, wafikie angalau shilingi elfu sabini na wao ili waweze kuendeleza kutatua matatizo yao madogo madogo. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, mimi juzi nilifanya ziara ya kwenda Unguja Ukuu Kaskazini "B". Nilipofika kule kwa sababu hili jambo mimi ninalifahamu, nikapata baadhi ya walimu kule katika kufanya *research* yangu, niliwakuta walimu thalathini kule Kaskazini "B" ambao maposho yao hadi leo na hawa hawajapewa. Kwa hivyo, sijui kuna utaratibu gani mpaka sasa hivi ingawa mwenzangu Mheshimiwa, hapa aliyekaa kitako punde hivi, aliligusia suala hili la walimu wake kiupande wake kwenye jimbo lake kama hawajapata mishahara. Na mimi niseme kwamba hili suala jamani tuliangalie kwa kina hasa tukizingatia mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani baadhi yao walimu hawa wana familia, wanadaiwa; wale wanataka nguo za skuli, wale wanataka nguo kwa ajili ya Sikukuu na vile vile, kwa kupata mahitaji mengine, ni vyema kuwaona.

Mhe. Naibu Spika, mimi niliseme kwamba bila ya walimu wetu hawa nao kutunzwa, zile chekechea au ndoto zetu ambazo tumezianzisha zinaweza zika-*delay* na zisije juu. Na wanafunzi kwa kuwapeleka maskulini tu kama kawaida basi utoto wao mkubwa utakuwepo kwa watu kwamba, kule skuli walimu wapo, lakini kazi nyingi na wanafunzi wameshafikia idadi kubwa. Ni vyema kugawanya kama hivi ambavyo tuligawanya, lakini tu niseme kwamba navyo ni vyema kuboreshwa na vile vile, kuanzishwa japo vituo, kwa sababu pale zamani tulikuwa tunakaa chini ya miti au kwenye baraza zetu au twende sehemu za watu tu kawaida. Kwa hivyo, ni vyema na hapa, hawa nao wakaanzishiwa tu madarasa madogo madogo kwa ajili ya kuona watoto wetu nao wanapata elimu kwa hali ambayo inastahiki.

Mhe. Naibu Spika, mimi nikiendelea nije kwenye suala la walimu wetu wa skuli za kawaida sasa. Serikali kwa kupitia wizara ilisema itawaongezea walimu mishahara. Mishahara hii ambayo itawawezesha kuweza kukimu majukumu yao madogo madogo. Lakini kuna walimu ambao ni cheti walioambiwa kama wameshatimia umri wa miaka thalathini kwenye kazi zao. Hawa ndiyo wale ambao waliambiwa wataongezwa mshahara. Lakini je, hawa walimu ambao kuanzia miaka ishirini na tisa, hawa cheti kushuka chini, vipi wao mipango yao nao kuongezea hili suala la mishahara? Vipi itakuwaje? Kwa sababu na wao kama hawakuongezewa wataona, aah! Jamani wenzetu mishahara yao imeengezwa lakini sisi mishahara midogo. Kwa hivyo, ninahisi hapa kutakuwa na hali moja ambayo itawafanya wavunjike moyo.

Mhe. Naibu Spika, ili kuepusha hayo Mhe. Waziri na hili nalo uliangalie kwa kina kwamba, kuna walimu hawa wa cheti ambao wameshafanya kazi kwa muda miaka thalathini waliambiwa mishahara yao itaongezwa. Kwa hivyo, walio chini yao na vile vile ni vyema wakaangalia kwa kina. Pia, kwenye upande wa diploma nao kuna walimu ambao waliambiwa kuanzia miaka kumi na tano na kuendelea, nao pia wataongezewa mishahara yao. Vile vile, tuzingatie kwamba kuna na wenziwao ambao kuanzia hapa miaka kumi na tano kushuka chini, vile vile, nao wanahitaji kuongezewa mishahara yao, ili kuweza kuona kwamba na wao wanajikimu katika mahitaji yao.

Mhe. Naibu Spika, nimuombe Mhe. Waziri, ajitahidi kulisimamia jambo hili ili kuona na wao wajisikia faraja na wenziwao wakiwa wamo katika jamii kwa pamoja. Isije ikaleta fitna kwamba wengine wameongezewa na wengine hawajaongezewa.

Vile vile, Mhe. Naibu Spika, nimuombe Mhe. Waziri, atakapokuja hapa atwambie huku Kisiwani Pemba na Unguja, ni majengo mangapi ambayo yamefikia kutaka kuezekwa na bado hayajaezekwa. Vile vile, ni mpango gani wa mara hii mwaka huu wa fedha 2016/2017, ni majengo mangapi ambayo anahitaji kuyapatia huduma kwa ajili ya uwezekaji ili watoto wetu wapate sehemu nzuri za kukaa. Vile vile, akija hapa atwambie katika mwaka wa fedha 2016/2017, ni majengo mangapi ambayo yataezekwa.

Mhe. Naibu Spika, mimi leo sina mengi nilitaka kuchangia hii sehemu ili kuona kwamba hawa walimu wetu wanapata mishahara yao na maposho yao kadri siku zinavyoendelea. Kwa sababu tunavyojua suala la elimu ni suala ambalo ni kubwa, bila ya elimu na bila ya walimu kuwezeshwa licha ya changamoto ambazo Wizara hii inazikumbana nazo.

Lakini mimi niiombe serikali na nimuombe Mhe. Waziri, ashirikiane na watendaji kuona haya majukumu yanaondoka kadri siku zinavyokwenda. Ninaamini Mwenyezi Mungu kwa hekma alizowapa *inshaallah* haya majukumu yataondoka na ili hawa watu nao wajisikie faraja katika nchi yao na kazi zao ili waweze kuzifurahia. Kwa sababu bila na wao kuwezeshwa basi zile nafsi zitaanza kukaa vyengine. Wataona loo! Hii hali imekuwa ngumu, ndiyo pale pale tutapiga kelele watoto hawasomi, watoto wanadhurura ovyo.

Mhe. Naibu Spika, lakini vile vile nimuombe Mhe. Waziri, aangalie kule Kisiwani Pemba watu wanaipigia maneno kwenye wizara yake kwamba, sasa hivi kule Kisiwani Pemba hali ya siasa imekuwa kubwa sana, hususan na wafanyakazi ndani ya wizara yake kwamba, asubuhi wafanyakazi wanaifanya kama mwiku au niseme uporo, mchana wanaifanya vishuka na usiku vile vile wanaifanya kama daku. Jambo ambalo hili uwajibikaji siyo mzuri, kwa sababu watu kama mwenzangu alivyomaliza Mheshimiwa, hapa alisema kwamba kuna watu wanazitumia ofisi vile wanavyotaka wao, hawaendi pale kufanya zile kazi ambayo wanatakiwa wafanye.

Unakuta ndani ya madarasa muna watoto wapigana, lakini walimu wamo ndani ya ofisi zao wanakaa wanazungumzia siasa tu; sijui leo itakuwa hivi, kesho itakuwa hivi, jumatano itakuwa hivi. Kwa hivyo, hii hali aione hususan kule Pemba. Mimi ninamuomba hasa afanye ziara na watendaji wake aende hasa na wizara yake kule Pemba, ayatembelee yale maskuli hususan Kaskazini kule kisiwani Pemba ndiyo hii siasa imehamia, aende akaone zile hali ambazo zimekuwepo.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, nikiendelea nimuomba Mhe. Waziri, kuna skuli yetu pale katika jimbo letu la Tumbe ile iliyojengwa na hawa Wachina. Ile Skuli ni nzuri, kubwa inafaa vya kila aina, lakini niliambiwa ile skuli itapata uzio. Lakini mpaka leo ile hali ya uzio naona imekuwa ni tete. Kwa hivyo, hili aende akaliangalie kwamba ile skuli iliambiwa itatiwa uzio ili kwa kuona kwamba wananchi waliokuwepo pale hawaendi kulifanyia uharibifu lile eneo kwa ajili pengine kulima ovyo ovyo, ama kuzichukua zile nafasi kwa kufanya miradi mengine au kwa wale wafugaji ambao wanawakera wale walimu kutokana na ile skuli ambayo wanakwenda wakifunga ng'ombe karibu karibu. Kwa hivyo, na hili pia nimuombe aliangalie kwa kina ili kuona kwamba ile skuli ule uhalisia wake ulionao usipotee na vile ambavyo ulikadiriwa kufanikisha basi lifanikishwe.

Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, mimi niwatakie dua watendaji hawa, Mwenyezi Mungu awajaalie gurudumu hili walifikishe salama na sote tuliomo

humu atujaalie tumsaidie Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuona kwamba majukumu yake aliyonayo na sisi tuna mchango mkubwa. Hivyo, ninaiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana ninakushukuru Mhe. Ali Khamis Bakar. Sasa mchangiaji anayefuata ni Mhe. Rashid Makame Shamsi na baadae atafuata Mhe. Zaina Abdalla Salum na hapo atafuata Mhe. Said Omar Said na baadae atafuata Jaku Hashim Ayoub.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuichangia Wizara yangu tukufu ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Awali nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini vile vile nimpongeze Mhe. Waziri, Naibu Waziri na watendaji wake kwa hotuba nzuri iliyopangika ya kitaalamu ambayo imewasilishwa wiki iliyopita. Lakini vile vile nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati ya Elimu na Afya Mhe. Mwinyihaji Mwadini Makame, kwa uwasilishaji wake. Taarifa yao kwa kweli imetoa muongozo mkubwa na mapendekezo mengi kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Na nimuombe sana Mhe. Waziri, aitazame sana ripoti ile ina mambo mengi ambayo yameweza ku-*cover* vitu muhimu sana vya kuiendeleza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Lakini vile vile niwapongeze Waheshimiwa, wenzangu walioendelea kuchangia hotuba hii kwa michango yao. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nitakuwa mkosefu wa fadhila sana bila ya kuichangia wizara yangu hii ambayo ndiyo imenilea kwa miaka thalathini na sita. Na niseme tu kwamba kabla sijaenda mbali, mimi ninaiunga mkono hii asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, wizara hii ndiyo wizara mama za wizara nyengine. Ni wizara muhimu ndiyo ambayo inaandaa wataalamu wa fani mbali mbali, ni wizara ambayo inapaswa kuwekezwa zaidi kuliko wizara nyengine kwa sababu tegemeo la wizara nyengine ni Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Nimuombe sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, kuweza kuhakikisha kwamba bajeti hii, wizara yetu hii inapata asilimia kubwa sana ya vifungu vya matumizi. (*Makofi*)

Wizara ya Elimu ina changamoto nyingi sana Mhe. Naibu Spika, hususan ukiangalia hivi sasa kwamba kutokana na tamko la Mhe. Rais wetu la elimu kuwa bure kwa ngazi ya maandalizi mpaka msingi, basi changamoto zimekuwa ni nyingi mno, kiasi ya kwamba watendaji wangu ndani ya wizara hii vichwa

vinawauma. Ningependa sana nimuombe sana ndugu yangu Dkt. Khalid kuweza kuitazama kwa jicho la huruma la huruma sana wizara hii, kuona kwamba vifungu vyake vya bajeti mwaka huu basi vinafika asilimia kubwa kuliko ilivyokuwa mwaka jana. Mwaka jana tulikuwa tunaambiwa uchaguzi, uchaguzi sasa umekwisha, sasa ni kazi tu. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, katika michango yangu baada ya utangulizi huo mimi niende katika suala zima la Chuo chetu la Taifa (SUZA). Mhe. Naibu Spika, tulianza kuvichukua au kukichukua Chuo cha Ualimu Nkrumah kuwa chini ya SUZA. Na hivi sasa kuna nyimbo nyingi za kuweza kuvichukua Vyuo vyengine kuwa chini ya SUZA. Kuna Chuo cha Afya kinatajwa na hilo, kuna Chuo cha Kilimo kinatajwa na hilo, kuna Chuo cha Utalii inatajwa na hilo. Juzi juzi ninasikia na Chuo cha Kiislamu kinatajwa na hilo na Uongozi wa Fedha.

Mhe. Naibu Spika, lazima tupembue. Haiwezekani kwamba vyuo vyote hivi vya nchi hii kuwa chini ya SUZA. Ni dhahiri kwamba tutaibebesha mzigo mzito na ule ufanisi ambao tulikuwa tunautarajia usipatikane. Mimi imani yangu ni kwamba vyuo hivi ni kuvipa uwezo vyenyewe na nina imani kwamba elimu itakayotolewa itakuwa inakidhi haja kwa Wazanzibari.

Hivi sasa maadili ya ualimu yamepungua baada ya kukiondosha Chuo cha Ualimu Nkrumah. Hivi sasa kozi za ualimu zinazotolewa kwa kweli *ethics* hasa za kiualimu zimepungua sana. Ni dhahiri kwa kweli tukivichukua hivi mbali mbali tukiviingiza SUZA, basi hata hizo fani nyengine zitaanza kutetereka. Hivi sasa unaweza ukamuona kijana anayechukua *diploma* pale Beit el Ras, basi suruali yake kaiteremsha, halafu unaambiwa huyu anachukua *diploma* ya ualimu, anakwenda kufundisha nini, maadili gani. (*Makofi*)

Tuviwezeshe vyuo vyetu hivi navyo vifanye kazi na vinaweza vikatoa elimu za juu, si lazima vyuo vyote viingie katika SUZA, Mhe. Naibu Spika. Lakini hata hivi Vitivyo ambavyo ni vipya ambavyo tutavianzisha, lazima tuvianzishe Vitivyo hvi kulingana na masharti ya *TCU*. Hatuwezi tu tukakurupuka tukaanzisha Vitivyo. Lazima tuwe na *staff members* wa kutosha ambao wataweza kuviendesha Vitivyo hivyo. Lakini *facilities* za kutosha ndani ya eneo husika.

Mhe. Naibu Spika, leo tuna kozi za afya lakini wanafunzi wanalazimika mpaka waje Mbweni wawe wanafanya mazoezi afya. Tunaenda wapi? Kozi hiyo ukitazama *staff member* wa Zanzibar ninafikiri ni mmoja. Tunategemea Wacuba. *TCU* hawawezi kukubali hilo. Lakini na vyuo vyengine tukianzisha tutakuja kukuta hivyo hivyo. Tumeanzisha kozi ya michezo ya *diploma*,

viwanja wafuate viwanja vya Mnazi Mmoja watoke Tunguu. Wapi na wapi hayo jamani! Lazima tunapoanzisha hivi Vitivyo vile vile tuweze kufikiria jinsi gani tutaweza kuwarahisishia mafunzo wanafunzi wetu.

Mhe. Naibu Spika, nije sasa katika hii taasisi ambayo niliifanyia kazi ya Baraza la Mitihani. Hii ni programu ya upimaji na tathmini. Kwanza niwapongeze sana kwa kuendesha shughuli zao kwa ufanisi. Wamesimamia mitihani mingi kulikoni uzoefu ulivyokua unaonesha baada ya kuingia mfumo huu wa sera hii ya 2006, wamepima mitihani ya darasa la sita, kwa hivyo, kazi zimeongezeka.

Lakini Mhe. Naibu Spika, bajeti wanaotengewa hawa watu ni ndogo, kazi hizi za Baraza la Mitihani ni nyingi, ningeomba sana. Lakini vile vile hata asilimia iliyoingizwa mwaka jana ni ndogo, kiasi ya kwamba Baraza hili lina madeni yanayohusiana na vyakula, lina madeni yanayohusiana na posho za walimu. Kwa kweli hatuitendei haki, bajeti hii mwaka huu nimuombe sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, kuweza kuipandisha.

Suala jengine ni kwamba tunatoa majina ya hadhi kubwa sana, hili ni Baraza hivi sasa, lakini mfumo unaoenda nao sio wa Kibaraza, mfumo huu ni wa kiidara. Kwa hivyo, niiombe sana Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika hili kulitazama. Hii taasisi ina changamoto nyingi, taasisi hii haina jengo, niiombe sana Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ifikirie kuweza kuona kwamba Baraza hii la Mitihani lina jengo ambalo linajitegemea. Jengo ambalo lipo halikidhi haja kwa kweli na linalipiwa kodi ya pesa nyingi sana.

Mimi nafikiria kwamba kama utakua na mpango wa kujenga jengo kubwa sana, basi ingewezesha pengine Baraza la Mitihani, taasisi ya elimu zikaingia humo, kwa sababu hata taasisi yangu ya elimu ina chumba kimoja tu cha watendaji katika wizara, ambayo haiwezekani taasisi ye elimu ndio muhimili wa elimu bora katika nchi yoyote ile. Kwa hivyo, niiombe sana wizara kuweza kuhakikisha kwamba inapata majengo kwa ajili ya hizi idara ambazo ni za muhimu sana katika wizara yetu.

Mhe. Naibu Spika, nije katika suala zima la elimu bora au ubora wa elimu. Mhe. Naibu Spika, taasisi ya elimu ndio muhimili mkubwa wa kuweza kupandisha suala zima la ubora wa elimu Zanzibar, ina majukumu mengi. Kwanza niipongeze sana chini ya Mkurugenzi wake, inafanyakazi nyingi lakini kwa kweli hali ya taasisi hii inasikitisha, taasisi haiwezi kuwa na chumba kimoja tu cha watendaji au vyumba vyake vya kukodi, kodi, tumpatie jengo ndugu Mkurugenzi ili aweze kuendesha kazi zake vizuri. Hawa watendaji

angalau na wao wapelekwe wakajifunze, twendeni hapo Dar-es-Salaam tukaione taasisi ya elimu, taasisi ya elimu ni chombo kikubwa sana.

Vile vile, ndani ya taasisi ya elimu hii ndio inayotakiwa iweze kutunza zana na vifaa vya ufundishaji, lakini leo vitabu vyote vya kufundishia na zana nyengine zinamilikiwa na idara nyengine, ina maana utamkuta Mkurugenzi hana mamlaka ya kuweza ku-*control* vifaa na zana za ufundishaji, hii ni hatari, kwa sababu vikiibiwa maana yake nani wa kujibu. Hivi sasa Mhe. Naibu Spika, utakuta vitabu vya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali vinaonekana katika maduka mengine, sasa hivi ni Zanzibar na hata Tanzania Bara na kuna kesi ambayo wengine wanakamatwa. Akija Mhe. Waziri, ningemuomba sana atueleze kesi ile ya wizi au uuzaji wa vitabu katika maduka binafsi imekwendaje, kwa sababu bila ya hivyo, ina maana hizi mali zetu ambazo tunasema haziuzwi, ina maana kila siku zitaendela kutoka na serikali ina gharamika.

Mhe. Naibu Spika, sasa nije katika fani yangu kwenye hii programu ya michezo na utamaduni katika skuli zetu. Mhe. Naibu Spika, kutokana na suala hili la elimu bila malipo au elimu bure, imekua sasa suala la michezo linaweza kuwa na ugumu. Hii bajeti kwanza iliyotengwa kwa kitengo hiki ya shilingi milioni 250.3 hii ni ndogo, ukiangalia na changamoto za ufundishaji wa somo la elimu kwa michezo. Skuli nyingi hazina vifaa vya michezo, vile vifaa vya wanafunzi ambao hawana ulemavu na wale wanafunzi wenye ulemavu, hivi vitu havipo, tutafundisha vipi, mitaala tunayo lakini haitekelezeki na pia hatuna walimu wa kutosha wa kuweza kulifundisha hili somo.

Mhe. Naibu Spika, nitowe pendekezo kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Tunacho Chuo cha Ualimu cha Kiislamu, hapa sisi tulijipinda tumeandaa mtaala wa michezo, lakini haufundishwi na viwanja vipo, sasa tunatarajia tutapata walimu wa michezo katika skuli za msingi watoke wapi, hatuwezi kuwapata. Kwa hivyo, tuweke mkazo sana hapa katika suala zima la ufundishaji wa elimu kwa michezo katika vyuo vyetu vya ualimu ambavyo vitapelekea kuweza kuwapata walimu ambao watafundisha katika ngazi za primari na ngazi za sekondari.

Vile vile, hayo mashindano yetu ya elimu bila malipo yalikua yanakwenda kutokana na michango ya wanafunzi na michango ya walimu. Lakini leo skuli utazikuta hazina fedha kwa sababu michango haipo, hivyo, ruzuku inahitajika. Kwa hivyo, niiombe sana Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuweza kupitisha ruzuku kwa hizi skuli, kwa sababu bila ruzuku basi ufundishaji

hauwezi kwenda wa masomo yakawaida, lakini pia ufundishaji hata kwa masomo haya ya michezo itakuwa ni mgumu.

Mhe. Naibu Spika, hivi karibuni nilikutana na mwalimu wa michezo mmoja, akaniambia kaambiwa na mwalimu mkuu kwamba kila mnapoendelea kushinda nyinyi basi mnaiumiza skuli, kwa sababu hatuna pesa, sisi tunataka mshindwa hasa kwenye hayo mashindano, maana tumeshachoka. Sisi tunataka tukuze vipaji, lakini unakuta vipaji hivyo haviwezi kukuzika bila ya kuwa na pesa.

Mhe. Naibu Spika, vifaa vya michezo ni ghali sana, hivyo, ningeiomba sana Wizaa ya Elimu kuwa na mikakati kwa kushirikiana na wizara inayohusika na michezo kuweza kuona hili linapendekezwa. Nija katika vipaumbele vya wizara, hapa kuna skuli mpya ambazo zitajengwa. Tuishukuru sana Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kuweza kushirikiana na wafadhili wetu kwa kujenga majengo mengi na mazuri ambayo yanasaidia sana kuleta maendeleo ya elimu katika ngazi ya msingi na sekondari. Katika bajeti hii kuna skuli 10 za sekondari zitajengwa na skuli moja mpya ya msingi itajengwa.

Mhe. Naibu Spika, niiombe sana Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika hili, kwanza kufikiria jinsi gani skuli hizi zitaanzishwa. Skuli ambazo zimejengwa mpya hivi sasa nyingi zina nyufa. Sasa hii hata sijui ni vipi. Nafikiri kuna vitu viwili; kuna suala zima la kiwango, lakini vile vie kuna suala zima la upembuzi labda katika ardhi ambazo zinajengwa skuli hizi. Niiombe sana Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kushirikiana na wakandarasi, katika mipango ya ujenzi wa skuli hizi kuanza upembuzi wa ardhi ambazo zitajengwa katika skuli hizi.

Kwa mfano, ukienda Muyuni pale Mhe. Jaku Hashim Ayoub, amejenga nyumba nzuri, lakini inamshinda kukaa imejaa nyufa, hakuinyima saruji, lakini kutokana na mazingira ya ardhi ya Muyuni, basi inataka utaalamu wa kina wa kupembua udogo, sasa inawezekana hizi skuli mpya katika ujenzi wake hakuna upembuzi wa ardhi, lakini vile vile inawezekana kuna hitilafu katika ujengaji, kwa sabahu inawezekana kiwango hakikufikiwa. Kwa hivyo, niombe sana ili serikali isiingie hasara basi majengo haya mapya yatakayojengwa kuwa na umakini mkubwa na wakandarasi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nije katika jengo la skuli ya Sekondari ya Kibuteni. Mhe. Naibu Spika, hii skuli ya Kibuteni iko miaka mingi haijamaliza hata asilimia 45 haitatimia. Napenda sana atakapokuja Mhe. Waziri, aweze kutueleza nini ambacho kimechangia kuzorota kwa ujenzi wa skuli ile. Kama kuna sakata kati ya Mkandarasi, Wizara na Mfadhili basi atueleze wazi, kwa sababu jengi lile ni

la miaka mingi na nina imani kila likiendelea kuwepo vile ina maana linaitia serikali hasara. Pia, atuambie ni lini ujenzi wa skuli ile utaendelea, kwa sababu sisi tuna hamu nayo.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie katika suala zima la ukarabati wa majengo. Tuna majengo mengi na ninajua kwamba wizara yangu uwezo wake wa fedha za kimaendeleo ni mdogo, lakini kuweza kutazama ukarabati wa majengo yetu yakiwemo mabanda ya skuli, hata na nyumba za walimu. Juzi nilikwenda Jambiani nilisikitishwa sana Mhe. Naibu Spika, kuna nyumba tano pale, lakini nyumba nne walimu wanakaa kwa tabu kweli kweli nyumba zote zinavuja. Suala hili litazamwe upya na zitazamwe nyumba mbali mbali ili ziweze kufanyiwa ukarabati, kwa sababu tusipofanya ukarabati maana yake nyumba hizi zitaanguka, halafu tutawaomba wafadhili kujenga nyumba nyengine.

Mhe. Naibu Spika, mwisho ni kwamba ndani ya jimbo langu katika Skuli ya Maandalizi ya Magomeni, skuli hii paa lake ni la siku nyingi, imejengwa toka miaka ya 1970, hivi sasa paa lile linavuja. Mimi ni mjumbe wa kamati na viongozi wangu wa skuli ile tayari wameshapeleka barua Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ili kuweza kupitiwa lile jengo kuangaliwa. Juzi katika mvua hizi dari lilianguka likawagonga wanafunzi na mwalimu. Nimshukuru sana Mhe. Mwakilishi, aliyepita Mhe. Salmini Awadh Salmin, Mwenyezi Mungu amlaze pahala pema, alitia pesa za maendeleo pale mwaka 2013 ukafanywa ukarabati, lakini paa lile limeshachoka. Kwa hivyo, naiomba sana Wizara ya Elimu na Mafunzoya Amali ikalitazame paa lile ili tushirikiane katika kuona kwamba paa lile linajengwa, kwa sababu hivi sasa wanafunzi wengi sana katika kila daraka unakuta wamo wanafunzi 80, badala ya ile 45 kutokana na elimu bure.

Kwa hivyo, niiombe sana Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na nimuombe sana Waziri, tukamatane mikono twende ili nione kwamba skuli yangu ile ambayo inasaidia sana watu wa jimbo langu, lakini hata jimbo jirani la Mpendae basi inafanyiwa ukarabati mkubwa ili watoto wetu wasome kwa salama na amani.

Baada ya kuchangia hayo Mhe. Naibu Spika, niushukuru tena uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kwa kuweza kuwasilisha hotuba hii na niombe sana wizara kuwa karibu sana na mimi vile vile kuweza kuisaidia, kwa sababu mimi ni mdau wa elimu na nimelelewa ndani ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Naendelea kusema kwamba naichangia hotuba hii ya Mhe. Waziri ndugu yangu, Mhe. Riziki Pemba Juma, kwa asilimia mia kwa mia, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana nakushukuru Mhe. Mjumbe. Mchangiaji anayefuata ni Mhe. Zaina Abdalla Salum, baadae nimesema atachangia Mhe. Said Omar Said na atafuta Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Mhe. Zaina Abdalla karibu.

Mhe. Zaina Abdalla Salum: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, aliyetujaalia uhai na uzima na kuweza kufika hapa tukiwa sote ni wazima na afya njema. Pili, napenda kukupongeza Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia fursa hii ambayo ni adhimu kwa siku hii ya leo na mimi niweze kuchangia machache katika hii Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Naibu Spika, huwenda ikawa mengine keshanifilisi mwenzangu Mhe. Mwantatu Mbaraka, lakini mimi ni kiongozi siwezi kukosa ya kuchangia kwa sababu na mimi ni mtetezi, kwa hivyo, ni lazima niyapate ya kuweza kuchangia, nitachangia machache kwa sababu mengine yameshachangiwa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa vile tu wajumbe wenzangu wameshatangulia kuchangia mengi, mimi nitazungumzia kuhusiana na Elimu ya Maandalizi hasa kwa watoto wenye ulemavu bado elimu hii haijazingatiwa vizuri, kwani watoto wenye ulemavu bado sijawaona katika elimu ya maandalizi. Kwa hivyo, Mhe. Waziri, akija hapa atatuambia kuwa watoto hawa wenye ulemavu kuhusiana na Elimu ya Maandalizi sijui kawapangia vipi. *(Makofi)*

Pili, Mhe. Naibu Spika, naipongeza sana serikali kwa kutupatia Elimu ya Mjumuisho. Lakini Mhe. Naibu Spika, elimu hii bado haijazingatiwa vizuri hasa katika utoaji huu wa elimu, kuna baadhi ya walimu bado wananyanyapaa katika kuitowe elimu hii vizuri kwetu sisi wenye ulemavu. *(Makofi)*

Sasa namuomba Mhe. Waziri, aifanyie kazi elimu hii ili iweze kutolewa vizuri katika watoto wale wenye ulemavu.

Jengine ni changamoto ambazo zinazoikabili hii Elimu Mjumuisho ni ukosefu wa vifaa, ama vitendea kazi hasa kwa walimu na wanafunzi wenyewe, kwa sababu utakuta kila mmoja na ulemavu wake. Kuna wanafunzi walemavu wasioona wale ambao wanatakiwa wapate maandishi ya nundu. Kwa hivyo, Mhe. Waziri, tunamuomba sana azingatie hili kwa kuwapatia vifaa na vitabu vyenye maandishi ya herufi kubwa, ili kwa wale wenye uono wao mdogo basi waweze kuona vizuri wapate kusoma, na wale wanaotakiwa kupata maandishi

ya nukta nundu wazipate vizuri ili waweze kusoma masomo yao na kufanya mitihani yao vizuri kwa kuielewa hii elimu yao. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, jengine napenda kusema kwamba kuna baadhi ya wazazi wanakuwa wanawaficha watoto wao wenye ulemavu ili wasipate elimu hii, na hii inakuwa ni kosa la jinai kwa kumkosesha mtoto elimu yake ya msingi. Kwa hivyo, naiomba serikali kwa kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, ichukuwe hatua kali kwa yeyote yule iwe mwalimu au wazazi anayemkosesha mtoto huyu kupata elimu hii ya msingi au ya chuo kiuu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa haya machache napenda kusema kwamba naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Samahani Mhe. Naibu Spika, nataka nimuombe Mhe. Waziri kwamba, Baraza lake la Mitihani liangalie vizuri kuhusiana na watoto wenye ulemavu wa akili, kwa sababu watoto hawa wao wanasomeshwa ili kupata tu yale mazoezi ili wajuwe kujijengea uwezo wa kuweza kujua nini wanachofanya. Sasa mitihani inafanywa sawa sawa na wale wenye ulemavu wa uzima au wenye akili timamu. Kwa hivyo, hawa wapunguziwe ile mitihani yao wafanye ili na wao wapate kujua kiwango gani ambacho walichokuanacho cha fahamu.

Mwisho, naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja, ahsante sana Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Zaina Abdalla. Tumpishe basi Mhe. Said Omar Said na baada ya hapo atakuja Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Ajitayarishe Mhe. Ali Suleiman Ali Shihata, na baadae atakuja Dkt. Makame Ali Ussi.

Mhe. Said Omar Said: Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu *Jallah Subhanahu Wataallah,* aliyenijaalia uzima na afya na kuniwezesha kuwepo katika kikao hiki asubuhi ya leo.

Pia, nichukuwe fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, kwa jinsi alivyoiwasilisha hii mada kwa umahiri mkubwa sana. Alipokuwa anaiwasilisha mada ilikuwa ukipepesa jicho tu basi humkuti, yaani hujui yuko wapi. Tumshukuru sana kabisa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa wengi wameshayazungumza mengi basi mimi niende moja kwa moja kwenye suala la huduma ya ukaguzi. Kwanza niipongeze Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kuweka programu hii ya ukaguzi wa elimu, kwa sababu wazee walisema kwamba; 'uundwao si kama kusabiliwa'. Wakaguzi ndio watu pekee wanaotoa misukumo kwa wafanyakazi

kuweza kufanyakazi kwa ufanisi, bila ya kuwepo kwa wakaguzi basi kazi haziwezi zikafanywa kama ilivyopangiwa. Lakini kwa kuwepo kwa wakaguzi kazi zinakwenda kwa murwa kutokana na umahiri na taaluma za wakaguzi walizonazo.

Mhe. Naibu Spika, wako wafanyakazi ambao hawahitaji ukaguzi, yaani wako walimu ambao hawahitaji kukaguliwa. Hawa ni wale ambao wanaona kuwa huku kufundisha, sisi hawa tunaowafundisha tunawafundisha ndugu zetu na kaka zetu basi wale hawahitaji kukaguliwa. Lakini wako ambao wanahitaji kukaguliwa ni wale ambao wanaona kuwa sisi tunafundisha watoto wa serikali, wa wizara na wa idara, basi lazima kiwepo kitengo hiki cha ukaguzi ili kiweze kuwaweka sawa, baina ya hawa waliokuwa hawahitaji kukaguliwa na hawa wanaohitaji kukaguliwa, wote wakaguliwe ili wende sambamba kulingana na malengo ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Naibu Spika, moja katika kazi za wakaguzi ni kuhakikisha kwamba walimu wanafundisha kulingana na miongozo waliopewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, lazima mkaguzi ahakikishe kwamba mwalimu anafundisha kutokana na miongozo ya Wizara ya Elimu, kwa mfano mwalimu kabla ya kuingia darasani lazima awe na mabuku mnne ya kazi, ahakikishe mwalimu anayo *Scheme of work, Preparation book, Daily Record* na *Assessment book,* hapo mwalimu ndio aingie darasani, akiingia darasani katika hali hiyo ataifanya kazi yake kwa kujiamini na wanafunzi wake watamuamini, watakuwa karibu nae na watamfahamu mno mwalimu yule kwa kuwa na haya, kwa sababu ameyapanga na wanafunzi ili wafahamu lazima waende hatua kwa hatua, kila mtu ana akili yake na uwezo wake wa fahamu ndio ikabidi walimu waende kwa taratibu hizo ili wanafunzi waweze kumpata yule mwalimu kwa wale wenye kufahamu haraka na wale ambao wanafahamu kwa uzito, wote wende sambamba kutokana na mwalimu kufuata hatua alizopewa na Wizara ya Elimu.

Endapo mwalimu anaingia darasani lakini hana mabuku hayo na kwa bahati akatokea mkaguzi pale basi hapo mwalimu huyo atakwanga tu siku hiyo, kwa mfano anaweza kufundisha kuhusu maziwa makuu ya Afrika ya Mashariki, lakini kwa kuwa hana maandalizi na hayuko *okay*, na mkaguzi yupo anaweza kujishtukia yuko Iran anachimba mafuta huko, wale wanafunzi wakamshangaa yule ameanza je na amemalizikia vipi. Kwa hivyo, ni wajibu na ni kazi za Wakaguzi kuhakikisha kwamba kila mwalimu anayekubalika kufundisha katika shule za Serikali lazima awe anayo mabuku manne yale ya kazi kabla ya kuingia darasani, anapokuwa na mabuku hayo ndio yatakayomuwezesha yeye kuitwa mwalimu na hapo atakuwa hana dosari yoyote katika ufundishaji huo.

Lakini si kazi hiyo tu pia wakaguzi wana kazi au wana majukumu ya kuhakikisha kwamba, je, hawa wanafunzi wanaifanya kazi wanayopewa na mwalimu, wakaguzi pia ni kazi yao hiyo, kuhakikisha kwamba hao wanafunzi wanaifanya kazi wanayopewa na mwalimu, lakini sio hilo tu, pia kazi wahakikishe kwamba huyu mwalimu hii kazi aliyoitoa, je, anaiangalia. Mkaguzi hatokuwa mkaguzi bora yule ambae ana-*deal* na mabuku manne tu yale ya kazi, kwa sababu kuna wakaguzi wengine akifika mwalimu baada ya kuchukua mabuku yake ya kazi yote ni sawa, yako *okay*, basi huyo anakwenda zake hata hawezi hata kumuangalia angalau dakika mbili au tatu jinsi anavyofundisha. Au hawezi akaingia hata mule darasani, sasa hapo bado hujam-*assess* yule mwalimu, wala hujawa-*assess* wale wanafunzi, wewe ni mkaguzi wa walimu na wanafunzi kwa faida ya wanafunzi.

Kwa hivyo, lazima yule Mkaguzi baada ya kuhakikisha mabuku manne anayo mwalimu, aingie darasani na aangalie japo dakika mbili, tatu, pia, anaweza kukusanya baadhi ya mabuku ya wale wanafunzi akakae sehemu aangalie, je, haya mabuku yanasahihishwa. Mhe. Naibu Spika, kuna baadhi ya walimu wanafanya kazi sawa kwa nguvu na wanawapa kazi wanafunzi, lakini hawajui wanafunzi wale kazi waliyopewa wameipatia au wameikosea, sasa hapo itakuwa mwanafunzi yule unampumbaza wewe mwalimu hajui kazi uliyompa ameipata, kama hakuipata usahihi ni upi, itakuwa yeye anakwenda tu, hili pia ni jukumu kubwa la wakaguzi.

Nije katika Programu ya Elimu Mbadala, mimi niipongeze sana Wizara ya Elimu kuendeleza Elimu Mbadala na watu wazima, kuna watu wanasema; "mtu mzima hasomi", lakini mtu mzima anasoma na mtu mzima ndiye anayesoma, kwani upo mfano halisi. Mtume Mohammad (*SAW*) alianza kusomeshwa ana miaka 40, sasa yeye anaelewa Mwenyezi Mungu kwamba, huyu mkubwa ndiye anaweza kuipokea taaluma kuliko huyo mdogo, sasa akaanza kusomeshwa kwa muda wa miaka 40 na yeye ndio mwalimu wa dunia nzima.

Baada ya Wizara ya Elimu kuelewa haya ikaanza kufungua madarasa ya kisomo mjini na vijijini kwa Unguja na Pemba. Hivi sasa Mhe. Naibu Spika, nataka nikuhakikishie kwamba hii taarifa inayosema hapa kwamba ifikapo 2020 kiwango cha kujua kusoma na kuandika kitapanda kutoka asilimia 84% mpaka 90% ni kweli. Kwa sababu sasa hivi wana kisomo kwa hatua ya nne ambao kwa skuli tuite kama daraja la darasa la nne, kwa sababu kule wanasoma kwa hatua, hatua ya kwanza, hatua ya pili, hatua ya tatu, hatua ya nne. Sasa wanakisomo wa hatua ya nne, huku shule tunafanya kama mwanafunzi wa darasa la nne.

Mhe. Naibu Spika, nataka nikuhakikishie kwamba, mwanakisomo wa hatua ya nne anaweza akasoma risala mbele ya hadhara ya watu elfu kumi, anaweza kusoma utenzi mbele ya hadhara ya watu elfu kumi, tofauti na mwanafunzi aliye darasa la nne, hii ni kuthibitisha kwamba yaani mtu mzima anapokea taaluma kuliko mtoto mdogo, tushaanza kuwaona katika sherehe mbali mbali, sherehe zao, yaani kila mwaka wana sherehe zao.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa, umebakiza dakika nne.

Mhe. Said Omar Said: Ahsante Mheshimiwa, kwa hivyo, hapa ina maana inathibitisha kwamba wanakisoma wa hatua ya nne ni bora kuliko wale wanafunzi wa darasa la nne.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na kazi wanayoipata walimu, hao walimu wa hiki kisomo ni kubwa mno, ni tofauti na walimu wa skuli, kwa sababu walimu wa kisomo wanawafuatia wale wanafunzi wao mpaka majumbani mwao kwa ule uzalendo wao, kwanza tuwapongeze sana walimu wa kisomo Unguja na Pemba kwa uzalendo, wanakwenda mpaka ndani kwenye majiko; "vipi wee bibi wewe, hujui kuwa leo ni siku ya darasa? Ah! Nenda, kwanza mimi nakuna nazi" Mwalimu yule wa kisoma anakaa juu ya mbuzi anakuna nazi, baadae ndio anamchukua yule kwenda kule darasani.

Kwa hivyo, kwa juhudi kubwa wanayoifanya tunaomba Wizara iwajongeze jongeze kidogo hii posho ya walimu, kwa sababu kwa kazi yote wanayoifanya wanapewa posho la shilingi thalathini elfu, kwa kweli kwa kazi yao ni ngumu na ni kidogo sana, kwa hivyo, tunaomba sana Wizara kidogo ipeleke jicho la huruma pale kwa walimu wa kisomo.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie katika programu ya utawala na uongozi niwapongeze maafisa wa Elimu na Mafunzo ya Amali wa Wilaya na walimu wakuu jinsi wanavyofanya kazi.

Mhe. Naibu Spika: Umebakiza dakika mbili Mheshimiwa.

Mhe. Said Omar Said: Ahsante sana Mheshimiwa. Niwapongeze sana walimu wakuu pamoja na maafisa wa Elimu na Mafunzo ya Amali ya Wilaya jinsi wanavyojitolea, pamoja na kwamba Wizara ina changamoto na changamoto zote hizi zinawafika wao, naomba nizieleze baadhi ya changamoto za Wizara ya Elimu. Kwa mfano uhaba wa walimu, walimu wakiwa haba wanasakamwa walimu wa kuu, pamoja na maafisa, madeni makubwa ya matumizi ya maji

katika mashule, yote wanasakamwa hawa wawili hawa, malimbikizo ya fedha nyingi za walimu za likizo na mishahara, wanasakamwa hawa, kukatwa walimu mishahara yao kimakosa na bado hawajalipwa mpala dakika hii, yote wanasakamwa hawa. Mhe. Naibu Spika, ningemuomba sana Mhe. Waziri, hili suala hili na changamoto hizi awapunguzie walimu wakuu pamoja na maafisa wa Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mwisho kabisa ukija katika programu ya mafunzo ya Amali, programu hii ina lengo la kutoa elimu kwa vijana ili wajiajiri wenyewe ni kweli, lakini ningemuomba hapa Mhe. Waziri, alieleze…

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa muda wako umekwisha.

Mhe. Said Omar Said: Anieleze ni wanafunzi wangapi Pemba wamemaliza Chuo cha Amali na ambao wamewezesha ili kuweza kujiajiri.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo, niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja nakushukuru sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa fursa hii ya kuchangia Wizara ambayo ni muhimu Wizara ya Elimu, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu na nimshukuru sana Mhe. Waziri, kwa hotuba yake nzuri yenye vipaumbele, itakuwa sijamfanyia haki vile vile Naibu Waziri na yeye kama sikumshukuru, Katibu Mkuu na zaidi Naibu Katibu Mkuu kwa umakini wake wa hali ya juu, niliwahi kufanya nae kazi Naibu Katibu Mkuu ni msikivu.

Mhe. Naibu Spika, nije katika ukurasa wa 21, kuhusu Programu tano za ukuaji wa Elimu. Mhe. Naibu Spika, programu hii naiunga mkono moja kwa moja lengo lake ni kutoa elimu kwa ngazi zote; huduma za mitaala, vifaa vya kufundishia, huduma ya upimaji na tathmini ya Elimu na huduma ya ukaguzi wa Elimu.

Mhe. Naibu Spika, naweza kuthubutu kusema hivi sasa elimu Zanzibar imeshuka na hapa naomba Mhe. Waziri, aangalie jaduweli lake alilotupa kuwa hii elimu imeshuka na nini kilichosababisha kushuka, nafikiri atakielewa kwa vile alikuwa mwalimu na najua hii Wizara ataiweza.

Mhe. Naibu Spika, ukiangalia takwimu za matokeo katika ukurasa wa 69, naomba kunukuu Mhe. Naibu Spika; " Watahiniwa walikuwa 1959 mpaka 2015 watahiniwa walikuwa 673" kwa msingi huo idadi ya wanafunzi

waliohitimu kidato cha sita imeshuka kwa kiwango kikubwa, na ukiangalia takwimu hizi katika jaduweli Nam. 6 (C), Idadi ya wanafunzi waliofeli kupitia daraja la nne na la tatu imekuwa ni kubwa. Ukilinganisha na skuli binafsi nini tatizo lake, ushauri wangu kwa Serikali au kwa Wizara hii kuanzia *Primary* sasa hivi umeshafika wakati wa kusomesha kwa lugha ya Kiingereza kwa masomo yote.

Mhe. Naibu Spika, sisi sote ni mashahidi humu kuwa skuli za binafsi zimefanya vizuri, kwa nini zikafanya vizuri, sababu ilikuwa ni kutokana na msingi wa Kiingereza kwa masomo yote, kwa hivyo, ajiandae kupanga utaratibu wa mitaala kufundisha kutoka *Primary* mpaka Sekondari aanzie na lugha ya Kiingereza, asije akaanzia na Sekondari *Form l,* huo ndio ushauri wangu kwa Wizara.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo, nije katika mitaala, mitaala ibadilike, wanafunzi wanafundishwa kwa lugha za Kiingereza nimeshalizungumza hilo, sasa nije kwenye ukurasa wa 23, wanafunzi wa darasa la sita na darasa la saba mwaka jana waliofanya mitihani jumla walikuwa 54,529, waliofaulu katika masomo ya Sekondari walikuwa 50,000, tukiangalia mtokeo ya mtihani wa kidato cha sita mwaka jana kama watahiniwa walikuwa 673, waliofaulu 653, tunakwenda wapi? Hatufiki pahali kwa mwendo huu, hatufiki pahali.

Baada ya hapo nije kwenye Mkopo wa Elimu ya Juu, ukurasa wa 15, wanaoumia Mhe. Naibu Spika, ni watoto wa kinyonge, Serikali ilitakiwa itie bilioni 8.2 lakini ikaja ikatia bilioni 3.6 sawa na asilimia 44, nani kapata mkopo huu na nani kakosa mkopo huu, pesa kidogo na wanafunzi walioandikwa humu nafikiri waliofaidika ni 3,046 wakiwemo wanafunzi 575 ni wapya, ni mtihani, Mhe. Naibu Spika, hapa Mhe. Waziri, aliangalie na aje anipe maelezo kwa umakini.
Mhe. Naibu Spika, kuna wanafunzi wanasoma nje na wanahitaji kupelekewa pesa zao, leo karibu miaka miwili hawajapata pesa zao, ukizingatia wengine ni watoto wa kike, ni mtihani huu Mhe. Naibu Spika, kwa waliofanya *research*.

Mhe. Naibu Spike, nije kuhusu Elimu ya Mjumuisho, ukurasa wa 27. Hapa palikuwa pana bajeti ya kutiwa milioni sitini, Serikali ikatia shilingi laki nane, kitu cha kichekesho hichi, ina maana hawa watu elimu yao itaendelea kushuka au sijui tuseme tutumie lugha gani; hawathaminiwi au vipi, kwa kuwa ni viziwi, shilingi laki nane kutoka milioni sitini! Mhe. Waziri, hapa uje kunifahamisha ili niweze kufahamu, lakini najua si kosa lako, "mbuzi anakula majani kutokana na ukubwa wa kamba yake", lakini milioni sitini kwa shilingi laki nane watasoma wapi watu walemavu au ndio wamekosa bahati, u-*serious*

haupo, yaani umakini haupo, tutakuwa tunapiga kelele tu, kutoka milioni sitini mpaka laki nane ni tofauti kubwa sana Mhe. Naibu Spika, na kama haikutokea kampuni ya *ZANTEL* kusaidia ingekuwa mtihani, tunashukuru kwa kusaidia kitengo hichi, ingezidi kuwa mtihani na Jumuiya wasioona ndio waliosaidia kitengo hichi, watu wawili hao, kama hawakusaidia ingekuwa mtihani mkubwa, ni kitu cha kusikitisha.

Lakini vile vile nitahitaji maelezo kuhusu mambo matatu; kodi ya nyumba shilingi ngapi walimu wanakatwa, *Teaching allowance* shilingi ngapi, na nauli za usafiri, hichi kimekuwa gumzo tokea nilipokuwapo, walimu wanatoka Muungano kuja mjini wanapewa shilingi mia nane, wakati wanatoka Unguja Ukuu kuja Mjini anapewa shilingi elfu moja, sijui masafa gani au kipimo gani kimetumiwa, nitahitaji maelezo.

Lakini nimshukuru jirani yangu Mhe. Shamsi, alizigusa nyumba za jimboni kwangu Jambiani na kama sikuzizungumza hizi itakuwa sijawafanyia haki wananchi walionichagia na kunileta huku, nyumba zile ziko tano, moja kidogo inatizamika, Mhe. Waziri, umefanya ziara baadhi ya skuli na hii nakuomba tufanye ziara, lakini hapa kidogo kuna asilimia tatu, nne nitakuzuia, mimi nilikuwa sina nia ya kuzuia bajeti yako. Bajeti yako iko wazi na imepata wataalam na inafahamika, lakini itakuwa sijafanya haki kwa wananchi walionichagua kwa sababu nyumba zinavuja na cha kusikitisha wanalipa hizi nyumba tokea kipindi nilichokuwepo kile nilipigia kelele lakini Mwenyezi Mungu kwa uwezo wake amenirejesha tena, wala si uwezo wangu, namshukuru, lakini hapa nitahitaji maelezo na hizi nyumba wanalipa.

Kitu cha kusikitisha sana halafu kuna vitabu kipindi kilichopita vilizuiwa humu ndani sijui vimefikia wapi vya Kiarabu na *English* vya *primary*, na dini ilikuwa gumzo sana, hoja hii na hivi vitu havipo hivi sasa, hawawezi kusomeshwa watoto *primary*.

Waziri hili ukija nalo ulifanyie utafiti. Lakini Mhe. Shamsi Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Magomeni alizungumza kuhusu Skuli ya Kibuteni, Skuli ya Kibuteni ni sawa sawa na Skuli ya Mtule.

Niishukuru sana Kampuni ya *RANS* kwenda kuokoa jahazi lile. Skuli imejengwa miaka 3 haijafika inavuja, utaalamu gani mtotumia hizi pesa za walipa kodi au ndio kwa kuwa msaada tena hatuuthamini, skuli imejengwa juzi miaka 3 Mhe. Naibu Spika, inavuja. Wanafunzi baada ya kusoma wakati wa mvua wanatafuta wakati kutoa maji nje.

Skuli ya Kibuteni hata asilimia 35 haijafika miaka 3 jengo limekaa vile vile, mikataba gani mnayotumia Wizara ya Elimu bado hatujasoma tu kuhusu suala hili. Si mara ya kwanza, si mara ya pili, si mara ya tatu tunaendelea na mashaka haya, hatuwezi kufika mbele skuli imekaa kama pambo pale Kibuteni, mbao zile za zege zimeshaanza kuoza kule. Kama mnalijua mshalikagua sawa.

La mwisho la kumalizia kuhusu Chuo Kikuu cha SUZA kuna harufu harufu ninasikia hiki Chuo huenda wakakataa kukiunganisha.

Mhe. Waziri nikushauri Chuo cha SUZA kimefanya kazi kubwa kiendelee kubaki vile vile kama kilivyo. Huu ni ushauri wangu. Nafikiri umesoma pale, ulikuwepo pale unaujua umuhimu wa Chuo hiki, Chuo hiki kibaki vile vile usije ukaunganisha na vyuo vyengine kama vya Chwaka vile aa. Huu ni ushauri utapima mwenyewe, ni mtu uliyesoma kuliko mimi Mhe. Waziri lakini mapendekezo na hii Kamati niliwahi kufanyia kazi.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Naibu Spika, nimezuia kama sinia mbili mpaka tano ili nipate kujibiwa vizuri kutokana na wananchi wangu walionituma niweze kupitisha bajeti hii panapo uhai.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Jaku, Waheshimiwa Wajumbe kuna jambo ambalo nilikuwa nataka niwaombe tufanye mfumo huo kwa wale ambao watapeleka kwa maandishi kwa Mhe. Waziri basi majina yao au ambao wameshapeleka, tunataka kuanzisha mfumo wa kwamba wale ambao wataleta lazima kwanza ipitie kwa Spika, ili tuweze kuandika orodha yetu ili kuwe na uwezo mtu ambaye apeleke kwa maandishi aweze kutambulika wakati anapiga buti, sijui mumenifahamu Waheshimiwa.

Kwa hivyo naomba wale wote ambao wameshapeleka waniletee majina yao niweze kuyarikodi katika *list* yangu. Lakini mfumo huo sasa utaendelea kwa maandishi yote yatapitia kwa Spika, halafu Spika, ndiye atapeleka kwa Mhe.Waziri. Naomba tuendelee.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa mbele ya Baraza lako tukufu na kuchagia mambo machache katika Wizara hii ya Elimu, hasa nikizingatia kwamba Waheshimiwa wenzangu wengi wameshangia na mimi naweza kurudia baadhi ya mambo kidogo.

Mhe. Naibu Spika, nampongeza sana Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Manaibu Katibu Wakuu, Wakurugenzi wote na Makamishna mbali mbali pamoja na walimu wakuu na wanafunzi wetu.

Mimi kwa upande wangu niseme tu kwamba wizara hii naiunga mkono kwa asilimia mia moja, hasa tukizingatia kwamba kila aliyekuwemo humu ndani ya Baraza na baadhi ya walioko nje ya Baraza inawagusa kwa asilimia yoyote katika mahitaji yake. Kwa hivyo nawapongeza tuwape nguvu viongozi wetu hawa waende vizuri na watendaji wao ili elimu iwe nzuri zaidi katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, nitazungumzia suala la Chuo cha Ualimu, Nkrumah. Chuo hiki ni cha historia katika nchi yetu na walimu wetu wengi wamepata elimu yao hapa na kuwa walimu bora hasa kutokana na maendesho yake mazuri na utaratibu mzuri, kwamba mwalimu akisomeshwa katika Chuo maalum hasa Chuo kinachotambulika cha Nkrumah basi hata maadili wanasomea huko vizuri na wanajua wajibu wao katika kuwaendeleza wananchi wetu. Lakini la kusikitisha hivi sasa Mhe. Naibu Spika, Chuo cha Ualimu hasa kinachotambulika Zanzibar mimi naona hakipo.

Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atueleze, Chuo hiki Mhe. Naibu Spika, kimezalisha walimu wengi na mpaka sasa kuna walimu wengi ambao wamemaliza mwaka 2007 mpaka 2008 wamekaa mitaani hawana ajira yoyote.

Ningemuomba Mhe. Waziri hawa walisomeshwa kwa gharama na wamekwenda Chuoni wenyewe kwa gharama zao, lakini yanapotokea mahitaji basi wapewe kipaumbele ili na wao wawe katika walimu ambao wametoka Chuo kinachotambulikana hapa kwetu Zanzibar.

Jengine Mhe. Naibu Spika, huko nyuma ninakotoka mambo mengi nimefilisiwa, waliowahi wamewahi kunitangulia lakini na mimi nitapata kidogo kuyasema. Kuna malalamiko kama baadhi ya waheshimiwa walivyosema kwamba kuna walimu wetu wanaosomesha masafa marefu, yaani nachukulia masafa marefu kutoka mjini kwenda vijijini. Kwa mfano Mahonda, Kiwengwa, Dunga, Uroa mfano tu hiyo Mheshimiwa lakini nauli inayostahiki hawalipwi. Kwa mfano ukitoka hapa ukienda Mahonda mfano unalipa nauli shilingi elfu moja, bahati nzuri au mbaya walimu hawa huwa wanalipwa shilingi mia saba au mia sita. Namuomba sana Mhe. Waziri hili walifuatilie na wajue ukweli huo kama upo, lakini wakitaka ushahidi kwa kuwa tunakaa na walimu hao tutawapa maelekezo, na walimu hao wawalinde tu kwa usalama wao, wako tayari kutoa ushahidi.

La pili kutokana na hiyo nauli kuna mengine hutokea hata siku siku 26 au 24 tunasema katika mwezi huwa hawazipati, siku 22 au ishirini na ngapi, wanakatwa siku 15 wanapewa au siku 17 na hili lipo. Nawaomba Waheshimiwa Mawaziri wetu na Naibu wake ni watu waadilifu ninawaamini, haya wakitaka tuwape ili kuwasaidia walimu wetu wasipate bughdha wanapokwenda.

Mhe. Naibu Spika, jengine ni suala la likizo, walimu wetu wanalalamika kwamba fedha za likizo hawapati, hata wakipata siku nyengine usumbufu umetokea miezi mitatu, minne, mitano ndio anakuja kulipwa baadae lakini kwa asilimia kubwa hawapati kabisa.

Namuomba Mhe. Waziri hii aje atupe maelezo mazuri, tujue hatma ya walimu wetu hawa ambao na wao kazi yao kubwa kuhakikisha baada ya kazi ngumu kupata mapumziko, lakini ile stahili yao na wapate kwa ajili ya maisha yao kama sheria ilivyoweka.

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo nataka kulizungumza hapa niishukuru Serikali lakini ninamshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Mheshimiwa wetu kayaleta mambo mengi mazuri, mojawapo la kusema elimu ya msingi yote bure. Hili suala tusilichukulie mashara, sote tunategemewa katika majimbo yetu harakati za wazazi wetu au wapiga kura wetu wanajua shida walizokuwa nazo kwa watoto huko nyuma, na mpaka leo lakini asilimia kubwa ile ya kero imepungua. Kwa hivyo hii nampongeza Mhe. Waziri lakini naomba Wizara isimamie vizuri zoezi hili liendelee bila ya matatizo.

Nikilichukulia hilo nachukulia pia kwa wazee kuwa elimu bure hii nitakujakusema katika Wizara yangu ya Kazi, Wanawake, Watoto, Vijana na Wazee nitakuja kuisemea siku hiyo kwa sababu iko katika taarifa yetu ya Kamati. Lakini niseme tu kwamba hili naomba tuendelee. Lakini katika sekondari ningemuomba Mhe. Waziri, Mhe. Rais alitoa ufafanuzi kwamba kutoka kidato cha kwanza nafikiri mpaka cha pili au cha nne sina uhakika sana, aje atoe ufafanuzi kwa sababu baadhi ya wanafunzi wanalalamika kuna makato ambayo hawayaelewi, ili kuweka sawa na wananchi wafahamu, ili lielekezwe ili watu wajielewe nini cha kuchangia au cha kusaidia. Huwezi kuichangia elimu, lakini kusaidia imo. Kwa hivyo akitoa ufafanuzi wananchi wetu wataelewa juu ya suala hili.

Mhe. Naibu Spika, pia niipongeze wizara au serikali yetu kwa jumla katika kuhakikisha kwamba elimu yetu ya sekondari inaongezeka kwa kasi, na ndio maana ikasema katika kitabu hiki kuna skuli kumi zitajengwa katika maeneo mbali mbali.

Mimi kwanza naipongeza serikali, skuli ya mwanzo kuipata na mimi katika Jimbo langu la Kijitoupele. Jimbo letu la Kijitoupele sehemu ya Kwarara chini ya msaada au makubaliano ya Korea ya Kusini, wanajenga skuli nzuri ya kisasa, na wanafunzi watafaidika hapo lakini pia patakuwa na Chuo cha Habari katika kushughulikia mambo ya elimu hapo hapo. Ningewaomba sana Waheshimiwa Mawaziri wetu na Naibu wake, kila panapowekwa haja hii basi tuisimamie vyema, lakini na Mwakilishi, Mbunge na Madiwani ni kazi yetu. Sisi tunasema tu kwamba kwa upande wangu mimi naishukuru serikali kwa asilimia mia moja kwa jambo hili zuri.

Mhe. Naibu Spika, kwa bahati mbaya Jimbo la Kijitoupele, jimbo jipya lakini tulikuwa hatuna skuli hata moja katika skuli za serikali, *private* zimo nyingi. Ukiacha skuli ya Pangawe jirani sisi hatuna skuli yoyote tunayokwenda nayo. Kwa hivyo hili ninamuhakikishia Mhe. Waziri na Naibu Waziri kama Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Kijitoupele nitaisimamia skuli hii kwa uangalifu sana na kwa uwezo wangu wote, kuhakikisha inakwenda sambamba kama ilivyotakiwa imalizike, ili vijana wetu haraka wapate elimu kusoma pale na kuondokana na masafa marefu.

Mhe. Naibu Spika, nina wazo jengine ninaiomba serikali kupitia Wizara ya Elimu, tumesema tu kwamba wanafunzi wa darasa la kwanza mpaka la tatu, la nne, wanakwenda masafa marefu. Mwanafunzi kutoka Kwarara yaani sehemu mbali mbali, tuseme mbali kabisa anakwenda skuli Kijitoupele mashine ya maji ni mbali na kuna siku za mvua ni hatari. Kwa hivyo pamoja na kujenga sekondari, hii siingilii, mambo mengine tutayazungumza baadae, lakini kwa kuwa wanafunzi wetu wadogo wanakwenda mbali, sekondari watakuwa wapo karibu tunashapata kiwanja mimi na Mbunge au uongozi wetu wa jimbo, tunataka kuanza skuli yetu ya msingi, serikali tunajua utaratibu wetu tupige *foundation* tumalizie kila tunapotakiwa, baadae wanafunzi wetu wamaliziwe skuli hiyo haraka ili tuhakikishe kwamba 2017 mwakani haitomalizika lakini hata kama katikati waje wakatishwe watoto waendelee huko baada ya kumalizika, skuli hiyo imalizike na wasome huko, kuwaondolea adha kwenda mbali wanafunzi wetu. Azma hiyo tunayo na kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu atatusaidia tutalifanikisha hilo.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala ambalo hili kila leo na mimi nalitaka nilipigie kelele kama wenzangu wamesema na mimi nalisemea tena. Nchi yoyote duniani historia ni kama familia, historia katika nchi ni jambo la msingi kuliko lolote. Huwezi kujijua uko wapi, unatoka wapi na unakwenda wapi. Naiomba serikali somo la historia jinsi tulikotoka, tulipo na tunakokwenda vijana wetu wasomeshwe maskulini ili wapate kujitambua.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilibahatika kwenda kusoma Urusi namshukuru Mwenyezi Mungu, naishukuru Serikali yangu hii ya Chama cha Mapinduzi, wakati huo ni JWTZ.

Jambo la mwanzo unapofika kule kama wiki mbili tatu au mwezi mzima unasomeshwa historia ya Warusi, vipi walivyoipata na hata ukitoka ugeni wowote ukienda katika nchi ile mpaka hivi sasa kuna mikate yao wanaita kheleb, hiyo utaila ukitaka usitake, ni mikate ya boflo ambayo inawekwa kwenye friji kama miezi miwili mitatu, lakini wewe kwanza chakula huli, wakuwekee ile upate. Maana anakwambia yeye ndio historia yetu ya ushindi wa nchi tulivyopindua, walipopigana vita.

Kwa hivyo nawaomba sana Mhe. Waziri na Naibu Waziri turudi nyuma tuangalie tuone nini historia, historia ndio inayowapatisha tabu vijana wetu sasa hawajielewi katika nchi yetu. Na kama vijana wetu wanaielewa historia ya nchi yao hii basi wasingepata tabu hadi leo.

Mhe. Naibu Spika, mimi hapa nilipo niliyoyaona mimi sio vijana wetu wa leo, mimi nimekulia katika Afro Shirazi na mwanzilishi wa CCM. Kwa hivyo, madhila mengi niliyaona kwa kuwa mdogo niko Kiwengwa unakaa miezi mitatu minne gari huioni. Hiyo siku ya kuja gari ya Mzee Saad wa Upenja hatulali kucha Kiwengwa. Mzigo wa chakula kutoka Kinyasini mpaka Kiwengwa unapelekwa kwa baiskeli, leo vijana wa Kiwengwa wote wana magari yao na kila kitu chao, hayo ni maendeleo katika nchi yetu. Lakini hao hao bado wamo wengine historia hawaijui na hawaamini kama haya kweli yalikuwa yapo.

Kwa hivyo, nasema kwamba tu Mhe. Naibu Spika, namuomba sana Mhe. Waziri na Naibu wake na watendaji wote wa Wizara ya Elimu, somo la Historia litafutiwe pa kuingizwa, sio somo la kuendelea, litoe historia ya nchi yetu tulikotoka, tulipo na tunapokwenda, hapo tutapata viongozi wazuri baadae katika nchi yetu, na hao vijana wetu wanaopaparika kwa kubabaishwa watajijua kumbe huku tunapotea tuelekee huku.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache narudia tena kauli yangu sote tunahitajika katika kuwasaidia walimu, walimu wetu wasaidiwe, wawezeshwe, ili wafanye kazi zao vizuri. Lakini pia wizara katika maombi yake naishauri sana serikali wapewe walichoomba, ili wafanye kazi zao vizuri na elimu yetu itukuke, iwasaidie vijana wetu kwa maslahi ya taifa letu.

Baada ya hayo nashukuru naiunga mkono hotuba hii asilimia mia moja sina matatizo. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kunipa nafasi hii nami niwe mmoja katika wachangiaji wa Wizara hii adhimu ya elimu.

Kwanza kabisa nianze kwa kusema kwamba naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Imeelezwa vizuri imeandikwa vizuri na wataalamu waliobobea, na mimi nampongeza sana Mhe. Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa wizara hii. Kwani hii ndio wizara iliyotulea sote hapa, tumeanza kusoma tangu wadogo tumeendelea hadi kufikia hapa na bado tunaendelea.

Mhe. Naibu Spika, niruhusu kusema kwamba elimu ni nguzo imara na nyenzo thabiti ya maendeleo yanayostahiki, maendeleo yote yanahitaji elimu, elimu ni mkombozi wa watu wote. Unawakomboa kutokana na ujinga, maradhi pamoja na umaskini.

Mhe. Naibu Spika, sote tunaelewa kwamba wanafunzi waliohamasika au hamasa za wanafunzi ni msingi wa ufaulu katika mitihani yao, na kiashiria tosha kinachoweza kueleza hali halisi ya elimu kwa wanafunzi. Matokeo yasiyoridhisha katika elimu hususan kwa wahitimu wa madarasa ya saba, kidato cha nne na hata kidato cha sita katika miaka ya karibuni yanatosha kueleza hali isiyoridhisha inayoikabili jamii na sekta ya elimu kwa jumla.

Mhe. Naibu Spika, naomba uniruhusu nitaje mambo ambayo yakifanyiwa kazi ipasavyo yanaweza kunusuru hali ya elimu kwa vijana wetu, na kuwafanya wapate ujuzi utakaowasaidia waingie katika soko la ajira, ambalo hivi sasa lina ushindani mkubwa. Halikadhalika elimu itawasaidia sana kukabiliana na changamoto za maisha.

Mhe. Naibu Spika, mambo yenyewe haya nimeyatoa kwenye kitabu hiki cha bajeti, ambayo wameeleza kuyaboresha, na nitayataja moja moja, ni mambo saba, yako mengi lakini nimeyataja saba na nakubaliana na maboresho watakayoyafanya. Lakini kama sikupata nafasi ya kueleza moja moja basi

nasema huo uboreshaji uongezewe kasi, na hiyo kasi yenyewe iwe kubwa ili ulete maendeleo kwa ufanisi zaidi. Mambo yenyewe ni haya.

Kwanza kuna Sera ya Elimu imeelezwa humu sera ya elimu na mipango. Pili kuna uboreshaji wa mazingira ya skuli kama *direct* au *indirect* lakini imetajwa, vifaa vya kufundishia, lugha inayotumika kufundishia, vitabu, mitaala na walimu. Nimeona niyachukue haya kwa sababu haya ni mambo muhimu sana.

Mhe. Naibu Spika, nikianza na Sera ya Elimu na Mipango. Hii lazima ilenge kwenye kuwashirikisha wadau wote ikiambatana na kuboresha mapungufu yote yaliyopo bila ya malumbano au kuingia itikadi za kisiasa zenye lengo la kupinga au kuvuruga juhudi za maendeleo. Maana kuna itikadi za kisiasa nyengine zinajenga, kwa hiyo sio vibaya zikafundishwa kule skuli, lakini kuna itikadi nyengine za kuvuruga, wenzangu wamesema hapa, ni kweli huko skuli kuna siasa. Wale ambao wanakwenda kwenye upinzani wanawagawa wanafunzi, hawa wako huku na hawa wako huku matokeo yake ni kuwapotosha. Kwa hiyo, Wizara ya Elimu iliangalie sana jambo hili, kwamba pale walimu wamepelekwa kwenda kusomesha sio kufundisha siasa za kibaguzi.

La pili nilisema ni uboreshaji wa mazingira ya skuli. Mazingira ya skuli yanahitaji sana kuboreshwa ili iwe kivutio kwa wanafunzi kuhudhuria kila siku na kufanya vyema katika masomo yao. Hii ni pamoja na kuendelea au kuandaa michezo ya aina mbali mbali, kuwaandalia mambo ya sanaa na utamaduni, kuweka mazingira safi na kuyavutia pamoja na kuwapatia zawadi mbali mbali. Maana yake sio lazima afanye vizuri ndio umzawadie, ukimpelekea kizawadi kidogo tu mwanafunzi anafurahi siku ya pili anataka kwenda. Kwa maana anaonekana kwamba anaona walimu wangu wananijali, kwa hiyo *attendance* itakuwa ni nzuri.

Aidha, kuwapa nafasi waoneshe mambo wanayoyamudu na ambayo yatawafurahisha wenzao ni jambo la faraja pia. Sasa hivi nakwenda haraka haraka ili niende kwa wakati.

Pia nigusie kwenye *vifaa* vya kufundishia. Vifaa vya kufundishia viko vya aina nyingi, kuna *black board* hivi lazima pia viwe katika viwango vinavyotakiwa. Utakuta ma-*black boards* mengine yameandikwa, mengine yamefutwa, ukiandika tena hata hiyo chaki haioneshi yanakuwa ama hayana rangi au yamechoka, lakini ni vizuri kuwa na vifaa ambavyo kwa kweli vitakuwa vizuri vinavyoweza kuvutia hata wanafunzi. Nyenzo na vifaa vya kufundishia lazima ziwepo na za kutosha na katika hali nzuri.

Ukosefu wa vitabu ni moja kati ya tatizo kubwa hususan vile vya sayansi, aidha, kuna upungufu au ukosefu wa maabara katika skuli zetu nyingi sana.

Mhe. Naibu Spika, haya ni mambo muhimu sana, kuwaandaa wanafunzi ili wawe walimu bora au wawe watendaji bora katika maisha yao ya baadae. Ni vizuri pakawekwa mkazo kwenye upatikanaji na uwepo wa mahitaji yote ya kufundishia.

Jengine nililolisema hapa ni lugha. Lugha hii ni muhimu sana, lugha ni urithi wetu tangu mababu na mababu, tangu ilipoumbwa dunia tunaitumia lugha. Lugha tunaitumia kwa kusaliamiana, kupashana habari, kuelezana matatizo, kufarijiana na kadhalika na kadhalika. Lugha inayofaa ni lazima iwe ile inayoweza kutoa mwelekeo bora kwa kufahamika kwa urahisi katika somo husika. Ni budi wanafunzi waelimishwe vya kutosha ili waweze kuimudu vyema lugha inayotumika, kama ni Kiingereza basi tuhakikishe wanafundishwa Kiingereza, jambo la kusikitisha utakuta *form six* Kiingereza chake hakifahamiki na hajui. Sasa kama hajui Kiingereza na mtihani unafanya kwa Kiingereza atawezaje kufanya mtihani.

Kwa hiyo, lazima tutie mkazo sana wakijue Kiswahili kwa yale masomo ya Kiswahili wakijue hasa, wakienda wakifanya mtihani wa Kiswahili wanajua hapa pameelezwa nini kwa hiyo nijibu nini. Kiingereza nacho ni hivyo hivyo haitakuwa busara kuwafundisha jambo lolote kwa kutumia lugha wasiyoijua au wasiyoifahamu, kwani hii inaweza kuwafelisha hata katika mitihani yao. Walimu na wanafunzi wenyewe wanapaswa wazielewe lugha zinasomeshewa.

Mhe. Naibu Spika, sasa nigusie kwenye vitabu. Ili usomeshe lazima uwe na kitabu, na kitabu lazima ukisome, lakini vitabu hivi vina watunzi wa aina nyingi. Kitabu cha sayansi cha aina moja kinachoeleza tuseme ini la mwanadamu kikitungwa na watu tofauti kitabu kile kinaweza kikawa tofauti kimaelezo kidogo. Kwa hivyo, ni vizuri sana tutafute kitabu ambacho pengine watunzi wake wawili watatu ambao wamekwenda sambamba na yale mahitaji tunayoyataka, ili kusijekuwa na *confusion,* akaenda akasoma kitabu cha ini pahala pengine ambacho hakikubaliki maelezo yake sio anafelishwa mwanafunzi. Kwa hivyo, basi uchunguzi wa vitabu vinavyotumika ni jambo litakalosaidia sana kupatikana kwa vitabu vitakavyowasaidia kuondoa tatizo hilo kwa wanafunzi, hasa ukizingatia kwamba tumo kwenye soko huria, waandishi wengi hujitokeza wakaandika vitabu tu hata kama hajui lakini aandike tu ilimradi kitabu chake naye kitoke. Kwa hiyo, tuangalie sana vitabu tunavyosemesha viwe ni vitabu vinavyoeleza kitu kimoja, isiwe huyu kaeleza hivi, huyu kaeleza mwanafunzi anasoma huku anajiandaa mtihani ameshasoma

kumbe anakwenda kule hawezi kujibu maswali yaliyokuwa kwenye kitabu kingine ambacho hakukisoma.

Kuhusu mitaala yetu hii ni vyema tukaiboresha ili iende sambamba na mahitaji ya jamii na inayoendana na elimu ya kujitegemea. Hii itawezesha wahitimu kupata elimu itakayowasaidia kujiajiri wenyewe pale wanapomaliza masomo.

Vile vile nigusie tena walimu ambayo hii itakuwa ni ya mwisho nakwenda haraka haraka, kama watahitaji waheshimiwa walimu unajua wanajua sana mambo mengi, kama watahitaji tukae tuyazungumze moja moja tuyafafanue basi niko tayari waniite tukae pamoja.

Nimeshakaa nao sana walimu, nafahamu siku za nyuma tunakwenda tunapeana mawazo hasa wakati ule walipofeli vijana wa darasa la saba, walipokopia wakafutiwa mitihani yao wakati ule tulikwenda sana Wizara ya Elimu kujaribu kutetea tetea. Sasa walimu…

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa umebakisha dakika nne za kumalizia.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Zinatosha Mheshimiwa wangu.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu walimu katika majimbo yetu hususan kama jimbo langu la Mtopepo pale nina skuli mbili, Skuli ya Mtopepo yenyewe na kule Kidatu juu. Katika skuli hizi walimu hawatoshi, hakuna walimu, walimu ni kidogo sana, kuna mahitaji makubwa ya walimu. Sasa ukiangalia pale nimefanya *study* ndogo tu nimeona kuna walimu wenye *degree* wapo pale pale, kuna wenye *diploma*, kuna wenye *certificate* hawajaajiriwa nao wanaishi kwenye jimbo lile lile ambapo haitakuwa kazi kubwa kwao kupewa nauli wakaenda wapi, wakasafiri wapi. Tunaomba na hili Waheshimiwa tuliangalie sana ili tuweze kuajiri walimu wale waliopo pale pale kwenye jimbo lile ili waendeleze elimu. Kwani imeonekana kwamba kwa sababu ya ukosefu wa walimu, wazee wengi wanawahamisha watoto wao wanakwenda skuli za mbali.

Sasa niseme tu kwamba elimu bora huunda ualimu bora ambao kutokana na mafunzo bora na ya kutosha. Kwa hiyo, semina na mafunzo mbali mbali kwa walimu huweza kupanua wigo wa uelewa wao kielimu.

Aidha, mazingira mazuri ya kazi na ya kuridhisha huwaweka walimu katika hali ya utulivu, makaazi na kazi yao ya walimu lazima yaboreshwe, tena yaboreshwe sana ili yawavutie katika kazi yao.

Mhe. Naibu Spika, kuna jambo jengine lile la *supervision* kwa walimu hata kwa wanafunzi ni vizuri ifanyike mara kwa mara, ili kuhakikisha kwamba yale malengo yaliyowekwa, yale yaliyokusudiwa kutekelezwa basi yanatekelezwa kwa vile ambavyo yamekusudiwa. Kwa vile Mhe. Naibu Spika, amenambia hapa muda wangu umekwisha, na mimi nilitaka kuendelea sana lakini naheshimu muda, kwa hiyo niseme tena kwamba nawapongeza sana Wizara ya Elimu na Mwenyezi Mungu awasaidie sana waende vizuri na naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nitawapa waheshimiwa wengine wawili na baada ya hapo naomba ambaye hakusikia jina lake alete kwa maandishi, kwa sababu sasa hivi baada ya hapo tutawataka mawaziri wachangie kwa ajili ya kufanya majumuisho ya Naibu pamoja na Mhe. Waziri. Mhe. Bi. Panya Ali Abdalla nitafurahi sana ukitumia muda mdogo mheshimiwa ili na wengine wapate nafasi.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia uhai tukaweza kukutana mahala hapa, lakini pia nichukue fursa hii kukupongeza wewe na mimi kunipatia nafasi japo chache nikaweza kusema machache kwa sababu wengi wameshasema mengi.

Pia, nichukue fursa hii kumpongeza kwa dhati Mhe. Waziri na Naibu Waziri na watendaji wao wote kwa kazi kubwa na nzuri kabisa, na Mwenyezi Mungu atawajaalia kila la kheri *in shaa Allah*.

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze mchango wangu katika mikopo ya elimu ya juu ambayo wanapatiwa wanafunzi. Wenzangu wamelichangia kwa kina jambo hili na mimi namuomba Mhe. Waziri aliangalie sana jambo hili, kwa sababu kuna wanafunzi inaonekana hata mikopo inachelewa kulipiwa kule katika vyuo wanavyosoma. Kwa hiyo, wanapomaliza wanafunzi wanacheleweshwa kupewa vyeti vyao kwa sababu ya kuonekana hawajalipiwa.

Pia, wenzangu wamesema sana kuhusu fedha za kujikimu. Mhe. Naibu Spika, naomba wazingatiwe kuna watoto wanyonge sana ambao wanashindwa kujitimizia mahitaji yao.

Mhe. Naibu Spika, pia niishauri wizara kwa wale wanafunzi wanaosoma nje ya nchi basi kuangaliwa masomo wanayosoma ikiwa fani hizo hapa nchini zipo, basi si busara tukawasafirisha watu kuwapeleka huko wakati hapa huduma ile

inapatikana. Tujitahidi huduma hiyo tuitoe hapa ili fedha zile ziweze kusaidia kwa mambo mengine.

Mhe. Naibu Spika, niende katika suala zima la hatimiliki. Suala hili kwa kweli katika wizara nyingi inaonekana halipewi umuhimu wake.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka kujua kwa sababu kuna chuo hiki, taasisi nyingi ambazo ziko katika Wizara ya Elimu hasa kile Chuo cha Kiislamu ambacho muda mwingi kinakuwa kikisemewa katika Baraza hili kwamba bado chuo kile hakina hatimiliki na kilikuwa na eneo kubwa kabisa ambalo kwa sasa limeshavamiwa.

Mhe. Naibu Spika, nataka kujua utakapokuja hapa kunihakikishia kama chuo hicho bado hakijapata hatimiliki, na kuja majengo mangapi ambayo bado yaliyo chini ya wizara yako ambayo hayana hatimiliki au na mangapi yameshapatiwa hatimiliki kwa kuona umuhimu wa jambo hili ili kuepusha ule uvamizi. Na tunasema tunaweza labda eneo tukakosa kulizingia labda kwa ukuta au kwa nini lakini tunaweza tukaweka angalau viguzo vikaweza kuhifadhi hilo eneo ili lisije kuvamiwa.

Mhe. Naibu Spika, niende katika sekta hii ya ukaguzi. Wenzangu nao wameigusia na mimi nataka niseme kama sekta hii ni muhimu sana. Sekta hii inapokosa kufanya kazi zake vizuri maana yake mimi naweza kusema hata hilo suala la ualimu halipo.

Mhe. Said wakati anachangia hapa alieleza kama mwalimu lazima awe na mabuku manne wakati anaingia darasani. Sasa iwapo sekta hii haifanyi kazi ya kumkagua mwalimu kwa hiyo mwalimu huyo ataingia kwa kujiamini hana zana yoyote ambayo kajitayarisha nayo kwa kwenda kumfundisha mwanafunzi.

Mhe. Naibu Spika, hili suala la ukaguzi kwa sasa mimi naliona liko kiujumla jumla ambalo haliwafikii hasa wale walimu tunaopaswa kwenda kuwakagua. Mimi naishauri serikali juu ya suala hili kwamba wale wakaguzi tuwafanye wawepo kiwilaya, kwa sababu watakuwa wapo karibu na maeneo wataweza kufanya kazi vizuri na ile elimu bora ambayo tunailenga kuikusudia tunaweza tukaifikia. Lakini ukaguzi huu wa jumla jumla haiwezekani kuyafikia maeneo hayo yote.

Mhe. Naibu Spika, zamani kulikuwa walimu wakuu pia walikuwa wakiwakagua walimu wao, pia kuna ukaguzi wa walimu wakuu. Sidhani jambo hili kwa sasa kama linafanyika kama inavyoonekana, kwa sababu kwa sasa

wanaonekana walimu pamoja na juhudi kubwa wanazifanya, lakini utaona walimu wanakwenda skuli wakati wanaotaka wao hali ya kuwa vipindi vinawapita. Sasa kama ukaguzi ule walimu wakuu unafanyika basi walimu wasingepata fursa hizi za kuwa mwalimu aingie skuli wakati anaoutaka.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia wenzangu wamezungumza kwamba walimu wanapata fursa ya kuzungumza siasa, kama wanakagua walimu wakuu jambo hili lingekuwa hapana. Kwa sababu walimu wakuu wanakuwa wapo pale pale maskuli na mwalimu asingepata nafasi ya kufanya hivyo. Kwa hivyo, mimi naomba ule ukaguzi wa walimu wakuu pale skuli kama mwalimu mkuu na kuwakagua walimu wake ifanyike, kwa sababu kuna mambo mengi yanafanyika pale skuli ambayo walimu hawafanyi kazi ipasavyo na sisi lengo letu ni kuiboresha elimu.

Mhe. Naibu Spika, niende katika hii huduma ya urajisi wa elimu. Wametueleza katika kitabu hiki kama kuna skuli 128 ambazo zimekaguliwa kati ya hizo 83 ni za Unguja na 45 ni za Pemba. Niseme kuna skuli ngapi ambazo bado hazijasajiliwa na ni vipi wanafikiwa hawa katika utekelezaji wa sheria na sera na maagizo yale ya Wizara, wakati ukizingatia suala la muhimu hili la mwanzo tu la kusajiliwa wakatambulikana halijafanyika.

Halafu wakaeleza kuna skuli thalathini za hapa Unguja na skuli kumi na tatu za Pemba na kumi na sita za skuli binafsi zimepatiwa usajili wa muda, lakini moja imepatiwa usajili wa kudumu, nilitaka kujua pia ni skuli gani hiyo.

Mhe. Naibu Spika, jengine niende katika Wilaya yangu ya Kaskazini B. Mhe. Naibu Spika, ndani ya Wilaya yangu kulikuwa na skuli ya sekondari ya Muwanda. Wakati wa ugawaji wa mipaka skuli hiyo sasa imeingia katika Wilaya ya Kaskazini A. Je, sisi katika Wilaya ya kaskazini B ni vipi Wizara inaweza kutuzingatia kuipata ile skuli yetu ya sekondari ili tukienda sawa sawa na mgao ambao Rais mwenyewe alikuwa ameupanga kila Wilaya kuwa na skuli ya sekondari.

Mhe. Naibu Spika, nilitaka nisichukue muda mrefu, na mimi kwa kweli naomba wenzangu waendelee kuchangia kwa kuboresha suala la elimu, kwa sababu suala hili ndilo ambalo niseme Wizara hii ndio mfinyanzi wa kila kitu, kwa sababu Wizara hii ndiyo inayomfanya kila mtu kujitambua. Lakini nilitaka niende katika tathmini ya vipindi vile vya tucheze tujifunze.

Nasema labda katika tathmini yenu mmeona ni vipi mafanikio yanapatikana katika kipindi hichi kwa ule muda ambao mnakitoa, maana nahisi ule mda

unaotolewa ni muda ambao watu wote wapo katika harakati. Je, lile lengo la kuweko hichi kipindi kinatusaidia na mafanikio gani labda yamepatikana.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia walimu hawa nasema kwa nini Wizara isiandae ikawachukua walimu hawa kuwaajiri na wao, kwa sababu tayari wameshapata mafunzo wataweza kusaidia katika skuli zile za maandalizi.

Mhe. Naibu Spika, pia, niende katika upimaji na tathmini. Katika upimaji na tathmini kumeonesha pale kijumla jumla skuli zile za darasa la sita na la saba ambazo zimefanya mitihani yake. Sasa mimi nilitaka tu nipatiwe uchambuzi wa kuweza kujua ni darasa la sita walikuwa wanafunzi wangapi na la saba walikuwa wangapi ili tuweze kujipima kiwango cha ufaulu, hasa ukizingatia wanafunzi hawa walisoma bila ya kuwa na vitabu kwa mwaka huu ambao limejitokeza suala hilo.

Mhe. Naibu Spika, niende katika walimu wa maandalizi. Wenzangu wamezungumza na mimi nilitaka niligusie. Kuna walimu wachache ambao wenye sifa ya kusomesha katika skuli hizi za maandalizi, na kwa mujibu wa Sera ya Elimu ya 2006 kila penye skuli ya msingi pawe na skuli ya maandalizi, lakini walimu ndio wanaonekana wachache, lakini nyinyi wenyewe kama wizara muda mwingi sana mumesomesha walimu wa maandalizi katika skuli ile ya Saateni. Je, ni kwa nini walimu hawa msiwaajiri wakaweza kuziba lile pengo katika skuli hizi za maandalizi kuliko kuanza kujipanga tena upya, isipokuwa wao mkawapa masharti ya kujiendeleza katika zile fani ambazo watazianzisha wao pale.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli mimi mchango wangu haukuwa mkubwa, lakini niwapongeze tena, na niwatakie kila la kheri, kwa sababu hii Wizara ndio Wizara mama, ambayo mtu lazima usome uweze kuingia katika fani yoyote.

Kwa hivyo Mheshimiwa naunga mkono kwa asilimia mia moja ya hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kaskazini tunaiunga mkono. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Bi. Panya. Mchangiaji anayefuatia ni Mhe. Shamata Shaame Khamis, na baada ya hapo Mhe. Abdalla Maulid Diwani, tuna wachangiaji wawili wa mwisho ambao ni Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa) na Mhe. Simai Mohamed Said. Mhe. Shamata hayupo kwa hiyo atachangia Mhe. Abdalla Maulid Diwani na baada ya hapo watachangia niliowataja hapo.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Naibu Spika, na mimi kunipa fursa hii adhimu leo kuchangia katika Wizara ya Elimu.

Awali ya yote sina budi kumshukuru Mungu kunijaalia afya kusimama kwenye Baraza lako Tukufu hili kuweza kuchangia.

Vile vile, natoa shukurani zangu za dhati au pongezi kwa Wizara, kwa kuleta hotuba nzuri yenye maadili makubwa sana, uongozi uliotukuka katika Baraza letu hili tukufu pamoja na aliyeisoma hotuba, kasoma kwa makini kabisa kila mmoja kafahamu Mwenyezi Mungu amzidishie asimamie vizuri malengo yake.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuendelea mimi ni Mwakilishi wa Jimbo la Jang'ombe, na katika Jimbo langu la Jang'ombe nimebahatika kuwa na skuli mbili za Serikali katika Jimbo la Jang'ombe, skuli mbili kwa nne. Lakini skuli zile kwa muda mrefu sana zimekuwa yatima, nathubutu kusema zimekuwa yatima, kwa sababu mara tu baada ya kumalizika uchaguzi nilifanya ziara ya kuzitembelea skuli zile nimekuta changamoto nyingi nyingi na vilio, na kikubwa sana katika skuli ya Jang'ombe kuna kilio cha muda mrefu kuhusu suala lao la kutiliwa *fence* katika Skuli ya Sekondari ya Jang'ombe, waliahidiwa muda mwingi sana lakini imekuwa ndio nyimbo, tutafanya tukijaaliwa lakini mwisho wa siku hakuna ufafanuzi wowote. Kwa hivyo, mimi haraka haraka Mhe. Waziri, kikubwa hapo nitakamata kidogo mpaka nijue mustakabali wa skuli zangu zile zinafaidika vipi na ujengwaji wa *fence* yake ile.

Mhe. Naibu Spika, vile vile kuna skuli yangu ya Kidonge Chekundu, ni skuli ya zamani sana, nashukuru skuli ile wamepita watu wengi sana Zanzibar basi wamepita pale tokea enzi za *Hulmud School*, watu wengi sana, hata huyu Rais wa Zanzibar alipita pale Hulmud, kwa hiyo, inaonesha skuli ile jinsi gani ilivyokuwa pevu, lakini kwa kweli sasa hivi majengo yake au maeneo yake yamekuwa si ya kuridhisha.

Nashukuru tulipata msaada wa chumba cha *computer*, lakini ndio yale yale tunapeleka vifaa, lakini bila ya kuweka mazingira ya vile vifaa vilivyopelekwa.

Mhe. Naibu Spika, hivi karibuni tumekwenda kuangalia pale kweli kuna chumba cha *computer* lakini hakina hadhi za kukaa, zile *computer* baada ya muda mdogo tu *computer* zile zote zimekufa.

Kwa hiyo nafikiri Mhe. Waziri, uje utufafanulie katika hilo, tusije tukaja tukapeleka ule mradi pale lakini hatukuangalia mazingira ya kuzisaidia zile

computer ziishi kwa muda mrefu katika maeneo yale pale, na hiyo ni kwa skuli zangu, nafikiri kila mmoja atasema kwa upande wake.

Mhe. Naibu Spika, vile vile jengine ninalotaka kuzungumzia tumepata malalamiko katika skuli ile. Kuna walimu wangu wengi sana, wamesimamia mitihani ya *Form II* hawajalipwa malipo yao, na kesho kutwa wakisimamia tena mwaka mzima umetimia hawajalipwa malipo yao, na hilo Mhe. Waziri atakapokuja naomba aniambie kulikoni, muda umekuwa mwingi, na wale walimu wanafanya kazi nzuri sana, kazi ya kutufanya sisi sote mpaka leo tumekuwa viongozi tumepitia kwenye mikono ya walimu, lakini kama walimu kidogo hatuwapi ile thamani iliyokuwa kubwa zaidi, ndio maana msanii mmoja akafika kutunga nyimbo *hajaona milele chumvi pongezi kupewa*, ile chumvi ni mwalimu, kwa hiyo huwezi kuwa popote bila ya kupita katika mikono ya mwalimu.

Sasa tuangalie mazingira ya walimu wetu walivyo sasa, walimu nathubutu kusema kama nitasema lugha mbaya nisemeheke, thamani yao iko ndogo lakini wanafanya kazi kubwa sana na kazi nzuri sana, lakini Mwenyezi Mungu *in shaa Allah* atawalipa kwa kile ambacho chema walichokuwa wakitufanyia, kwa sababu sisi sote tumepita mikononi mwao, na mpaka leo hii tumepata ujabari na ujeuri kusimama kwenye chombo kama hichi kupitia kwenye mkono wa mwalimu, lakini ukimuona mwalimu mazingira yake utatamani kulia.

Mhe. Naibu Spika, vile vile nitazungumzia juu ya suala zima la mtaala wetu wa elimu. Wengi waliopita wamezungumza lakini na mimi nitarudia vile vile kuzungumza, kwa sababu nilikuwa nayo tokea mwanzo, lakini kwa sababu nimekuja mwisho mwisho imekuwa yale mambo mengi yamezungumzwa.

Mhe. Naibu Spika, mtaala wetu wa elimu uangaliwe upya Mhe. Naibu Spika, kwa sababu imekuwa ni kilio cha muda mrefu sana, kusema kwamba wanafunzi wetu mbeleni hawafiki vizuri kwa sababu wanatoka, mfano mdogo tu kuna wanafunzi waliofanya mtihani 1957 wa kitado cha pili, lakini waliofaulu pale ni 573 umeona; kwa sababu gani mtaala wetu uko mgumu, tunasomesha Kiswahili kuanzia *standard one* mpaka darasa la sita au la saba baadaye tuna-*change* tunakwenda kwenye Kiingereza, kuwahamisha pale tunawapa wakati mgumu, na ndio maana wanafunzi wengi sana wanashindwa ku-*cope* na masomo yale kwa sababu ya kufundishwa kwa Kiingereza.

Mhe. Naibu Spika, kwa hiyo ningeomba tu Serikali hii pengine kupitia Wizara ibadilishe muundo, tuanze kusomesha Kiingereza tokea mwanzo, kwa sababu watu wengi sana humu kwa ukweli usiofichika miongoni mwetu. Sote humu

watoto wetu wote sisi wanasoma *private school,* na tunaziacha skuli zetu za Serikali kwa sababu unaweza kuona kwamba pengine ufundishaji wao hauko mzuri au mtaala hauko vizuri, tunawapeleka kule kwamba tuna imani kwamba wanatoa elimu bora na ndio imani yetu.

Ukipiga hesabu katika japo skuli za *private* zitakuwa kidogo lakini zinafaulisha watoto wengi zaidi kuliko skuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kutokana na mtaala, kwa sababu wale kule tokea darasa la kwanza wanaanza kusoma kwa Kiingereza mpaka wanapoendelea, kwa hiyo inakuwa haiwapi shida mabadiliko yale kutoka *standard six* na *seven* kuingia *form one* na *form two,* kwa sababu ni lugha ile ile hawapati tabu, lakini hawa huku wanapata shida baada ya kutoka kwenye Kiswahili, Kiswahili kwenda pale inaingia Kiingereza kidogo inakuwa vigumu na ndio tunapoteza wanafunzi.

Mhe. Naibu Spika, ukiangalia wanafunzi wanaotoka *primary* kuingia *secondary* utawakuta wengi, lakini watoto wale baada ya miaka miwili wanafanya mtihani, *Form Four* wengi sana wanabakia pale hawawezi kuendelea mbele kwa sababu ya lugha, kwa hiyo ningeomba Mhe. Waziri hili suala uliangalie kwa umakini, ikiwezekana tubadilishe mtaala wetu angalau uendane sawa sawa na skuli za *private*.

Mhe. Naibu Spika, vile vile nitapenda kuzungumzia juu ya suala zima la mitihani. Nabaki pale pale kwamba mitihani yetu tunapofika *Form Four*, Baraza la Mitihani la Taifa linafanya mtihani, lakini sidhani kama tuna-*cope* na zile *syllabus* nzima ambazo wanazosomesha wenzetu upande wa pili. Kwa sababu wale kule wanafaulu vizuri sana kuliko Zanzibar, kulikoni! Nitaomba Mhe. Waziri atakapokuja anijibu hili swali, kwa sababu gani mtihani mwanafunzi atakayefanya *Form Form* wa Zanzibar na *Form Four* atakayefanya Dar basi wengi sana wanafaulu kwa Tanganyika au kule Tanzania Bara kuliko Tanzania Visiwani, na hii inaonesha kwamba zile *syllabus* haziendi sambamba, hayo ni mawazo yangu lakini kama si hivyo ningemuomba Mhe.Waziri atakapokuja naomba anisaidie.

Mhe. Naibu Spika, jengine ninalotaka kuzungumzia ni Bodi ya Mikopo, limeshazungumziwa na wengi sana waliopita kwa sababu ni kadhia kubwa ambayo inatukabili.

Kwanza niipongeze Bodi ya Mikopo ya Taifa ya Tanzania, kwa sababu imeweza kutusaidia kwa moja au jengine, kutusomeshea karibu wanafunzi 3100 kwa Zanzibar ambao wamepata mkopo kupitia Bodi ya Mikopo ya Taifa, lakini Bodi ya Mikopo ya Zanzibar imekuwa kilio au jipu kwa muda mrefu

sana, wanafunzi wetu waliopo nje ya nchi wanasoma wanapata shida sana, pesa za kujikimu hawapatiwi, pesa za kufanyia utafiti hawapatiwi, ukiangalia wako nje ya familia zao, ni matatizo tunawasababishia, ijapokuwa huyu Mjumbe aliyepita aliwaonea huruma sana watoto wao wa kike, lakini hata wanaume wanapelekea kuharibika katika suala hilo, kwa sababu wote ni binadamu na wote wana mahitaji sawa sawa.

Mhe. Naibu Spika, watoto wanacheleweshewa sana kupata hivi sasa hivi, kuna karibuni mwaka mmoja na miezi sita wanafunzi walikuwepo China hawajalipwa fedha zao za kujikimu, je, unategemea wale watu wataishi vipi kule, hawana baba, hawana mama. Na kama Mjumbe aliyepita alisema kwamba kama masomo yale ambayo yanapatikana kule basi wasipelekwe wasomeshwe katika vyuo vyetu vya hapa kupunguza mzigo kwa Serikali, kwa sababu mzigo umekuwa mkubwa na hatuwatimizii, lakini katika mikataba yao imo, lakini kutokana na pengine na hali ya Serikali yetu inasema kwamba hatuwezi kuwakimu, ni tatizo. Kwa kweli tunawapa matatizo makubwa sana, kufika wengine mpaka wanafanya kazi za *day worker* kuweza kujikimu angalau siku ziende, masomo yamalize waendelee, nafikiri hatuwatendei haki, katika hicho Mhe. Waziri uwe makini sana na bodi yako ya mikopo, namna gani wale watu tunawafanyia ili pesa zao za utafiti na pesa za kujikimu wanapata ndani ya muda.

Leo hii wewe iwe wiki mbili tu hujapata pesa kilio chako unakijua mwenyewe, leo hii mwanafunzi kule hana baba hana mama atamlilia nani. Basi nafikiri na hilo Mheshimiwa lazima uliangalie.

Mhe. Naibu Spika, vile vile Bodi ya Mikopo ya Zanzibar iliingiziwa karibu bilioni nane nukta mbili (8.2 bilioni), lakini hali halisi walichopata ni bilioni tatu pointi sita (3.6), fedha hizi ambazo zimetiwa kwa wanafunzi 575, lakini kuna wanafunzi wengi walikuwa wanahitaji haya masuala ya mikopo nafikiri kiwango kimekuwa kidogo sana, na wakati kama tunataka tuendelee kwa kweli, kwa sababu tunahitaji elimu, kwa hiyo hizi fedha ambazo zinazoahidiwa katika Wizara ya Fedha kupitia Bodi ya Mikopo basi waingiziwe Mhe.Naibu Spika, *at least* waweze kujitanua nao yale mahitaji wanayohitaji kwa wanafunzi yaweze kupatikana. Hiyo ndiyo itakuwa njia pekee kutukwamua hapa tulipo, na vilio hivi vya kulia kila *time* kwamba kukosa pesa za kujikimu, fedha za mitaala zitakuwa zimeondoka.

Mhe. Naibu Spika, vile vile nizungumzie juu ya suala la majengo. Tunashukuru kwamba tunapata misaada katika ujenzi wa skuli za Wilaya lakini hizo skuli naona sasa hivi zinakuwa tatizo. Mwenzangu Mjumbe aliyepita

alisema kwamba zimejengwa juzi tu lakini hazina viwango, sasa hatutambui kama *engineer* siye aliyetumika, au ndiyo hiyo habari ya watu unapoambiwa upeleke mifuko kumi unapeleka miwili, ukizitembelea zile skuli sasa hivi Mhe. Naibu Spika, unaweza kulia jinsi ukiziona asilimia nyingi sana skuli zile zimepasuka, sina nyufa za kutisha, skuli hata haijafika miaka minne mitano, kwa hiyo sitegemei kama kule wanafanya upembuzi yakinifu yakini hasa kwamba kujenga zile skuli *at least* ziwe za muda mrefu, skuli ile inapitwa na skuli ya Kidonge Chekundu iliyojengwa tokea siku nyingi, japo skuli ya chini lakini nyufa kwanza zipo kwake zipo kidogo kuliko skuli ambayo imejengwa juzi tu miaka miwili au miaka mitatu.

Mhe. Naibu Spika, na vile vile katika kilio hichi mara nyingi sana tunatumia majengo ya skuli katika kuwahifadhi watu waliopata majanga, sawa hatuna pa kuwaweka lakini tunawanyima nafasi watoto wetu kuendelea na masomo. Kwa hiyo ningeomba Serikali pindi linapotokea janga ghafla imetokea tu labda *time* yoyote tutafute njia mbadala hawa watu waliopatwa na majanga wahifadhiwe, na watoto wapate fursa ya kuendelea na masomo; kipindi kilichopita watoto walikaa karibu mwezi mzima hawaendi skuli, kwa sababu skuli ile ina watu wa majanga.

Mhe. Naibu Spika, nilitembelea mimi Skuli ya Mwanakwerekwe "C", na baada ya kumaliza majanga nilikwenda kutembelea pale kwa kweli inasikitisha hali iliyokuwepo pale, madeksi yake yamevurugwa vurugwa, uchafu yaani mpaka hausemeki, nilijaribu kufanya usafi na wenzangu nimekuta hali siyo nzuri katika skuli ile, kwa sababu imetumiliwa vyenginevyo si lengo la skuli, watu walikuwa wanakaa mle, wanaishi katika watu wa aina mbali mbali, kwa hiyo tumesafisha mle vile tulivyovikuta mle kwa kweli vinasababisha hata kuzungumza, tumeona mpaka mipira ya watu wazima, imeonekana mpaka katika vyumba vya kusalia, na pale skuli imeshafunguliwa kuna watoto, nafikiri linapotokezea janga kama hilo kwa kweli itafutwe njia mbadala, tusitegemee majengo ya skuli, japo tuna uhaba wa majengo basi tutafute sehemu ya dharura alau tutafute mahema, patafutwe uwanja, pajengwe mahema ya *temporary*, choo, ili watoto waendelee kusoma na wale kule wahifadhike, kama si hivyo tutazidi kuwadumaza watoto, kwa sababu itabidi tuwa-*keep busy* zaidi, kwa sababu unapomzuia mtoto mwezi mmoja kwa hiyo unamuweka nyuma ya *syllabus*, hawezi ku-*cover* pale, keshokutwa mtihani kwa hiyo itabidi unamu-*over doze* masomo kuja kufanya mtihani kuweza kufaulu, na hilo suala limetokezea. Sasa hivi katika skuli ya Kwerekwe "C" baadhi ya wanafunzi sasa hivi pengine muda wa kucheza hapana, ni kusoma tu kwenda mbele, kwa sababu wanakabiliwa na mitihani baada ya mwezi mmoja mzima kuwa nje ya skuli.

Mhe. Naibu Spika, hii ilitokana na azma moja ya kuwasaidia watu wetu ambao walifikwa na maafa katika sehemu mbali mbali, kwa hiyo wazo la Serikali ni zuri kuwasaidia watu wake, lakini na wao wanafunzi tuwape haki yao, inapotokezea tatizo kama hili ningeomba sana Mhe. Waziri utafute njia mbadala, watu wahifadhiwe lakini na wanafunzi wapate fursa ya kutumia nafasi yao ya kusoma, vyenginevyo itakuwa tunakuja hapa tunapiga kelele watoto wanafeli hatujui namna gani tulipokosea, kumbe vile umekosea kuondosha wanafunzi zaidi ya mwezi mmoja, watoto wenyewe leo hii wanasoma skuli na hali kama hiyo, leo hii mwezi mzima unapowaweka nje itakuwaje.

Mhe. Naibu Spika, vile vile...

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa umebakiza dakika nne.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante Mheshimiwa. Vile vile nizungumzie masuala ambayo mengine yamezungumzwa na mimi napenda kukazia tu juu ya suala zima la nauli au maposho ya walimu wanaokaa sehemu za mbali, masuala mazima ya usafiri.

Kwa kweli nathubutu kusema narudia tena pale pale kwamba mwalimu ni mtu muhimu sana, lakini thamani yetu kwao imekuwa ni ndogo, kwa hiyo tunashindwa kuwasaidia na tukawapa kipaumbele muhimu sana, *at least* na wao wakajisikia kwa kweli skuli na furaha. Walimu wanakaa sehemu mbali mbali wanasomesha skuli sehemu mbali, utakuta mwalimu anakaa Fuoni anasomesha skuli ya Kombeni, angalia masafa kutoka Kombeni mpaka anakofanya kazi apande gari mbili afike katika skuli ile.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli lazima Wizara yako Mhe. Waziri, iwe makini sana katika suala kama hilo, ikiwezekana iondoshe uhamisho wa namna hiyo, kila mwalimu wamuweke karibu na eneo lake ili kumpunguzia ugumu wa maisha na ugumu wa kutumia nauli, ambazo nauli zenyewe ukizipiga thamani pengine mtu anatumia zaidi ya alfu ishirini, thalathini kwa mwezi, wakati yeye katika mshahara wake unazidi kuchelewa kupata nauli yake.

Mhe. Naibu Spika, kwa hiyo kama ulivyosema nisiendelee sana muda sio rafiki, mimi nachangia hayo, na sitounga mkono hoja moja kwa moja, nitaunga kwa asilimia kama tisini na nane, na mbili nitasubiri Mhe. Waziri, atakapokuja kunijibu vizuri juu ya mustakabali mzima mambo yangu niliyoyazungumza basi nathubutu kumuunga mkono, baada ya hapo naomba kuwasilisha.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mheshimiwa, nakushukuru sana. Sasa mchangiaji wetu anayefuata ni Mhe.Mohammed Said Mohammed (Dimwa) na baada ya hapo ni Mhe. Simai Mohamed Simai.

Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa): Mhe. Naibu Spika, nikushkuru sana kwa imani yako kwangu, lakini vile vile nimpongeze sana Mhe. Waziri, amewasilisha hoja yake vizuri sana, kwa sababu namjua yeye ni mtaalamu wa Kiswahili.

Vile vile nimpongeze Naibu Waziri, lakini kupitia kwao nimpongeze sana Katibu Mkuu, Wakurugenzi pamoja na watendaji wote waliotayarisha hotuba hii nzuri kuisoma na kuiwasilisha hapa katika Baraza lako Tukufu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mimi umenipa dakika chache, lakini nataka nizitumie hizo hizo kwa sababu nataka niseme tayari nimeshampelekea Mhe. Waziri baadhi ya mchango wangu kwa maandishi na kutaka ufafanuzi baadhi ya vifungu katika hotuba yake hii ambayo ameisoma hapa.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa niende kwenye Skuli ya Mpendae. Nataka nichukue fursa hii ndani ya moyo wangu kuipongeza sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo imetekeleza Ilani yake ya Chama cha Mapinduzi kwa vitendo kwa kujenga skuli ya ghorofa katika jimbo la Mpendae.

Tuipongeze kwa sababu mbili, sababu moja imetekeleza Ilani yake, lakini sababu ya pili ni kuwatendea haki wananchi wa Jimbo la Mpendae. Jimbo la Mpendae tulikuwa yatima hatuna hata skuli, ingawaje sasa baada ya mgawanyiko wa kishehia tumepata ile skuli ya Migombani.

Skuli ya Mpendae ni skuli nzuri sana lakini ina matatizo madogo madogo ambayo yapo, ningeomba sana wizara iangalie kwa upeo huu ambao nitautaja.

Skuli ile haina uzio, na muda umekuwa mkubwa sasa tayari ninahofia isije ikaanza kuchafuka au wakapita watu wasio na nia njema kabisa ya kuweza kuiharibu skuli ile. Hivyo, tunaiomba wizara iweze kuliona suala hili kwa umakini zaidi, kutujengea uzio huu na sisi viongozi wa pale tuko tayari kushirikiana nao ili kuona tunadumisha mazingira mazuri yaliyoko pale.

Mhe. Naibu Spika, ile skuli ni ya mchepuo wa sayansi, na wakati mwengine watoto wengine wanaokaa mbali wanataka kusoma pale wanakodi nyumba za

jirani, lakini wengine wanakodi sehemu mbali mbali. Sasa tungeomba sana pana kiwanja pale ambacho tumewatengea skuli hii kiweze basi kuonewa jicho la huruma kwa wanafunzi wale angalau hali ikiruhusu waweze kuja kujengewa na tuone mambo yanakwenda sawa.

Mhe. Naibu Spika, nataka nirudi kwenye skuli ya Migombani. Skuli hii tuipongeze sana serikali kwa sababu viongozi wengi wametoka pale waliopo sasa hivi madarakani, lakini skuli ile imekosa haiba kabisa, skuli ni chakavu sana, na nimuombe Mhe. Waziri kupitia hapa tukimaliza bajeti tu hii tukafanye ziara ya pamoja mimi na yeye, ili tuone sehemu gani itakuwa ina uchakavu, wao watachangia nini na sisi tuweze kuchangia kupitia katika Mfuko wa Jimbo.

Vile vile niipongeze sana serikali kwa skuli ya Migombani kuanzisha elimu ya awali, imeanzishwa kwa nia njema sana lakini cha kusikitisha zaidi kuwa watoto wale hawana hata vikalio.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf amesema hapa angalau wapelekewe yale mabusati waweze kukaa kwa hatua ya mwanzo tuone, ikiwa hatukuwapelekea chochote na mashimo makubwa yaliyokuweko pale ni aibu kubwa sana kwa skuli ile. Skuli ile ina matatizo mengi, kisima kina matatizo, vyoo vina matatizo, lakini tunajaribu kwa kadri ya uwezo wetu viongozi kusaidia pale lakini na wizara ituunge mkono kwa hali ya juu kabisa.

Mhe. Naibu Spika, niingie katika Vyuo Vikuu. Kwanza niipongeze sana serikali kwa kuanzisha Chuo Kikuu cha *SUZA*, lakini kwa jitihada zake kubwa za kuongeza vyuo vikuu hapa Zanzibar, kwa sababu vijana wetu wengi watasoma hapa kuliko kwenda nje. Lakini tuipongeze sana *SUZA*, tumpongeze sana Profesa Idrissa Ahmada Rai, yeye ni *Vice Chancellor* pale, jitihada zake kubwa ambazo anajitahidi kukiendeleza chuo kile.

Mhe. Naibu Spika, wewe unajua jitihada zinazofanyika pale ni kubwa sana, sasa hatupaswi kuwavunja moyo wataalamu wetu tuwaunge moyo, wakati mwingi tuwape nafasi ili wafanye kazi zao.
Mhe. Naibu Spika, nataka kwenda kwenye udahili ambapo wanafunzi wengi wanafanyiwa. Wanafunzi wengi wanafanyiwa udahili kwa njia ya *Central Admission System (CAS)*, lakini nadhani kuna vyuo hapa Zanzibar haviendi na *system* ile, kwa sababu gani mimi sijui. Tunataka tuangalie wale watoto au wanafunzi tunaowadahili, je, wana viwango husika? Tusije tukawadahili watu wakawa hawana viwango husika na kupelekea elimu ikawa bora elimu tu sio elimu bora.

Mhe. Naibu Spika, kuna vyuo vingi sasa vya amali au vinaitwa *professional studies*, vimeanza kujitokeza vingi Zanzibar. Mimi ningeiomba wizara iwe na utaratibu wa kuvipitia vyuo hivyo, je, vinatoa elimu bora au bora elimu. Kwa sababu ni vingi na vimekuwa vingi zaidi.

Mhe. Naibu Spika, nije haraka kwenye Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Wenzangu wamezungumza na mimi nitazungumza kidogo, lakini mimi nitazungumza kwa aina yake.

Mhe. Naibu Spika, tumpongeze sana Mkurugenzi wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, lakini tuwapongeze sana Wajumbe wa Bodi pamoja na Mwenyekiti wa bodi hiyo. Mimi niipongeze sana na Bodi ya Mikopo ya Vyuo Vikuu ya Tanzania Bara, kwa sababu wamefanya kazi kubwa katika miaka midogo sana.

Mhe. Naibu Spika, Mkurugenzi huyu anafanya kazi kubwa sana lakini nataka kusema tumempa jiko hatumpelekei chakula atafanya nini? Tungeomba serikali imsaidie sana katika kutunisha Mfuko wake ili aweze kuwapelekea wanafunzi kule waliko. Nataka niwaambie *mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni*, anafanya kazi kubwa, na mpaka anatoka mvi za kichwa cha kufanya hana. Mimi namhurumia sana, lakini nimwambie tu aendelee kushika hapo hapo ndio kazi za utumishi wa umma zinavyokuwa.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kabisa wanafunzi wengi wanakosa kupelekewa pesa za kujikimu au zile za tafiti kwa wakati. Sasa hii inapelekea wanafunzi wetu kuwa katika hali mbaya. Mheshimiwa hata kwangu wanakuja wale wa jimbo langu, na hii sisemi tu kwa jimbo langu hata na kwa Wawakilishi wa majimbo mengine, ukiona watu wazima wanalia ujue kuna jambo hapo.

Sasa nataka niseme kwamba serikali ifanye haraka sana kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kuona basi inawapa pesa za kujikimu wanafunzi wale waliokuwa nje ya Zanzibar, lakini hata hawa walioko Zanzibar, kwa sababu wakati mwengine pesa za wazee zinakuwa ni ndogo sana hawawezi kujikimu.

Mhe. Naibu Spika, usajili wa elimu nije kwenye Elimu ya Sekondari. Tuipongeze sana serikali katika miaka sita iliyopita kuanzia 2010 mpaka sasa tumeona skuli nyingi sana za ghorofa zimejengwa, na hilo ni jambo zuri la kupendeza sana katika serikali yetu. Lakini jambo la msingi kuangalia nako kuna Skuli ya Kibuteni, baadhi ya wenzangu wameigusia skuli ile ina muda mwingi sana, nataka Mhe. Waziri atapokuja hili aniambie wakandarasi wangapi tangu kuanza wamepewa pale, vile vile mpaka sasa anaendelea mkandarasi gani na kiasi gani serikali imekula hasara kutokana na suala lile.

Mhe. Naibu Spika, nirudi tena kwenye sera yetu ya elimu. Niseme sera yetu hii tumegundua ina mapungufu mengi sana, tuiombe wizara basi ikae na wataalamu iweze kuona mapungufu gani yanaweza kujitokeza. Mheshimiwa sio dhambi kuiga mambo mazuri, mwalimu wangu Maalim Haroun Ali Suleiman Mhe. Waziri anapokwama aende akachote maarifa makubwa, kile ni kisima kisichokuwa na mwisho, anaweza kumuongoza akaweza kufanya kazi zake kwa umakini zaidi, amefanya mambo mengi na kila wizara niliwahi kusema hapa wakati nikichangia hotuba yake, kila wizara aliyopewa Maalim Haroun amefanya mafanikio makubwa sana. Kwa hivyo, tusione tabu kwenda kuchukua ushauri kwake kwa sababu ni mtu ambaye ana *experience* kubwa sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa niseme hayo lakini mengi nimempelekea Mhe. Waziri ya kutaka ufafanuzi kwenye baadhi ya vifungu. Lakini nataka kusema siungi mkono hoja hii mpaka nipate ufafanuzi wangu katika vifungu ambavyo nimevitoa pamoja na haya ambayo nimeeleza. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa wema wako. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe mchangiaji wetu wa mwisho ni Mhe. Simai Mohamed Said. Nawaomba tena wale ambao walikuwa wana nia ya kuchangia ambao majina yao sijayataja basi wapeleke kwa maandishi, tayari kama mtu anahitaji kupiga buti au kumuuliza basi atakuwa na nafasi akipeleka kwa maandishi, na jina lake likiwepo ndani ya *list* yangu kwa wale ambao hawajachangia.

Baada ya hapo nitawapa pia nafasi Waheshimiwa Mawaziri na nitaanza na Mhe. Ali Abeid Amani Karume ambaye yeye ni Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, baada ya hapo Mhe. Said Soud Said, Waziri asiye na Wizara Maalum; Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto; Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango na nimeona mkono wa Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Waheshimiwa Mawaziri nimeona wengi wenu mtachangia lakini nilikuwa naomba mtumie muda mdogo sana ili kuhakikisha kwamba tunamaliza kwa wakati. Nawaomba kwa hilo, najua mna wajibu wa kujibu hoja ambazo zinawagusa moja kwa moja, lakini ningeomba basi kuangalia na wakati wenyewe. Kwa hiyo, Mhe. Simai Mohamed Simai unaweza kuanza mchango wako.

Mhe. Simai Mohamed Said: Mhe. Naibu Spika, ahsante na mimi nikumbushie kwamba jina langu ni Simai Mohamed Said sijui kwa nini unapenda kuniita Simai Mohamed Simai. Mimi naitwa Simai Mohamed Said.

Mhe. Naibu Spika: Endelea Mheshimiwa mimi nakujua kama wewe Simai Mohamed Said, endelea, ulimi unateleza.

Mhe. Simai Mohamed Said: Baada ya hapo na mimi ningetoa shukurani zangu na kumpongeza kabisa Mhe. Waziri kwa hotuba yake nzuri kabisa aliyoitoa, naamini na yeye pia ataweza kufanya mambo mazuri kama ambavyo ameweza kufanya Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora alipokuwa akiongoza wizara hii. Tukisema vijana wanaweza basi Mhe. Waziri ni kijana mwenzetu pamoja na Naibu Waziri wake basi naamini wataweza.

Baada ya kumpongeza vyote niseme tu kwamba baada ya maelezo yangu nathibitisha kwamba mimi nitakuwa siungi mkono hoja mpaka nitakapopata taarifa zangu ninazozitaka.

Kwanza ningependa kufahamu kwenye ukurasa wa 123 wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi nambari 5 kinachosema kwamba: "Kituo cha kulelea wajasiriamali kimeanzishwa, kituo hicho ni cha kwanza na cha aina yake katika ukanda wa Afrika Mashariki na kinatoa mafunzo katika fani za uchumi, TEHAMA, Utalii na Usindikaji wa Mazao ya Biashara". Ningependa kufahamu hiki kituo kipi kinazungumzwa.

Pia ningependa nipate majibu kwenye ukurasa wa 91 wa Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa Wizara za Zanzibar mwaka 2013/2014, lakini na hii inayozungumza kwamba kuna shilingi 89,043,805 zimelipwa kwa ajili ya matumizi ya ukaguzi na vielelezo vyake havikupatikana katika ukaguzi huo. Kwa hiyo, ningependa kufahamu ni vielelezo gani lakini havikuwepo.

Vile vile kwenye ukurasa wa 92 katika Ripoti ya Wizara ya Elimu imefanya malipo ya jumla ya shilingi 22,556,000 kwa Kampuni ya *Fasima General Traders.* Lakini pia kwa ajili ya vifaa vya ujenzi vya skuli ya Chumbuni lakini barua ya malalamiko ya madai kutoka Kampuni ya *Fasima General Traders* inaonesha kwamba shilingi 15 milioni tu. Hivyo, ukaguzi umeshindwa kupata maelezo juu ya ufafanuzi wa shilingi 6,956,000. Ningependa kufahamu hilo suala.

Mhe. Naibu Spika, nianze kuzungumza kwamba suala la elimu hasa kwa upande wa Mkoa wa Kusini na jimbo ninalotoka mimi la Tunguu lina mambo mengi sana. Nikianza kuzungumzia kutoka Kisiwa cha Uzi, nikija Unguja Ukuu Tindini, Kae Pwani pamoja na Kae Bona. Nikija Kikungwi, Bungi, Kibele na upande wa Jumbi, Tunguu, Bungi Mtakuja, Dunga Kiembeni, Dunga Bweni, Kinyongo na Gogoni pamoja na Mwera/Pongwe na Kiongoni na Ubago, jimbo lote hili kwa kweli lina changamoto nyingi sana kuanzia elimu, vitendea kazi na skuli zenyewe kwa ujumla.

Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri kama nitachukua muda kuzungumza kuhusu jimbo langu na maeneo yote anipatie njia ya upendeleo ili niweze kumuona yeye mwenyewe pamoja na mhusika wake aweze kunisaidia matatizo niliyokuwanayo kutokana na mazingira ya jimbo langu niliyokuwanayo. Kutoka visiwa, maeneo ya barabara yalivyo na maeneo kutokana na skuli zote. Kwa hiyo, ningeomba Mhe. Waziri anisaidie, na mengine nitakuja kueleza kwa kina kuhusu matatizo yangu ya walimu pamoja na skuli zote nilizonazo.

Mhe. Naibu Spika, nimejaribu kuangalia katika dunia na elimu zinavyokwenda, nikaangalia katika mtandao mwaka 1962 katika mkutano wa Antananarivo walifanya masuala ya elimu na kuhusu elimu ya Kusini mwa Jangwa la Sahara njia gani unatakiwa uende nazo.

Nikaangalia katika mkutano wa *World Bank* mwaka 1988 ambao walitaja maeneo manne. La kwanza ni *to improve quality*, pili *increase efficiency*, tatu *change output mix and increase participation in the financing by beneficiaries and the families*.

Sasa ningependa kufahamu ni mpango gani wa elimu ambao wizara yake inaufuata kwa upande wa Zanzibar katika malengo, sitaki kujua kwa sababu masuala ya *strategic plan*, nataka kufahamu ni mpango upi tunaokwendanao. Maana yake napata hofu kwamba unapotoka uwaziri inapokuja serikali nyengine mtu anakuja na mawazo mbadala anaondoka katika mpango mkuu ambao wizara inataka kutekeleza kwenda katika mpango mwengine kwa mawazo yake. Sasa nataka nielewe ni mpango upi pia unaofuatwa katika wizara yake.

Pia niseme mwaka 1960 Afrika tulikuwa tuna Vyuo Vikuu 18 katika nchi 48, lakini kwa kweli lazima niipongeze serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Serikali ya Zanzibar, ukiangalia leo tuna Chuo cha *SUZA* na vyuo vingi ambavyo vinaendelea. Hili jambo ni la kujipongeza, kwa hiyo naipongeza sana serikali.

Mhe. Naibu Spika, ningependa pia kufahamu suala moja muhimu, na kwa hili nitakuwa mkali kweli, ni suala la watoto wadogo wanavyopokea mimba wakati wako skuli. Hili ni tatizo, *teenage pregnancy*. Sasa nataka kufahamu katika hili suala la *child abuse* na hizi ambazo tunaziita *hidden crimes* zinafanyika kwa watoto wetu hasa wale katika umri kutoka miaka 13 mpaka 15 na 16, ni mpango gani wizara imejipanga katika *child policy*, katika kuwalinda watoto hawa mambo haya yanapotokezea, lakini pia ni hatua gani zinachukuliwa kwa ajili ya watoto. Kwa sababu hili tatizo limekuwa sugu, limezungumziwa pia na viongozi lakini lazima hapa panahitajika pafanyike maamuzi ya haraka ili kutokomeza tatizo hili.

Mhe. Naibu Spika, pia katika ukurasa wa 50 wa Hotuba ya Rais alipokuja kufungua Baraza la Wawakilishi hapa alizungumzia mambo mengi, lakini alizungumza katika masuala ghorofa kumi skuli zitajengwa; nataka kufahamu hizi skuli zenye mpango wa kujengwa ni maeneo gani.

Pia alizungumzia suala la kujenga Kituo cha Mafunzo ya Amali Makunduchi, Mkoa wa Kusini. Nataka kufahamu vigezo gani vilivyotumika kwa ajili ya hiki kituo kupelekwa Makunduchi na sio katika maeneo ya kati kati kwa Wilaya ya Kati ambapo kinaweza kuunganisha wananchi kutoka Paje, Makunduchi, Jambiani pamoja na Unguja Ukuu, Uzi, Kikungwi na maeneo yote.

Pia tukienda katika bajeti yake nimeona amekuwa anapata changamoto, na sio kidogo ni nyingi, namtakia kheri kama ataweza kuyafanya.

Mhe. Naibu Spika, nataka nizungumze suala la Chuo cha Karume, *Karume Institute of Science and Technology* ambacho kinaitwa *KIST*. Nimejaribu kuangalia ni vyuo gani ambavyo Tanzania au katika maeneo ya Afrika Mashariki tumefanana nao, lakini kuna chuo ambacho kipo kama hicho Kigali kinaitwa *Kigali Institute of Science and Technology*. Hiki kimeweza kufanya mambo mengi mazuri katika nchi yao na wameweza kujipanga.

Ningependa kumshauri Mhe. Waziri ajipange kwenda kutembelea hiki chuo ili tuweze kufanya mpango mkuu kukitoa hiki chuo chetu hapa kilipo. Kwa sababu moyo wote wa kuweza kuwasaidia Wazanzibari, kuwaunganisha na ajira za kuwa nje na pia kuanzisha ajira za kujitegemea zipo katika chuo hiki. Nimesema sana huko nyuma katika masuala ya *marine engineering, electrical engineering, mechanical engineering* na mambo mengi kabisa yanatokezea katika chuo cha Karume na lazima hizi mashine zao zibadilishwe.

Mhe. Naibu Spika, sasa nitapenda kufahamu kwa Mhe. Waziri katika mpango wowote anaojipanga katika wizara yake, katika hii miaka miwili au mitatu, chuo hiki atakitoaje hapa kilipo sasa hivi ili vijana wetu waweze kujitoa hapo.

Katika mchango wangu nilioutoa katika Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi na katika Wizara ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ nilizungumza suala la kutumia upande wa matrekta ambapo lile eneo liko chini yake Mhe. Waziri, kwamba atatumia njia gani ya kuweza kuunganisha matrekta, kujenga karakana ya kisasa, kuchukua vijana kutoka JKU pia kwenda kuwasomesha Chuo cha Karume alimradi tuweze kupata gereji ya kisasa pale ambayo itaweza kutoa ajira kwa vijana, kusaidia kutengeneza magari ya serikali ambapo mabilioni ya pesa tungeweza kuyaokoa. Pia kuwa mfano kwa ile gereji katika Afrika Mashariki ambapo wizara zetu zote zitafanya kazi kwa pamoja.

Vile vile nilitaka kuzungumzia katika suala zima la vijana wetu na nini hasa tunakosa hapa Zanzibar. Ukiangalia tunawasomesha vijana, changamoto kweli tunazo na nchi zote zipo changamoto katika elimu, kwa sababu tayari serikali inataka kuwasomesha wananchi wake aidha kwa njia ya kuwasaidia kwa kuchangia kwa ada ndogo au katika njia ya kulipia kabisa kuweza kuifanya elimu katika nchi husika. Lakini ukiangalia katika watoto, vijana wetu mwaka wa kwanza unakwenda mpaka mwaka wa saba unakuja katika *primary* mpaka *secondary*.

Unakuta kuna kitu tunakosa vijana wetu ni kitu gani? Watoto wetu hawana *confidence*, na hawana *confidence* kwa sababu *social study* pia imepunguzwa, ni michezo ambayo ya kufanywa. Lazima tutafute njia, unakuta mtu anapata *grade* nzuri kabisa lakini *confidence* ya kuzungumza imeondoka kabisa, ni sababu gani inayosababisha hii *confidence* kwa vijana wetu kuondoka na tutafanya vipi *confidence* ya vijana tuweze kuirudisha kama zamani.

Pia utumiaji fursa ya michezo ya kiutamaduni, michezo wa kuigiza lakini pia kutafuta njia ya watu ambao ni mashuhuri wenye uwezo...

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa umebakiwa na dakika tatu.

Mhe. Simai Mohamed Said (Mpaka basi): Mhe. Naibu Spika, utatumia njia gani kuwasaidia hawa vijana moja kwa moja kuweza kufikia malengo. Mtu anafika pahala anaomba kazi anaweza akaongea Kiiengereza na anajielewa anashinda, inakuwa ile *confidence* haipo na hili ni tatizo. Kwa sababu hata ajira zilizokuwepo ni chache, lakini wenzetu wanashindwa kuzipata.

Jana nilikuwa naangalia katika *BBC* nikaona China wanajenga uchumi wao kwa kutumia michezo, na inapofika 2020 wanategemea kupata dola bilioni mia nane kwenye *sports economy*. Sasa katika haya yote tunakwenda sisi na nchi tunataka kufanya mambo mengi lazima Mhe. Waziri atahitaji, najua ana kitengo chake keshaanzisha, lakini michezo lazima inyanyuliwe katika maskuli ili tuweze kushiriki na sisi kwenda nje.

Tuna *Olympic* mwaka huu lakini ni aibu kwamba hakuna mtu kutoka Zanzibar atakuwa anashiriki, lakini kwa upande wa Tanzania kutakuwa ni watoto watatu. Hili jambo ni la huzuni kabisa, tulikuwa tuna vijana hapa wanacheza *table tennis*, tulikuwa wanakimbia hapa, wengi tunajua hata Mhe. Rais wetu alikuwa ni mkimbiaji mzuri wa *marathon*, *cross country*.

Lakini leo hakuna haya yote, na ni kutokana na kwamba malezi watoto wetu wanakosa. Naomba Mhe. Naibu Spika atakapokuja Mhe. Waziri nipate haya maelezo ya kina mimi naunga mkono hoja asilimia 99.5.

Nitahitajri maelezo ya kina hasa jinsi watoto wanavyotolewa mimba katika maskuli yetu. Ahsante Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante nakushukuru sasa nianze kuwapa Waheshimiwa Mawaziri nafasi na wao ya kuweza kuchangia na kujibu hoja.

Mchangijai wetu wa mwanzo ni Mhe. Balozi Ali Abeid Karume na baadae atakuja Mhe. Said Soud Said.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii kuongea leo.

Kwanza kabisa nataka nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kufika hapa na afya nzuri, sote wazima, kuja kuchangia hotuba hii iliyotolewa na Waziri wetu wa Elimu na Mafunzo ya Amali.

Nataka kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kushinda katika uchaguzi ule wa tarehe 20/3/2016 na kumpata Rais wetu ambaye tuliyemtaka Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein.

Nataka pia nimshukuru Mhe. Rais wetu na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchukua muda kidogo kabla hajaunda Baraza la Mawaziri na tumeona faida yake ametupatia Balozi mwenzangu Balozi Seif Ali Iddi kurejea katika nafasi ya Makamu wa Pili wa Rais na katika wakati huo sikuwahi

kumfikiria mtu ambaye kweli angeweza kuiendeleza kazi hii, kuliko yeye ambaye ana uwezo huo na kapata uzoefu huo katika kipindi cha mwanzo kuanzia 2010 mpaka 2015. Imani yangu ni kwamba kama ni kepteni wetu wa timu hii atatuongoza na tutapata mafanikio ambayo tunayategemea.

Napenda pia kumshukuru Mhe. Waziri wa Elimu. Pia nimshukuru Rais kwa kututeulia kijana msomi, mtu anaweza kuchapa kazi vizuri. Kwa sababu katika wizara hii lazima tukubali kwamba wengi tunaowashughulikia kuwasomesha ni vijana. Sasa ukimuona kijana mwenzako pale na kafikia pale kwa kupitia elimu basi na wao pia watachangamka. Hilo napenda kumshukuru Mhe. Rais kwa uteuzi huo.

Mhe. Naibu Spika, pia nawashukuru watendaji wote wa wizara hii husika; Naibu Waziri na watendaji wengine wa wizara hii.

Mhe. Naibu Spika, leo sizungumzii kama ni Mwakilishi, leo napenda kuchangia kama ni Waziri katika Serikali na katika timu yetu hii ambayo tunataka kuwaletea wananchi wa Zanzibar maendeleo katika maeneo mbali mbali ukijumlisha pia maendeleo ya elimu.

Katika hilo nitarejea yale ambayo niliwahi kuyasema siku nilipochangia Wizara ya Habari, nikasema kwamba katika nchi zote duniani watu wanapokwenda katika harakati za siasa huwa wanakimbilia kwamba chama chao kishinde, kikishashinda wakiingia madarakani waweze kuja na sera nzuri za kuweza kuwaletea wananchi maendeleo.

Sera za elimu ni muhimu sana, na sisi lazima tushukuru kwamba tumeweza kushinda Chama cha Mapinduzi na tunaendelea na sera ya elimu kuwapatia wananchi wetu elimu nzuri hasa kwa kuanzia na vijana.

Tumeona katika historia, kwamba kuna kiongozi wa upinzani aliwahi kukamata nafasi kubwa sana nchi hii pamoja na wizara hiyo na akawa anajifanya mjanja sana wa kujaribu kutugawa katika nchi yetu kwenye hivi visiwa viwili muhimu.

Katugawa kielimu pale ambapo anatoa elimu kwa ubaguzi, nilikuwa na mpango wa kusema kwamba kama wanakwenda wanafunzi kumi nchi za nje kwenda kusoma basi nasema angalau wanne watoke kisiwa kimoja kule na wengine sita watoke kisiwa cha huku ambacho ni kikubwa zaidi.

Lakini ujanja wake ni kwamba alikuwa anakwenda kisiwa kile anatoa wanafunzi wanne na akija hapa Unguja anatoa wanafunzi sita watatu wanatoka

huko huko. Kwa hiyo, ukipiga hesabu mwisho utakuta waliokwenda huko ni saba kutoka kisiwa kimoja na watatu kutoka kisiwa chengine. Naamini wazi kwamba katika uongozi wa Dkt. Ali Mohamed Shein, na katika wizara hii ubaguzi wa aina hiyo au ubaguzi wa aina yoyote hautopewa nafasi. (*Makofi*)

Dunia hii huwa napenda kutoa mifano kwamba hatuko peke yetu, kuna visiwa tumezungukwa na bahari lakini pia tumezungukwa na nchi nyingi sana duniani. Tutafute mifano ya nchi nyengine, mfano mmoja ninaopenda kuutumia ni mfano wa Marekani.

Mimi mmojawapo nilibahatika kupata nafasi au fursa ya kusomea huku, nikasoma mambo mengi tu kuhusu historia yao. Wamarekani walitoa kipaumbele katika mambo ya elimu na ndio maana wakaweza kujenga uchumi wao umekuwa sasa hivi ni uchumi wa kwanza duniani.

Ukiwauliza nyinyi mumefikaje hapa, wanasema tulikuwa tunatoa kipaumbele kwenye mambo ya elimu, na kule Marekani watu wanalipia wenyewe. Sisi huku tangu Mapinduzi serikali inabeba mzigo huo, na napenda kumshukuru tena Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwamba kang'anga'nia sera ile ile ya Mzee Karume, kwamba wananchi wetu wapewe elimu ya bure. (*Makofi*)

Niliwahi kuzungumza naye faragha nikamchokoza kwa kuwa mimi ni mchumi, nikamwambia unajua mzigo wa elimu bure hatuuwezi tena huko tunakokwenda. Akanambia Balozi sisi tumesomeshwa na Serikali ya Mapinduzi, tumepewa elimu bure, kwa nini tuwanyime watoto wetu, tutaendelea na sera hiyo hiyo. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, leo katika kuchangia nilikuwa nataka nichangie kama nilivyochangia tulipokuwa tunazungumzia Wizara ya Habari ambayo pia inashughulikia mambo ya Utalii.

Nasema kwamba huko tunakokwenda Zanzibar itategemea mambo ya Utalii, na utalii pia lazima tukumbuke kama kuna mafunzo fulani yanatolewa ya kutusaidia katika utalii.

Napenda kushukuru kwamba hatua hizo zimechukukuliwa na naomba ziendelezwe, na katika mafunzo hayo ya Amali tutilie mkazo, na naamini tutatilia mkazo kwa miaka ijayo lugha za kigeni. Wanakuja watalii hapa wanatoka nchi mbali mbali, ni wajibu wetu kwamba tujifunze lugha za kigeni ili wakifika hapa na wao wakaribishwe na watu ambao wanajua hizo lugha za kigeni.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoahidi sitaongea sana kwa kuwa niko katika kumalizia, nataka nielezee tu kwamba masuala ya ajira kuna vijana wengi wanataka kupata ajira lakini ukiwauliza kiwango chenu cha elimu kinatosha kwenda kutafuta ajira wanakwambia ndio kinatosha.

Lakini ninachosema kwamba nataka wanisikie vijana wa nchi hii, kwamba elimu haina mwisho, na huko wanakokwenda kusoma afadhali waendelee kusoma mpaka wafikie vile viwango ambavyo vinahitajika, viwango ambavyo vitawawezesha kwamba wakienda kunako soko la ajira kule wanaajirika haraka sana.

Nataka kutoa mfano tu ambao nautoa mara nyingi kwamba alinijia mtu akanambia Balozi naomba kazi, nikamuuliza kazi gani, akanambia yoyote. Nikajua pale pale kwamba huyu hana elimu ya kutosha wala hana mafunzo ya kutosha, kwa sababu mtu aliyekuwa ana elimu ya kutosha na mafunzo ya kutosha hawezi kukwambia nipe kazi yoyote, atakuvutia kunako ujuzi wake na uzoefu wake, atakwambia mimi nimesomea kitu fulani naomba kazi katika eneo hilo.

Lazima vijana wetu wajifunze ili waweze kuajirika. Saa nyengine huwezi kumuajiri mtu haajiriki. Nilimwambia yule kijana unauona huu ufunguo wa nini, akajibu ufunguo wa gari, nikamwambia kesho Jumatatu asubuhi saa moja ufike hapa utakuwa dereva wangu akanambia bahati mbaya sijui kuendesha gari.

Kuendesha gari pia kunahitaji mafunzo, natoa mfano tena wa kule Marekani nendeni mkatembee kule mkimkuta daktari basi daktari wa kweli, hapewi leseni mpaka apate mafunzo yale ambayo yanastahili. Sisi kwetu hatutokuwa tafauti na hao wenzetu.

Mhe. Naibu Spika, nataka tu kuwaomba, maana yake hili ni ombi muhimu sana, nawaomba Wawakilishi wenzangu, maana yake mimi nimeanza hapa kama ni Mwakilishi namshukuru Mhe. Rais aliyeniteua kwanza kuwa ni Mwakilishi halafu ndio akaniteua kuwa ni Waziri. Nataka nikuombeni Wawakilishi wenzangu tuunge mkono bajeti hii.

Bajeti hii kama ina mapungufu yake ni kwamba hatukuwapa pesa za kutosha. Na hilo linaeleweka, kuna mambo mengi yanataka kufanywa, sungura wenyewe mdogo hakidhi. Lakini tutajitahidi kupeleka angalau bajeti ya sungura huko, lakini ukweli ni kwamba fedha hizi hazitoshi na ziko nchi

nyengine zinatumia fedha zaidi katika mambo ya elimu hata kuliko mambo ya ulinzi.

Kwa hiyo, kwa msingi huo nataka niwaombeni tu kwamba mtuunge mkono kwenye hili, na miaka ijayo katika huu mpango mpya tunaouzungumzia kwamba *Programme Based Budget,* ni kwamba tunaweka bajeti yetu mwaka huu mpaka mwakani tutaendelea mpaka tutakapokuja katika bajeti ya mwakani tutatoa *projection* mpaka ya mwaka 2020.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru tena kwa kunipa fursa hii, lakini nimalizie kabisa katika ombi langu kwamba mimi napenda kuwaomba wenzangu msije kudanganywa huko kwamba sisi *backbencher* lazima kwanza tuulize maswali mengi, lazima kwamba tuambiwe hili na lile huo ni wajibu. Serikali ni wajibu kujibu maswali yenu, lakini tukishamaliza yale majibu nakuombeni tena tuipitishe hii bajeti ili twende tukaendelee kuwasomesha vijana wetu, ili na wao wapate elimu, na wao katika maisha yao wapate kufikia malengo yao waliyojiwekea.

Jengo hili hatutobaki sisi maisha, miaka ijayo huko watakuja watu wengine. Tuhakikishe kwamba hao watakaokuja katika jengo kama hili waje hapa wakati wameshatayarishwa vizuri, wenye elimu nzuri kuja hapa kuchangia kwa nia ya kuhakikisha kwamba uchumi wetu unakuwa mkubwa na uchumi wetu utajengwa na watu waliokuwa wana utaalamu.

Mhe. Naibu Spika, namalizia hapo na nakushukuru sana, na naunga mkono bajeti hii mia kwa mia. Ahsanteni sana.

Mhe. Said Soud Said (Waziri asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi.

Awali ya yote napenda kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendeleza hoja hii ya kuwa elimu bure katika visiwa vya Unguja na Pemba. Hoja ambayo ilianzishwa na hayati Mzee Abeid Aman Karume na kuifanya tarehe 23 Septemba kila mwaka kuwa ni siku wa elimu bure katika visiwa vya Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, hakika hoja hii ya kuifanya elimu bure imetuwezesha Wazanzibari kupata nafasi ya kuweza kuelewa na kujifahamu kwamba sisi ndio tuliofanyiwa hayo Mapinduzi na tunatakiwa tujenge nchi yetu, na sisi tunatakiwa sasa tuwe viongozi wa kusimamia Mapinduzi na sasa tunatakiwa

sisi tuyapeleke maendeleo kwa wananchi hasa hiyo elimu iliyokusudiwa kuwa bure.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya Mapinduzi ya mwaka 1964 nchi hii ilikuwa hakuna elimu bure, na ilikuwa elimu inapatikana kwa matatizo makubwa na hususan kwa watu ambao walikuwa wakijiita *" ibnu kinanata, ibnu khuzaimata, ibnu mudrikata ibnu I-lyasa, wahuwa awwalu man ahda l-budna ilarihabil-haramiya"* . Hao ndio waliokuwa na uwezo wa kupata elimu, si watu wote waliobahatika kupata elimu.

Kwa maana hiyo elimu ilikuwa ni mtaji wa watu maalum, na ndio maana nchi hii ikawa imetawaliwa kwa miaka mingi lakini ikashindwa kupata lugha zaidi ya Kiswahili, walikuja waarabu hapa wakakaa zaidi ya miaka mia tatu lakini Kiarabu hakieleweki, wamekuja wazungu wamekaa zaidi ya miaka mia tano lakini Kizungu hakieleweki, ni kwa nini basi, kwa sababu elimu hawakutaka kuitoa kwa maslahi ya wazalendo wa nchi hii.

Kwa vile sasa lazima tujivune kwa Mapinduzi ya mwaka 1964 kuweza kupata elimu Wazanzibari, na matokeo yake ikawa tumezalisha mpaka maprofesa ndani ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, tutakapozungumza hoja hii na uzuri wake basi matokeo yake ndio haya yaliyotufikisha humu ndani, kwamba sasa tumekuwa wazalendo tulioweza kubuni na kufikia hatua, na kuwa Baraza letu la kutunga sheria kwa maslahi ya Wazanzibari. Pamoja na hayo nataka nichukue nafasi hii kuwaambia Wazanzibari kwamba hakuna uwezekano wa jimbo lolote linaloweza kujitolea kusema kwamba tunataka kuwalipa walimu mwisho wa mwezi, hakuna. Zaidi ya serikali hakuna uwezekano wa kuwalipa walimu hata kumi kwa skuli moja hawa ambao wamejitokeza kutoa elimu bure zaidi ni serikali.

Kwa hiyo, serikali yetu imesimama kidete kuendeleza elimu bure kwa wananchi wa Zanzibar bila ya kujali rangi, kabila, dini wala itikadi ya chama. Hili ni jambo la kupongezwa, hili ni jambo la kupigiwa mfano na kusema kwamba Mapinduzi Daima! (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, tukielewa umuhimu wa elimu lazima kutambua umuhimu wa watumishi.

Wawakilishi wa Zanzibar ndio sisi, tunao uwezo wa kuiangusha elimu au kuinyanyua elimu. Kwa sababu lengo la kuja humu ni kutunga sheria na

kusimamia maendeleo, miongoni mwa maendeleo haya yatakayopatikana kama hatuna elimu kwa vile kimsingi lazima wale Wawakilishi walioko katika majimbo wahakikishe kwamba elimu inayotolewa kwenye maskuli, kwenye majimbo yao inafanana na wakati tulionao hivi sasa. Haimaanishi kwamba Mwakilishi yuko pale haijui hata skuli yake kwamba pale kuna walimu wana shida, kuna walimu hawana vipando, kuna walimu wanalala na njaa, hajui yeye ni Mwakilishi tu wa kuwakilisha watu kwenye majimbo lakini skuli hazielewi.

Mhe. Naibu Spika, hakuna maendeleo yatakayopatikana katika dunia zaidi ya elimu, na hakuna kitu kitaweza kujitokeza kikapata ufumbuzi kama hakuna elimu. Kwa hiyo, kimsingi sasa sisi kama Wawakikishi tuna wajibu wa kuwasaidia walimu wetu katika maskuli tusiwalaumu tu tukasimama kwenda kuwalaumu tu walimu, lazima tuwasaidie walimu, hii ndio kazi ya serikali kama imeweza kuwasaidia Wazanzibari wote wapate elimu bila ya malipo, na sisi kama Wawakilishi tukawasaidie walimu wafanye kazi yao vizuri.

Mhe. Naibu Spika, masuala haya ya kuboresha elimu lazima yasimame na uzalendo. Wazanzibari tuwe na uzalendo wa nchi yetu. Tusiiseme serikali, tuwe wazalendo wa nchi yetu.

Wawakilishi sisi kama viongozi, tukaone matatizo katika maskuli yetu, tukaone shida za walimu, tuone shida za wanafunzi. Wanafunzi wana shida. Wazee wa nchi hii wengi hawana uwezo. Sisi kama viongozi tuwasaidie hawa watoto ambao wazee wao hawana uwezo ili waweze kupata elimu na kujenga nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, ndugu Wawakilishi bado tuna jukumu katika miaka mitano hii tuliyonayo, kuhakikisha kwamba elimu tunaisimamia na tunaiboresha katika mazingira yote, hasa tukiangalia mitaala. Mitaala lazima ielekeze na inaelekeza mitaala. Vijana wa nchi yetu wana wajibu wa kujua historia ya mapinduzi ya mwaka 1964. Siyo mtu anafikia umri wa kuwa miaka 18 mpaka anaoa hajui kama nchi hii ilikuwa ikitawaliwa nguvu na kwa mabavu. Lazima aelewe kwamba hii nchi ilipatikana mwaka 1964 kwa mapinduzi. Na hayo ndiyo yaliyomfanya yeye asome bure, hayo ndiyo yaliyomfanya yeye hata kama anasoma kwa pesa basi anasoma katika nchi iliyo na mapinduzi ya kumlinda yeye kuishi vizuri. (*Makofi*)

Kwa misingi hiyo mitaala itaelekeza kuwepo kwa suala zima la vijana kusomeshwa historia ya nchi yao. Mitaala itaelekeza kuwepo kwa utamaduni wa visiwa hivi. Hivyo nataka niseme kwamba, kila kitu kitakuwa kipo katika mstari kulingana na Waziri wa Elimu tuliye naye, ni mzalendo, Naibu Waziri

wake ni mzalendo. Tuna imani kabisa kwamba watafanya kazi ya kuiboresha elimu na kuirudisha Zanzibar pale ilipokuwa ikitajwa kwamba ina elimu. Elimu haijaporomoka, tuliopomoroka ni sisi. Tukijikaza tukasimama kwenye mstari elimu itapanda pale pale juu. (*Makofi*)

Kwa misingi hiyo ni wajibu wetu kusema tutoe kila *efforts* kwa serikali ili isimamie wajibu wake katika mazingira haya. Na sisi Wawakilishi tujihakikishe kwamba tunatoa nguvu zote kwa walimu na wazee waliokuwa hawana uwezo katika mazingira ya kuifanya elimu iboreshwe katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba.

Na nikizungumza suala la mitaala Waheshimiwa Wawakilishi lazima linawagusa mpaka wazee, haimaanishi walimu wapanga kusherehekea elimu bila ya malipo watoto wanaitwa pale waende wakacheze ngoma, wafundishwe utamaduni wa nchi hii, halafu wazee waseme aah! mwanangu mimi sebu, hiyo hatutaki. Tutakwita sisi kama serikali tukuhoji kwa nini hutaki mtoto wako aimarishe utamaduni wa visiwa hivi. Lazima ashiriki kikamilifu, nchi hii haibagui mtu dini, kabila wala rangi ya mtu. Nchi hii ni nchi ya Wazanzibari, na lazima vijana wasimame na misingi ya kizanzibari. (*Makofi*)

Mheshimiwa kwa sababu ni mambo mengi lakini naamini nimefahamika. Napenda tu niseme kwamba naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia, na ninawaomba Wawakishi wote tuipitishe hoja hii ili Wizara yetu ya Elimu ikafanye kazi yake vizuri na maendeleo ya nchi yetu yaweze kupatikana.

Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana ninakushukuru. Nimkaribishe basi Mhe. Mouldine Cyrus Castico na ajitayarishe Mhe. Rashid Ali Juma na baada ya hapo ni Mhe. Dkt. Khalid Salum na mwisho ni Mhe. Haroun Ali Suleiman.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, kwa heshima na taadhima naomba nichukue nafasi hii kwanza kuwashukuru wote viongozi, na kwamba wizara zote zilizopitishwa ni kwa busara za Wawakilishi waliopo, kuhakikisha kwamba walioletwa mezani kwa ajili ya faida ya maendeleo ya nchi yetu.

Pia naendelea kumpongeza Mhe. Rais wetu pamoja na Makamu wa Rais ambaye anamsaidia katika masuala ya ushauri kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

Pongezi ni nyingi na wala hazitokwisha. Kwa hivyo niendelee kusema tu kwamba napenda nitoe shukurani kwa wale wote ambao wameweza kuchangia kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kwa sababu kwa michango yenu ndiyo kuboreshwa kwa wizara itakapofanyika. Na kwamba kila mmoja aliyechangia amechangia makusudi kwa mfano sehemu kama ni mzazi na mlezi wa nchi hii.

Mimi nisingependa kusema mengi kwa sababu na mimi ninayo yangu ambayo yanaingiliana sana na masuala ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Naibu Spika, kitu ambacho ninachotaka kusema hapa, ninataka kusema kwamba kuna lile ambalo linasema watoto wanaanza wakiwa ni wadogo, wanatolewa katika majumbani kwenda kuanza kupewa ajira ili waweze kusaidia wazazi kwa ajili ya kuongeza pato la chakula kwa siku. Ni suala ambalo linagusa nchi nyingi duniani. Ni suala ambalo linakatisha tamaa. Ni suala ambalo linamuweka mtoto katika mazingira magumu.

Lakini kwa jitihada ya makusudi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na wizara zitakazohusika nyengine, ni kwamba pamoja na misaada ya *UNICEF*. Wamejitahidi sana kushirikiana na wizara kuhakikisha kwamba wale watoto wote wamepewa ajira katika umri mdogo wanafanyiwa utaratibu wa kurudi maskulini. Na wakirudi maskulini kuwashauri wazazi wao basi waweze kupewa utaratibu mwengine wa kuweza kuongeza pato la chakula kwa siku. Ni pamoja na wizara Mhe. Rais kuhakikisha kwamba anaongeza mapato kwa ajili ya mikopo mbali mbali na suala la ujasiriamali, na njia mbali mbali za kuhakikisha kwamba tunapata ajira, kuanzia watoto, wazee, vijana na wengine wote waweze kupata haki zao.

Mhe. Naibu Spika, sina maneno mengi ya kusema isipokuwa ninapenda kusema tu niunge mkono kwa asilimia mia kwa mia kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kwa sababu inahitaji msaada wa kila mtu anayeishi katika nchi ya Zanzibar na duniani kote. Kwa sababu mwalimu peke yake hawezi kumlea mtoto ikiwa mzazi anayempeleka mtoto hashirikiani naye. Watoto wote wanaoendelea, wanaofanya vizuri ni wale ambao wanakuwa karibu na walimu wao kuwafuatilia. Mzazi akiitwa skuli aende akasikilize, amjue mtoto yupo wapi na anafanya nini na wazazi waweze kujua kwamba walimu michango yao ni muhimu, kwa sababu yeye mzazi, mwalimu anapewa kwa muda wa masaa manane anamlea yule mtoto akiwa skuli. Lakini masaa yote yaliyobakia hayo yanakuwa chini ya uongozi wa wazazi pamoja na majirani, ndugu na marafiki. Kwa hivyo kwa ushirikiano huo ndiyo huo pekee utakaoweza kusaidia kwamba Wizara ya Elimu inafanya vizuri.

Mhe. Naibu Spika, kwa haya machache napenda kuunga mkono na kuwabariki sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Mouldine Caustico. Mhe. Rashid Ali Juma karibu.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi nichukue fursa kwanza kukupongeza wewe kwa umahiri ambao unauonesha hapo mbele na namna utakapotupangilia huku juu ya kuchangia hizi hoja ambazo zinawakilishwa na hususan hizi hoja zetu za bajeti.

Shukurani za pekee na mimi nimpelekee na kumpongeza sana Mhe. Balozi Mhe. Seif Ali Iddi kwa uvumilivu wake na umakini ambao wanatuonesha tangu tunapolianza Baraza asubuhi na kuwa naye pamoja na kukabiliwa na majukumu mengi, lakini bado tunakuwa tupo naye pamoja, anatupa nguvu kwa hili.
Mhe. Naibu Spika, nimpe pongezi sana Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kwa hotuba yake hii aliyoiwasilisha. Kwa kweli ni moja katika hotuba ambayo imewasilishwa kwa aina yake, imegusa mambo yote yanayohusiana na wizara hii. Na sisi kama walimu hotuba hii tunaipongeza na imetugusa sana.

Baada ya kutoa pongezi zangu hizo nitangulize kuunga mkono bajeti hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa asilimia zote ambazo tunapaswa kuunga mkono.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka nizungumzie mambo mawili matatu tu kwa ufupi wake. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, wizara hii ni moja katika wizara mama. Wizara ambazo si wizara zinahudumikia kwa namna moja au nyengine miradi mikubwa ya kuleta maendeleo, ya kuonesha mambo ambayo yanaonekana wazi wazi. Lakini ni moja katika wizara ambayo mimi ningeiita ni uti wa mgongo wa wizara zote. Na uti wa mgongo kwa sababu inagusa umuhimu mkubwa sana na kutokuwepo kwake utendaji wa wizara nyengine zote hazitoonekana. Kwa umuhimu wake huo ningependa sana kuwaomba Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu, lengo kubwa la uwakilishi wetu basi linagusa sehemu kubwa ya wizara hii.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, wizara hii ina mikakati mingi lakini katika mikakati iliyotajwa hapa na iliyochangiwa na wenzetu wengi Wawakilishi, waligusa

mashirikiano ambayo yanahusiana na Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.

Miongoni mwa mikakati iliyochangiwa kwa nguvu ni kuinua uwezo wa watoto wetu wakapata elimu ambayo itawasaidia kuendeleza maisha yao ya skuli na wanapoanza kazi za ajira kwa kuanza kujitegemea.

Lakini kuna mikakati iliyopangwa na kuombwa sana katika kuinua vipaji. Mimi nataka niamini wazi kwamba upatikanaji wa wanafunzi bora unategemea sana mashirikiano makubwa ambayo yapo tayari yanafanywa na yataendelea kufanywa na tutakaa nayo yawe endelevu pamoja na Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo hususan katika sekta ya michezo.

Tuna imani kwamba wanafunzi wetu wanapokuwa mahodari kwenye michezo basi hao wanakuwa na kipaumbele cha uhodari kwenye mafunzo yao. Na pale tunapohisi kwamba tunatoa wanafunzi ambao wana vipaji vya aina yake, wana elimu ya aina yake basi tuelewe wazi kwamba wanafunzi hawa wanakuwa na *extra* ya vipaji vyao katika sehemu nzima ya utamaduni na michezo.

Mhe. Naibu Spika, hivyo basi iliombwa sana kuonekana hapa ni namna gani kutaletwa mashirikiano baina ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.

Wanafunzi wanapofundishwa ziwe lugha mbali mbali kama ilivyochangiwa hapa na Mhe. Balozi Ali Karume, ni kweli kwamba vipaji vya lugha vinaweza vikakuza sana utalii wetu wa ndani ya nchi. Kwa sababu hawa ma-*investors* wetu wanaokuja hapa wote ni wageni wa lugha. Wachache ambao wanatoka ndani watatumia lugha zetu, lakini bado utalii unatawaliwa na lugha ambazo mafunzo yake yanapatikana na chanzo ni Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo wizara yangu itaendelea kushirikiana na kujibu hoja zote zile ambazo wanahisi kwamba mashirikiano baina ya hizi wizara yanaweza kuwa mafupi, tunataka tuwathibitishie kwamba wala Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali hana haja ya kujibu hoja nyingi sana zinazohusiana na masuala ya michezo, utamaduni na masuala ya kuendeleza utalii ndani ya nchi yetu, kwa sababu Mhe. Naibu Spika, hivi ni vitu ambavyo hutaweza kuvilinganisha ukavipembua ukaviweka mbali mbali. Ukitaka kukuza utalii ni lazima uwe na wanafunzi ambao wame-*qualify* vizuri katika sekta zile ambazo wewe unazitarajia zizalishe ipasavyo.

Mimi nataka niwaombe sana Waheshimiwa Wawakilishi, katika kutekeleza majukumu yetu husuan majukumu yetu ya Uwakilishi kwenye majimbo yetu, basi kuna hizi huduma za jamii ambazo kwa njia moja au nyengine zinaweza zikaleta mashirikiano makubwa ndani ya Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Katika kutekeleza ilani zetu za chama chetu ambacho kimetuleta hapa ndani ya Baraza la Wawakilishi, basi tutagundua wazi kwamba kuna mambo ya msingi hatuwezi kuyaepuka.

Kwenye kutekeleza majukumu yetu tunajua kwamba uhifadhi wa mazingira na kuhifadhi skuli ambazo zinatuzunguka katika majimbo yetu ni jambo la umuhimu. Kwa hivyo nawaomba sana Waheshimiwa Wawakilishi wauone umuhimu wa wao wenyewe kufanya jitihada katika kutimiza majukumu yao kwenye kuchangia ipasavyo ndani ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Nitoe mifano Mhe. Naibu Spika, kuna ujenzi wa mambo madogo madogo ya ndani ya skuli zetu ambazo zipo ndani ya majimbo. Nao ni ujenzi wa vyoo. Tutaona katika bajeti hii imeweka kipaumbele kuona kuna mambo ambayo yanarudisha nyuma elimu, viti. Inaonekana kwamba ni mambo ambayo yanarudisha nyuma sana, lakini sisi Wawakilishi na sisi tuna jukumu kubwa sana katika kuhakikisha tunachangia, tunasimamia na tunawafunza watoto wetu waweze kuyalinda na kuyatunza yale mazingira ambayo wanayapata katika muda wote wa skuli.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa nizungumzie suala zima la ajira. Ni kilio kikubwa sana. Inaonekana kwamba michezo kwetu ni ajira, michezo kwetu ni afya, utamaduni kwetu ni ajira, lakini hivi vyote ni vipaji ambavyo vinazalishwa kutokana na chanzo cha Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Watoto wanaopata elimu mpaka kufikia elimu za juu basi hao wanaweza kuwa na bahati ya kupata ajira kupitia serikali, makampuni, lakini wale ambao hawatopata nafasi kama hiyo, kazi za amali ndizo zinazowasababisha kupata ajira kwa nguvu. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, tunapofanya mafunzo ya amali ni pamoja na yale yanayojumuisha Chuo chetu cha Utalii, Chuo chetu cha Habari. Humo mote tunahitaji wanafunzi watoke vyema kwenye Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ili sisi tuwapokee katika hizo kazi za amali na wapate ajira, ziwe za wao wenyewe kujiajiri au za serikali kwa umoja wake.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa nataka niipongeze sana Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mashirikiano makubwa ambayo wanatupa sisi Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, kwa sababu wanafunzi chimbuko lote la kuwafunza tangu hawana kitu akilini mpaka wanakuwa wajuzi na wataalamu, chanzo chake ni elimu. Wakifanya kazi vizuri kwenye elimu pale sisi wizara nyengine ndiyo tunapokea vile vipaji ambavyo vinahitajika.

Nashukuru sana kwa mashirikiano yaliyokuwepo na tunataka tuwahakikishie Waheshimiwa Wawakilishi, tuwaombe tena kwa nguvu moja kwa jitihada zote tulizokujia hapa tuipitishe bajeti hii kwa asilimia mia kwa mia. Ni wizara ambayo haikuhitaji kuwa na kikwazo, kwa sababu sisi sote ndiyo chanzo chake.

Hii bajeti inataka kuwa kubwa kuliko bajeti yoyote na ndivyo inavyopaswa kabisa. Hii bajeti ionekane inahitaji fedha nyingi kuliko bajeti yoyote kwa sababu hii ndiyo inazalisha. Bajeti hii inazalisha. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana, nataka kuunga tena mkono hoja kwa namna nyengine na niwaombe tena Waheshimiwa Wawakilishi, hii siyo wizara ambayo inahitaji vikwazo. Tuipitishe kwa asilimia zote mia kwa mia, ili watoto wetu huko wakapate elimu iliyokuwa bora.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Rashid Ali Juma. Sasa hivi nimpishe Mhe. Dkt. Khalid Salum ambaye ni Waziri wa Fedha na Mipango, na mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa ni Mhe. Haroun Ali Suleiman na baadae atakuja Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kwa ajili ya kutoa ufafanuzi.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, nichukue nafasi hii kwanza kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Lakini kabla ya kuanza kutoa mchango wangu ningeomba kuchukua fursa hii kumpongeza sana Mhe. Rais wetu Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa umuhimu mkubwa anaotoa kwa wizara hii. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Rais na serikali yake imeondoa michango yote katika elimu ya msingi na elimu ya maandalizi. Na vile vile imeondoa michango ya mitihani kwa wale wanaotahiniwa kwa mitihani ya taifa ya msingi na ya sekondari.

Kuondoshwa kwa michango hii bila shaka yoyote kumewapunguzia mzigo wazazi waliokuwa wakichangia, lakini pia inaendeleza azma ya Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kama ilivyoasisiwa na marehemu Mzee Abeid Karume kutokana na mapinduzi ya mwaka 1964.

Kwa hivyo nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Rais kwa maamuzi yake hayo na hii ni uthitibitisho tosha ya kwamba Serikali ya Dkt. Ali Mohamed Shein imeweka kipaumbele katika kuongeza huduma za elimu kwa vijana wetu. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kama ilivyokuwa kwa bajeti zote zilizopita nyuma, sekta ya elimu bado ni sekta inayopewa kipaumbele katika bajeti. Na hata kwa mwaka huu ambapo bajeti yake tunaizungumza mwaka wa fedha ujao wa 2016/2017, ni sekta moja katika zile sekta muhimu ambazo zimepewa kipaumbele katika bajeti. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa mbali mbali wamezungumza masuala mengi likiwemo suala la mikopo ya elimu ya juu. Ningeomba kuchangia katika eneo hili kwa kusema kwamba serikali inaelewa tatizo tulilonalo, la kwamba fedha zinazotoka kwa ajili ya wanafunzi wa elimu ya juu hazitoshi, lakini zina sababu yake.

Vile vile tunaamini kwamba serikali inajitahidi kwa kadiri ya uwezo wake kuhakikisha kwamba fedha zinapatikana, zinatolewa kwa wakati na vijana wengi zaidi wananufaika kupata fursa ya mikopo ya elimu ya juu.

Mhe. Naibu Spika, tukiangalia takwimu za mwaka 2013/2014 tulikuwa na wanafunzi wa elimu ya juu waliopata mikopo 2,823, lakini kwa mwaka 2014/2015...

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri, kidogo naomba ukae utaendelea baadae.

Waheshimiwa Wajumbe muda wangu wa kukaa hapa umemalizika kwa sasa, hivyo nitampisha Mhe. Spika, atakuja kwa ajili ya kumalizia kwa Mhe. Waziri, lakini vile vile kwa mawaziri wengine. Kwa hivyo, naomba nimkaribishe Mhe. Spika.

(Hapa Mhe. Spika, alikalia kiti)

Mhe. Spika: Tuendelee.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, kama nilivyoanza kusema kwenye mikopo ya elimu ya juu ni kwamba serikali inajitahidi kadiri ya uwezo wake ili kuhakikisha kwamba vijana wengi zaidi wananufaika na mikopo hii ya elimu ya juu, na inatolewa kwa kiwango kinachotosheleza, lakini vile vile inatolewa kwa wakati.

Pia nikatoa mfano Mhe. Spika, kwamba kwa mwaka 2013/2014, wanafunzi wa elimu ya juu waliopata fursa ya mikopo ni 2,823, lakini kwa mwaka 2014/2015 idadi iliongezeka ya wanafunzi karibu 3,499 walipata fursa hiyo ya mikopo, ikiwa ni ongezeko la asilimia 24.

Kwa hivyo, hii inaonesha wazi kwamba serikali yetu pamoja na hali ngumu ya kifedha, lakini bado umuhimu wa elimu uko juu.

Vile vile suala zima la kuwapatia fursa vijana wetu wa elimu ya juu linatiliwa mkazo, kwa hivyo halipungui linaongezeka kadiri hali ya mapato inavyoongezeka.

Mhe. Spika, niseme tu kuanzia mwaka 2006 hadi 2016 serikali imeshatoa jumla ya shilingi bilioni 30 kwa ajili ya mikopo ya elimu ya juu. Kiwango hiki ingawaje hakitoshelezi, lakini ni kiwango kikubwa ukiangalia matumizi ya serikali kwa ujumla wake. Lakini tukiri tu kwamba pamoja na kima kikubwa kimetoka na madhumuni ya kuanzisha mfuko huu ilikua ni mfuko ambao utajiendeleza, kwa maana *revolving*, lakini kwa bahati mbaya marudisho katika kipindi hiki ni shilingi bilioni 1.52, kima kilichotoka ni kingi bilioni 30, lakini marejesho bado ni kidogo. Kwa hivyo, serikali bado itatakiwa kuendelea kutenga fedha katika bajeti yake na hilo linafanyika.

Kwa mfano, bajeti ya mwaka jana ambayo ni hii tunamalizia sasa hivi ya mwaka 2015/2016. Serikali ilitenga jumla ya shilingi bilioni 8, pamoja na matumizi tuliyokuwa nayo ya matumizi makubwa katika mwaka huu, lakini bado serikali iliweza kutoa shilingi bilioni 4.5 kwa ajili ya mikopo ya elimu ya juu.

Niwaeleze Waheshimiwa Wajumbe na wananchi kwa jumla, bado katika kipindi hiki hiki kifupi cha mwezi huu mmoja tuliobakisha, basi serikali itatenga fedha zaidi kwa ajili ya kuwasaidia vijana wetu hao kwa mikopo ya elimu ya juu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwenye hili pamoja na kwamba sheria inatuhimiza au inatutaka wale wanaokopa warejeshe fedha hizi baada ya kuajiriwa, basi ningeomba

kusisitiza sana wazazi na wanafunzi wenyewe, kwa wale waliokwishapata fursa ya ajira, basi wasisite kurudisha mikopo hii, kwa sababu kurudisha kwao ndio kutatoa fursa na wengine nao kuweza kufaidika na fedha hizi ambazo zinatolewa na serikali.

Mhe. Spika, liko sula la madawati, limezungumzwa na Mhe. Nadir Abdul-latif wa Jimbo la Chaani.

Ni kweli Mhe. Spika, tuna mahitaji makubwa sana ya madawati na hii inatokana pia na kwamba tuna idadi kubwa ya wanafunzi katika skuli za maandalizi, skuli za msingi na sekondari. Tuna idadi kubwa na mahitaji ni makubwa, lakini serikali inalielewa suala hili na juhudi mbali mbali zimekuwa zikichukuliwa na serikali yenyewe ya kutenga fedha kwa ajili ya madawati. Vile vile na washirika wengine wanasaidia katika suala hili.

Mhe. Spika, niseme sababu kubwa miongoni mwa sababu zilizopelekea serikali kuanzisha kodi ya miundombinu, basi ilikuwa ni kupata fedha kwa ajili ya kusaidia shughuli za madawati. Tokea kuanzisha kodi hii fedha zimekuwa zikitengwa mwaka hadi mwaka kwa ajili ya kusaidia madawati, na hata kwenye bajeti ya mwaka huu wa fedha Mhe. Spika, zimetengwa fedha kwa ajili ya madawati. Lakini nikiri kwamba fedha hizo tunazotenga na mahitaji halisi bado ni fedha chache. Lakini serikali kwa kutambua hilo, imeandaa utaratibu maalum ambao utaelezwa hapo baadae wa kusaidia kuharakisha upatikanaji wa madawati, ili kuweza kupunguza tatizo hili kwa kipindi kifupi kijacho.

Mhe. Spika, kuna suala lilizungumzwa na Mhe. Rashid Makame Shamsi wa Jimbo la Magomeni. Yeye alieleza kwamba Wizara ya Fedha na Mipango ihakikishe inatoa fedha za kutosha kwa wizara hii.

Mimi nakubaliana naye kuwa ni miongoni mwa wizara muhimu, na hata akiitizama, pamoja na kwamba mwaka 2015/2016 ulikua kidogo una matumizi mengi na makubwa ya lazima, lakini akitizama vifungu vya wizara hii, basi atakuta kwamba ni wizara ambayo imebahatika sana kupata fedha ukilinganisha na wizara nyengine. Hilo linafanywa makusudi kutokana na umuhimu wa wizara hii.

Mhe. Spika, lakini suluhisho la wizara hili lipo katika kuongeza mapato yetu. Niseme kwamba kama tulivyozungumza tulipokuwa tukiwasilisha bajeti ya serikali kwenye Baraza hili Mhe. Spika, tulisema mwaka huu tutajitahidi kwa kadiri itakavyowezekana, ili kuhakikisha mapato ya serikali yanaongezeka, lakini vile vile tunabana matumizi yasiyokuwa ya lazima.

Madhumuni ya hayo ili kuwa na fedha sasa za kuweza kuhudumia bajeti yetu hii kwa yale mambo ambayo ni ya lazima, na tayari yameshapitishwa katika Baraza lako. Miongoni mwa hayo basi ni bajeti ya wizara hii.

Mhe. Spika, Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata), yeye alizungumzia kuhusu madeni ya walimu na hasa madeni yale ya likizo.

Naamini Mhe. Mwakilishi alifuatilia bajeti ya serikali, na ndani ya bajeti ile miongoni mwa mambo ambayo tumeyakusudia kuyapa kipaumbele katika ulipaji wa madeni ni madeni ya walimu. Nilisema wazi wazi kwamba madeni ya walimu yatatiliwa mkazo na yatalipwa katika mwaka huu wa fedha, zikiwemo fedha za likizo za walimu.

Suala hili la fedha za likizo za walimu kwa kawaida wizara zenyewe wanapopata mgao wao wa *OC*, wanatakiwa watenge fedha kwa ajili ya malipo ya fedha za likizo za walimu, lakini kwa sababu tuna madeni tayari tumeshakaa na wizara inayohusika na tumeshakaa na waziri mwenyewe, tutapanga utaratibu wa kuhakikisha madeni yanayodaiwa hivi sasa basi tunayalipa mwezi hadi mwezi kadiri tutakavyokua tunatoa mishahara. *(Makofi)*

Kwa hivyo, hilo nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi wajue kwamba tumelichukulia uzito unaostahiki na tutalifanyia utaratibu ili madeni hayo yaweze kulipwa.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, naomba niseme kwamba na nitamke naunga mkono hotuba hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango. Sasa naomba nimwite Mhe. Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ili na yeye sasa aweze kutoa mchango wake. Mhe. Waziri karibu.

Mhe. Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe Spika, awali ya yote na mimi namshukuru Mwenyezi Mungu kwa mwezi huu wa Ramadhani kunijaalia kuchangia Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Spika, nitangulie kumpongeza sana Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Mhe. Riziki Pemba Juma, Naibu Waziri Mhe. Maalim Mmanga Mjengo Mjawiri. Kwa kweli nampongeza Mhe. Rais kwa kuwateua watu hawa wawili,

hawa ni *product* ya *SUZA*, na Mhe. Rais ameiangalia sana *SUZA* akaona hapa ndipo pa kuchukua, na hajafanya kosa, hivyo nampongeza sana, ni watu makini na ninahakika watakuja na matunda mazuri.

Kwa hivyo, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali waiangalie sana *SUZA*, kwa sababu ndio mashine yetu au ndio kiwanda chetu cha kutolea watu kama kina Mhe. Riziki Pembe na Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri na wengine wapo wengi kule *in shaa Allah*. *(Makofi)*

Mhe. Spika, niipongeze sana hatua ambayo Mhe. Rais ameichukua katika suala la elimu bila ya malipo. Suala la malipo lina unyonge mkubwa sana jamani. Naomba Mhe. Spika, mimi nitoe mfano halisi wa kabla ya Mapinduzi kwa suala la elimu ambayo imetugusa sisi wenyewe kwenye familia yetu, hao watu wako hai na wanauza maduka yao sasa hivi pale Mchangani.

Mhe. Spika, mwaka 1962 kuna mtu wetu wa familia alitangaziwa kapasi kuingia katika skuli moja, wakati ule ikiitwa St. Joseph, siku hizi inaitwa Tumekuja, zamani ilikuwa St. Joseph unalipia ukifika pale. Sasa ada ya kulipia pale nadhani kama sikosei ilikuwa shilingi tano kwa *term* moja. Sasa kaka yetu mmoja ndiye aliwajibika aende pale, lakini shilingi tano nyumbani hazipo.

Mhe. Spika, nakuhakikishia kaka yule hakupata fursa ile, huo ndio unyonge wa kutokuwa na pesa ya kulipa ada, umaskini matokeo yake ni kama hayo. Kwa hivyo, Mhe. Rais kayaona hayo ya umaskini. Matokeo yake ndio akasema elimu ya msingi itatolewa bila ya malipo na mitihani yote italipwa na serikali itasimamia. *In shaa Allah* Mwenyezi Mungu akitujaalia nina hakika na mwenyewe Rais keshasema, hali itakapotengemaa vizuri, basi *in shaa Allah* ana nia hata elimu ya sekondari nayo itakuwa hivyo hivyo tukijaaliwa *in shaa Allah* tumuombee Mwenyezi Mungu. Tushirikiane sote kwa pamoja katika kuijenga nchi yetu, hili jambo ni letu sote.

Mhe. Spika, nataka nizungumze kidogo mimi kwa upande wangu kuwaomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, jambo ambalo linafanyika na waendelee kulifanya.

Tumo katika kutekeleza sera ya elimu ya mwaka 2006, ambayo inasema miaka miwili ya maandalizi, miaka sita ya msingi na miaka minne ya sekondari. Naomba sana tuliangalie suala hili la elimu ya maandalizi bado mwamko ni mdogo katika maendeleo yetu ya jamii, kuna haja kubwa ya kuendeleza jamii zetu, kufahamu kwamba elimu ya maandalizi ni ya lazima, na ndio sera yetu ya elimu ya mwaka 2006 inavyotuelekeza.

Kwa hivyo, bado baadhi ya wananchi wetu hawajachangamkia sana elimu hii ya maandalizi, na ni muhimu sana. Tukianza kwa maandalizi basi tutapata msingi mzuri vijana wetu watapata mafunzo mazuri.

Jengine Mhe. Spika, kwa nini, na Mhe. Simai Mohamed hili, kwa nini yalitoka maamuzi *Vocational Training* iwekwe katika Jimbo la Makunduchi, kwa nini isiwe mahali pengine popote katika Wilaya ya Kati.

Serikali yetu hii haiangalii mahali kwa sababu ya kupenda tu. Inaangalia *distribution* ya maendeleo mbali mbali. Vyuo Vikuu vyetu vyote viko Wilaya ya Kati, *SUZA* tumejenga Wilaya ya Kati, Tunguu. Sasa kujenga *Vocational Training* kule ilikopelekwa sio kosa, kwa sababu maendeleo haya yanakwenda katika maeneo yote ya nchi yetu.

Mhe. Spika, Pemba inajengwa Daya pale Mtambwe, imejengwa Vitongoji kama ni Makao Makuu ya Mkoa pale *Vocational Training* ya mwanzo. Lakini pia tumeamua na Mkoa wa Kaskazini, wameamua wenyewe wizara, nakumbuka toka nipo mimi pale ikaamuliwa ijengwe katika Mkoa wa Kaskazini Pemba. Kusini wameshapata, sasa Kaskazini, na Kaskazini inajengwa katika Jimbo lile la Mtambwe katika sehemu ya Daya pale. Ni jambo zuri na maendeleo haya ni lazima yasambazwe kila mahali wapate maendeleo hayo.

Kwa hivyo, leo *SUZA* ipo Tunguu, *Vocational Training* inajengwa huko Kusini si kwa sababu yoyote, kwa sababu Makao Makuu ya Wilaya yako Kusini vile vile huko huko inakojengwa hii *Vocational Training*, sio tatizo, ni lazima tusambaze maendeleo huko.

Jengine *Vocational Training* inakidhi mahitaji ya wanafunzi mbali mbali ambao hawakupata bahati ya kuendelea na masomo mengine haya ya sekondari. Kule ni ukanda wa biashara ya utalii, kuna na suala zima la kilimo, uvuvi ni sehemu kubwa sana na barabara imetoka Michamvi mpaka inakuja Makunduchi, mpaka inakwenda Kizimkazi, Muyuni na Kitogani, ni eneo ambalo ni *very strategic* katika kuendeleza maendeleo ya kiuchumi katika eneo lile. Kwa hivyo, sio kosa kupeleka maendeleo yale katika eneo lile, mimi nadhani ni ku- *strengthen development* katika maeneo mbali mbali.

Mhe. Spika, jengine ambalo nataka kulizungumza kidogo ni suala la madawati. Mhe. Spika, nashukuru sana Waziri wa Fedha na Mipango amelizungumzia vizuri sana, na katika kulizungumzia amezungumza jitihada zinazofanywa katika jambo ambalo linamgusa sana Rais wetu basi ni suala zima la madawati.

Rais linamgusa, Makamu wa pili linamgusa, na mawaziri wote linatugusa na sote linatugusa suala hili la madawati.

Mhe. Spika, kwa taarifa Mhe. Rais ameunda kamati ya mawaziri pamoja na wajumbe wengine, kwa ajili ya kutafuta madawati hakuna kazi nyengine yoyote, kwa sababu tunaguswa sana na hali hiyo.

Nilisikia mchango wa Mhe. Raza na Mhe. Nadir Abdul-latif alichangia kuhusu madawati, akataka mpaka mabusati sijui mikeka ipelekwe sina hakika, sikuwepo lakini nimesikia hivyo nimeambiwa. Lakini nilimsikia Mhe. Raza anasema tuyachangie nusu na nusu apewe masharti kwamba apeleke jimboni kwake serikali ichangie. Hatuchangii kwa sababu ya kusaidia majimbo moja kwa moja, kwamba kila mtu achangie hivi na jimbo lake lisaidiwe hivi. Tukichangia tunachangia kwa jumla kwa nchi nzima. Sasa haiwezekani kwamba tunachangia halafu wewe kwa sababu umechangia nusu basi usaidiwe nusu. Isipokuwa tunapendekeza, tunafurahi kama wewe tayari umeshaamua basi itakuwa vizuri.

Mhe. Spika, *In sha Allah* tukijaaliwa serikali inakusudia kuleta kauli ya serikali hapa, kuhusu suala zima la madawati.

Nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi sote tushirikiane katika jambo hili, tuchangie katika suala hili la madawati, kuwahamasisha wananchi katika maeneo yetu ili kuhakikisha suala la madawati hili basi tunalichukulia hatua na tunachangia sote, kwa sababu linatugusa sote, hatufurahi kuona watoto wanakaa chini.

Mhe. Spika, niipongeze sana hatua ambayo inachukuliwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali sasa hivi. Niwaombe wafanyakazi wote wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kuanzia walimu, Maafisa Elimu wa Wilaya na Mikoa, watendaji, Wakurugenzi, Ofisi ya Katibu Mkuu na wasaidizi wake wote wampe mashirikiano makubwa waziri na naibu waziri. Nina hakika wana nia nzuri na watafika mbali sana katika maendeleo ya elimu katika nchi yetu.

Mwisho Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali nakuomba sana iangalie Skuli ya Kibuteni inayojengwa sasa hivi, nakuomba sana. Sitaki kuzungumza zaidi ya hapo, iangalie. Nashukuru kuna baadhi ya waheshimiwa walilizungumza suala hilo. Kwa hivyo, liangalie, inavunja moyo sana ukipita pale.

Mimi kila siku nikienda jimboni kwangu nikipita pale basi hata sitizami tena, naona vibaya na wananchi waliniuliza maswali nikawaambia basi *In shaa Allah* salamu zitafika, nimezifikisha, naomba Mhe. Waziri, Naibu Waziri na watendaji mlionao mnaielewa vizuri Skuli ya Kibuteni na *In shaa Allah* Mwenyezi Mungu atawasaidia.

Naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja *In shaa Allah*. Waheshimiwa sote tuunge mkono. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Waheshimiwa Wajumbe, sasa naomba nimwite Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali ili na yeye aje atoe mchango wake. Karibu Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii kujibu baadhi ya hoja zilizoletwa na Waheshimiwa Wawakilishi.

Awali ya yote nitumie fursa hii kumpongeza sana Rais wetu Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa ushindi wa kishindo alioupata. *(Makofi)*

Pia, nampongeza sana Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Pili wa Rais, lakini pia nawapongeza wawakilishi wenzangu wote tuliopata ushindi wa kishindo na tulioteuliwa.

Baada ya kushukuru sasa nianze kuwashukuru sana sana Wawakilishi wenzangu tulioanza kuichangia hotuba hii, lakini kwanza ningependa kusema kwamba ndugu Wawakilishi kwa hakika mnajua mengi sana ambayo sisi Waziri wa Elimu, na Mimi pamoja na watendaji wetu ambayo hatuyajui, lakini pia na sisi tunajua mengi ambayo na nyinyi hamyajuwi. Kwa hivyo tupo hapa kubadilishana kile mnachokijua mnatwambia na mmeshaanza na sisi tunachokijua tunawaambia, kwa hivyo tunaambiana kwa ajili ya maendeleo ya Zanzibar.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo sasa nianze kujibu baadhi ya hoja na nitaanza suala ambalo liliulizwa na Mhe. Shehe Hamad Mattar ambae alitaka kujua kuhusu malipo ya kujikimu na posho kwa walimu ambao wanasimamia mitihani ya darasa la sita na *Form* II. Mhe. Spika, ni kwamba walimu wanaosahihisha mitihani katika kiwango hicho, kwa kweli huwa hawalipwi

posho la kujikimu kwa sababu wanaishi kambini na hupatiwa huduma zote pamoja na nauli ya kwenda na kurudi.

Kwa upande wa walimu wanaosahihisha mitihani ya walimu ambao huwa hawakai kambini wao hulipwa posho zote ikiwemo posho la kujikimu, kwa hivyo hapa pana suala la ufahamu tu kwamba walikuwa labda Waheshimiwa Wawakilishi walikuwa hawaelewi hilo kwamba hakuna posho katika kazi hiyo, lakini inawezekana pia na walimu wenyewe wakawa walikuwa hawaelewi. Lakini waelewe kwamba katika kazi hiyo huwa hakuna posho maalum.

Mhe. Spika, ningependa pia kumjibu Mhe. Zulfa Mmaka Omar, yeye alitaka kujua Skuli ya Mgogoni kuna walimu kidogo ukilinganisha na mahitaji ya wanafunzi. Kwa kweli Mgogoni ina madarasa 27 na walimu 47 wa mgao wa madarasa kwa walimu ambao ni madarasa mawili kwa walimu watatu, skuli ingepaswa kuwa na walimu 41. Hivyo kuna ziada ya walimu sita, kwa hivyo hoja yake kidogo inakuwa mushkeli. Ni kweli idadi kubwa ya wanafunzi ambalo ni tatizo la kitaifa kwa skuli nyingi za Wilaya ya Magharibi matumaini yetu tutakapokamilisha madarasa yaliyopo tutaweza kupunguza idadi ya wanafunzi.

Mhe. Spika, pia kulikuwa na suala lililoulizwa na Mhe. Hamza Hassan Juma kuhusu ujenzi hasa mpango wa Wizara kuzuia mmong'onyoko katika skuli ya Sekondari kwa Mtipura. Ni kweli skuli hii hata mimi binafsi nilipata fursa ya kuitembelea tatizo hili la mmong'onyoko lipo, lakini suala hili naomba tushirikiane na uongozi wa jimbo katika kuwaelimisha wananchi athari za uharibifu wa mazingira. Aidha, Wizara yangu italifuatilia kwa karibu suala la skuli ya Kwamtipura na nyenginezo zenye matatizo kama hayo ili kuzipatia ufumbuzi unaostahili. Lakini kama Wizara tungependa masuala kama haya viongizi wa majimbo, Masheha na Wawakilishi kwa kweli msaidiane ili kuzuia athari kabla haijaleta madhara makubwa zaidi, ni kweli mimi nilipata fursa ya kutembelea skuli nyingi, tumegundua suala kama hili na tumewaelekeza Walimu wakuu, kwa kweli matatizo madogo kama haya washirikiane na kamati za skuli na viongizi wengine kutatua.

Mhe. Spika, kuna suala lililoulizwa na Mhe. Asha Abdalla Mussa na Mhe. Ali Khamis Bakari, kuhusu kutolipwa posho wasaidizi wa Wilaya ya Kaskazini B. Mhe. Spika, hawa ni wasaidizi wapya ambao hawakuingizwa katika bajeti iliyopita, hivyo katika bajeti mpya Wizara imewaingiza na *in shaa Allah* watapata malipo yao.

Mhe. Spika, kuna suala jengine ambalo limeulizwa na Mhe. Ame Haji Ali, yeye alitaka aelezwe kwamba uelewa wa jamii kuhusiana na mafunzo ya amali bado ni mdogo, Wizara inakubali kwamba uelewa katika suala la elimu hii ni mdogo sana sana wazee wengi tumebakia kuwaelekeza watoto wetu katika upande huu ambao tunaita *academic* zaidi, lakini kwa kweli misingi hasa wa elimu ni upande huu wa mafunzo ya amali. Kwa hivyo Wizara itaendelea kuchukua hatua za kuelimisha wazazi juu ya umuhimu wa elimu hii ambayo itawasaidia sana mbali na kupata mwamko lakini pia wataweza kujiariji, kazi hii tutaifanya kwa ushirikiano na Wawakilishi yaani ndio nyie waheshimiwa lakini pamoja na Kamati za Shehia na viongozi mbali mbali wa mitaa.

Pia ningependa kujibu hoja iliyoulizwa na Mhe. Wanu Hafidh Ameir ambae alikuwa anauliza tumesaidia vipi kupunguza idadi ya wasioajiriwa. Jumla ya wanafunzi 105 wamehitimu vikundi saba vya walimu vimekopeshwa mkopo nafuu usio na riba, vijana wasiopungua 35 wanajishughulisha na shughuli zao wenyewe kwa mara nyingine wameweza kujiajiri wenyewe. Baadhi yao tulipowatembelea wanaendelea vizuri na wameshaanza kutaka kuajiri wenzao.

Mhe. Spika, suala jengine limeulizwa na Mhe. Said Omar Said kuhusu mafunzo ya amali, yeye anauliza ni wanafunzi wangapi wa Pemba wamemaliza mafunzo ya Amali na wangapi wamewezesha kujiajiri. Mhe. Spika, jumla ya wanafunzi 267 wamemaliza mafunzo ya amali katika kituo cha Kitongoji Pemba tarehe 20 Disemba 2015, wanafunzi wamewezeshwa kujiajiri kwa kupatiwa mafunzo ya ujasiriamali. Pia wamepatiwa elimu ya kuanzisha na kundeleza vyama vya ushirika ambapo pindi tu wakimaliza masharti ya kuanzisha na kuvisajili vikundi vyao wana uwezo wa kuomba mkopo nafuu na usio na riba kutoka mamlaka, kwa lugha nyengine wamewezeshwa kupewa maarifa wapi wanaweza kupata mikopo, wapi wanaweza kufanya wakatambulika kwa mfano lazima vikundi vyao visajiliwe rasmi na vitambulike ili iwe ni sababu mojawapo ya kupata mkopo.Kwa hivyo tutatarajia wakimaliza mafunzo haya kusajili Mamlaka itawasaidia kuweza kupata mikopo nafuu.

Suala jengine ni lile lililoulizwa na Mhe. Asha Abdalla Mussa na Mhe. Khadija Omar nalo lilikuwa linazungumzia kutolipwa nauli. Mhe. Spika, Wizara inajitahidi sana kulipa nauli kwa wakati posho hili hutolewa sambamba na mishahara, naahidi tutafuatilia suala hili wasiolipwa na wanaostahili watalipwa. Wizara inawalipa mishara wakati wa mwisho wa mwezi na wale ambao watakuwa wamesahaulika Wizara itafutilia na kuhakiki na watapewa maslahi yao.

Mhe. Spika, suala jengine linahusu walimu nalo kuandaliwa mpango wa kuajiriwa walimu wa sayansi, ni kwamba Wizara imo katika hatua ya kukamilisha hatua ya uchambuzi wa mahitaji ya walimu wa sayansi. Hivi sasa tunahitaji walimu wa sayansi 607 na waliopo sasa ni 636 ndio maana nikasema kwa sasa tunafanya uchambuzi, ili kuona mahitaji halisi ya walimu wa sayansi. Itakapokamilika kama tulivyosema kwamba tutaiomba Serikali kupitia tume ya Utumishi kuweza kupata kibali cha kuajiri walimu hao.

Hoja nyengine imetolewa na Mhe. Ame Haji Ali nae pia alikuwa katika suala hili hili la walimu kupatiwa nafasi za ajira ya Wizara kutoka Afisi ya Rais Utumishi, bila ya shaka nimeshaeleza Wizara yangu hivi sasa inasubiri maelekezo kutoka Afisi ya Rais Utumishi juu ya namna itakavyoweza kutekeleza ajira hii kwa mujibu wa nafasi tulizokubaliwa.

Mhe. Spika, hoja nyengine ilikuwa ni upungufu wa walimu katika Mkoa wa Kaskazini na walimu kuhamishwa mara kwa mara, napenda nikiri kwa sasa kuna upungufu wa walimu katika Mkoa wa Kaskazini Unguja, hivyo Wizara yangu itafanya uchambuzi mpya kwa mahitaji ya walimu kwa Mkoa wa Kaskazini Unguja ili kufahamu upungufu uliopo na hatimae kutekeleza yafuatayo.

1. Kufanya uhamisho wa ndani ya Mkoa wa Kaskazini.
2. Kuwasilisha maombi yetu katika Afisi ya Rais Utumishi kwa ajira mpya.
3. Uhamisho wa walimu kuja mjini utaweka utaratibu mpya.

Kwa maana kwamba tunajaribu kuangalia mambo haya ili kuweza kukidhi au kupunguza mahitaji ya walimu, inawezekana wakati mwengine ikawa ni mpangilio mbaya kwa hivyo tunafanya uhakiki ili kuona pengine tunaweza kuhamisha mwalimu kutoka Chaani akenda Gamba, au Gamba akenda Pale hivyo tunafanya sasa hivi.

Mhe. Spika, hoja nyengine imetolewa na Maalim mwenzangu Rashid Makame Shamsi kuhusu wafanyakazi wa ghala na suala la wizi wa vitabu ghalani, ni kweli mwaka jana kulitokea wizi wa kuibiwa vitabu vya wanafunzi ghalani suala hili liliwahusisha wafanyakazi watatu wanaume ambao Wizara imechukua hatua zifuatazo:

1. Kulifikisha suala hili polisi kwa uchunguzi na hatua zao.

2. Kuwasimamisha kazi wafanyakazi hao kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi Serikalini Sheria namba mbili ya utumishi wa umma ya mwaka 2011.

Kwa hivyo suala hili linafanyiwa kazi na vyombo vinavyohusika.

Hoja ya Mhe. Hamza inahusika, nayo pia iko katika suala la walimu ulipaji wa posho la likizo na malimbikizo yanayotokana na marekebisho ya mishahara ya walimu; ni kweli hivi sasa tunadaiwa malimbikizo kutokana na kutolipwa kwa posho la likizo kwa wakati kutolipwa kwa malimbikizo ya Wizara yangu mwaka jana ilifanya vikao viwili rasmi na Wizara ya Fedha vikiongozwa na Mawaziri wawili yaliyokuwepo wakati huo kujadili namna ya kulipa malimbikizo hayo na ahadi iliyotolewa ni kuwa malimbikizo hayo yatalipwa kwa awamu, hivyo tunasubiri maelekezo ya Wizara ya Fedha naahidi tutafanya kikao chengine na Wizara ya Fedha kwa ajili ya utekelezaji wa suala hili. Na walimu waliostaafu kazi nitahakikisha wanalipwa haki zao.

Aidha, Mhe. Hamza Hassan Juma alitaka kujua uanzishaji wa kozi za elimu mjumuisho, kwa mujibu wa utaratibu wa Chuo kozi yoyote inayoanzishwa ni lazima ifanyiwe *need assessment* na kushirikisha wadau juu ya kozi hiyo, hivyo mtaala huu umeonekana unajitosheleza na programu hii haina mashaka kwa kuwa imekubalika na mamlaka ya vyuo vikuu Tanzania. Vile vile chuo huwa kinaazima walimu wa muda pale kinapohitajika kozi hii imeanzishwa rasmi kukidhi haja ya Sera ya elimu ya Zanzibar ya mwaka 2000, hata hivyo ushauri wa Mhe. Hamza tutaufanyia kazi.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa utaratibu ni kwamba kila programu inayoanzishwa inahitaji kufanyiwa utafiti wa kina kuona ubora wake na mahitaji yake na kisha ripoti hii inapelekwa katika mamlaka za vyuo vikuu ili kuthibitishwa na kupewa ruhusa ya kuanzisha kozi hiyo.

Mhe. Spika, napenda kujibu hoja ya Mhe. Salma Mohammed juu ya ajira kwa kujaza nafasi Wizara yangu hivi sasa ina hakiki taarifa za walimu waliostaafu kwa kipindi cha Aprili hadi Juni 2016, hivyo kazi hii ikikamilika itawasilishwa Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa hatua zao kabla ya mwezi huu kumalizika, hivyo Wizara yangu itajaza mapengo kwa skuli zenye upungufu mkubwa wa walimu.

Mhe. Asha Abdalla Mussa na Mhe. Ame Ali Ali wao pia wamekuja na hoja inayohusu wafanyakazi kujihusisha na siasa, Waheshimiwa Wajumbe nimepokea taarifa hii na nakuombeni tushirikiane kwa kuwabainisha hao

walimu wanaojishughulisha na siasa hali ya kuwa wako kazini, kanuni ya utumishi Serikalini ya mwaka 2014 iko wazi kuwa anayetaka kujishughulisha na siasa ana fursa ya kuchukua likizo bila ya malipo. Jambo hili katika ziara zangu za skuli mimi na Mhe. Waziri, tumekuwa tukiwakumbusha walimu juu ya kutii Katiba, sheria na kanuni zilizopo na tumesema kwamba kwa hatua ya mwanzo tunawakumbusha wazipitie sheria ili wajue lipi wanapaswa kufanya na lipi wanakatazwa ili zikija zikichukuliwa hatua wawe wajilaumu nafsi zao. Kwa hivyo Wizara imechukua hatua za kuwakumbusha walimu namna ya kutii, Katiba, Sheria na Kanuni za nchi.

Aidha, Mhe. Zulfa nafikiri tumeshamjibu na nadhani Mheshimiwa nimalizie hapo niseme tu kwamba mimi binafsi naiunga mkono hoja hii na nawaomba Wawakilishi, waiunge mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipatia nafasi hii kuweza kutoa mchanganuo wa hoja mbali mbali ambazo zimetolewa na wajumbe. Kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia neema hii ya uhai, uzima na afya leo kuweza kukutana hapa katika kuchangia na kuipitisha bajeti ya Wizara yetu adhimu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Spika, naomba nianze kwa kuwashukuru wale wote ambao wamechangia hotuba yaetu hii wale ambao walichangia na wale ambao walichangia kwa maandishi, nitaanza kwa kuwataja mmoja baada ya mwengine.

1. Mhe. Nadir Abdullatifa
2. Mhe. Mohammedraza Hasanali
3. Mhe. Asha Abdalla Mussa
4. Mhe. Ame Haji Ali
5. Mhe, Mwantatu Mbarak Khamis
6. Mhe. Wanu Hafidh Ameir
7. Mhe. Ali Khamis Bakari
8. Mhe. Rashid Makame Shamsi
9. Mhe. Zainab Abdalla
10. Mhe. Said Omar Said
11. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
12. Mhe. Ali Suleman Ali
13. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi
14. Mhe. Panya Ali Abdalla
15. Mhe. Abdalla Maulid Diwani
16. Mhe. Mohammed Said Mohammed
17. Mhe. Simai Mohammed Said

Mhe. Spika, Vile vile nawashukuru Mawaziri wenzangu nao kwa kuchangia hotuba yetu hii ya bajeti ya Wizara ya Elimu, nianze kwa kumshukuru.

1. Mhe. Balozi Ali Karume
2. Mhe. Moudline Cyrus Castico
3. Mhe. Said Sudi Said
4. Mhe. Rashid Ali Juma
5. Mhe. Dkt. Khalid Salum
6. Mhe. Haroun Ali Suleiman
7. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri.

Mhe. Spika, lakini vile vile naomba niwatambue wale ambao walichangia kwa maandishi wako baadhi ambao walichangia kwa maandishi, lakini vile vile walipata nafasi ya kuchangia kwa sauti, kwa hivyo wanaweza wakajirudia lakini walichangia pia kwa mchango wa maandishi.
Naomba niwatambue:

1. Mhe. Shehe Hamad Mattar
2. Mhe. Mohammed Said Mohammd
3. Mhe. Zulfa Mmaka Omar
4. Mhe. Wanu Hafidha Ameir
5. Mhe. Nassor Salim Ali
6. Mhe. Salma Bilali
7. Mhe. Khadija Omar Kibano
8. Mhe. Omar Seif Abeid
9. Mhe. Hamza Hassan Juma
10. Mhe. Mgeni Hassan Juma (Naibu Spika)
11. Mhe. Ali Khamis Bakari
12. Mhe. Harous Said Suleiman (Naibu Waziri wa Afya)
13. Mhe. Juma Ali Khatib (MBM)
14. Mhe. Shadya Mohammed Suleiman
15. Mhe.Chum Kombo Khamis (Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo)
16. Mhe. Shaib Said Ali
17. Mhe. Mwanaasha
18. Mhe. Miraji Khamis Mussa Kwaza
19. Mhe. Mussa Ali Mussa

Ni imani yangu kwamba wote ambao wamechangia nimewataja lakini kwa namna moja ama nyengine kama atatokezea Mheshimiwa kama sikumtaja basi

naomba pia atanieleza ili niweze na yeye kumuorodhesha katika orodha ya waliochangia. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nami naomba niendelee katika kutoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja mbali mbali ambazo wajumbe wameweza kuzichangia kwa wizara yetu hii tukufu. Kwanza kabisa nishukuru kwa michango yote ambayo wajumbe mmeitoa, michango ambayo mmeitoa lengo lake moja tu ni kujenga elimu ndani ya nchi yetu ya Zanzibar. Imani yangu kubwa sote tuliomo humu tunaumwa na elimu lakini vile vile kila mmoja wetu anapenda kuona elimu na ufaulu kwa vijana wetu nao unakuwa kwa kiasi kikubwa.

Kwa hivyo katika hili niwashukuru sana sana, watendaji wote wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Nikimuanza Katibu Mkuu pamoja na timu yake yote ya wizara. Kwa kweli tuseme kwamba kazi kubwa sana inafanywa na Wizara yetu ya Elimu. Kabla sijawa Waziri tunasikia mengi lakini baada ya kuwa katika nafasi na nimshukuru sana Mhe. Rais kwa hili, kwa kweli kwenda pale nimeona kwamba kazi kubwa sana inafanywa na watendaji wetu. Kwa hilo tuwapongeze sana. Lakini vile vile niwashukuru sana kwa mashirikiano yao ambayo sisi wanatupatia. Kwa kweli mashirikiano ni mazuri sana na Mungu *in shaa Allah* awazidishie juu ya hilo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, masuala mengi yamefafanuliwa na baadhi ya mawaziri lakini hata na Naibu Waziri pia nae ameyafafanua. Lakini twende na yale baadhi ambayo mengine hayakupata ufafanuzi wa kina nikianza na suala zima la ujenzi ambalo limezungumziwa na Mhe. Ame yeye alitaka kuja labda idadi ya majengo yanayotakiwa kukamilishwa kwa 2016/2017. Jua ya hili napenda niseme kwamba madarasa yote yanayohitajika kukamilishwa ni 367 kwa Unguja na Pemba na kwa mujibu wa bajeti yetu 2016/2017 Wizara inatarajia kukamilisha madarasa 120; 72 kwa Unguja na 48 kwa Pemba. Ukamilishaji wa madarasa haya utazingatia vigezo maalum kama vile wingi wa wanafunzi katika eneo husika. Hatuwezi kujenga madarasa pale pahala ambapo wanafunzi labda idadi ya watoto ni kidogo, zaidi tutazingatia eneo lina wingi wa watu wangapi, ama ni watoto wangapi ambao wanataka kupata elimu. Kwa kutokana na hilo hapo tutaweza kukamilisha madarasa ambayo yapo.

Vile vile kama ambavyo ameeleza Skuli ya Bwereo katika jimbo lake la Nungwi, kama ambavyo sisi wizara tutaona kwamba inakidhi hivyo vigezo ambavyo tumevitaja, basi Mheshimiwa nikuhakikishie na ridhika moyo wako kwamba hilo jengine tutalikamilisha. Lakini juu ya hilo wizara kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo kama vile Dubai *Care*, *Zanzibar*

Milele Foundation na wafadhili wengine inaendelea na ujenzi wa madarasa katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar Unguja na Pemba yake.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo limejitokeza ni suala la elimu mjumuisho ambalo Mhe. Mwantatu amelizungumza sana. Alitaka kujua vifaa vya kufundishia watoto wenye mahitaji maalum. Napenda nimjibu Mheshimiwa kama ifuatavyo; kwamba ni jumla ya vitabu 2540 vya wanafunzi wenye mahitaji maalum vimechapisha. Kati ya hivyo vitabu 1700 ni vya nukta nundu na vitabu 840 vya wanafunzi wenye uoni hafifu kwa masomo 10 ya darasa la tano na sita. Aidha, katika mwaka wa fedha 2015/2016 wizara iko katika hatua ya kununua miwani 470, mashine ya kuchapia maandishi ya wasioona moja, mashine za kurekodia 7 na mashine moja ya kupimia usikivu. Jumla Tanzania shilling 52,000,000 zitatumika kununulia vifaa ambavyo tumevitaja hapo. Kwa nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba wizara inaliona na inatambua mahitaji ambayo yapo, lakini hatujaacha mkono sekta hii na tutaenda nayo inshaallah na utaona mafanikio ambayo utayaona.

Kuhusu suala la kushirikiana na vyuo vikuu ili kutoa elimu ya mahitaji maalum na lugha za alama wizara imeweza kushirikiana na SUZA kwa kozi ya stashhada ya Elimu Mjumuisho, ambayo jumla ya alama ni miongoni mwa masomo yaliyofundishwa. Naomba nikuhakikishie juu ya hili Mheshimiwa kwamba kwa sababu na mimi nilitokea SUZA na kwa bahati nzuri nilipata nafasi ya kuwasomesha wanafunzi hawa wa elimu mjumuisho. Kwa hivyo na hiki kitu nakuhakikishia kwamba kipo si cha kudanganya.

Vile vile Mhe. Mwantatu alitaka kujua kuhusiana na kupatiwa walimu wenye sifa kusaidia kufundisha wanafunzi wenye mahitaji maalum. Juu ya suala hilo Mheshimiwa ni kwamba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ili kukabiliana na tatizo hilo tayari inaendelea kuwajengea uwezo walimu kupitia mafunzo ya cheti cha elimu mjumuisho ambayo yanatolewa kwa Unguja na Pemba katika Chuo cha Kiislam Mazizini, mafunzo hayo yanatolewa ya Elimu Mjumuisho. Lakini vile vile katika vyuo vya ualimu vya Pemba pia mafunzo hayo yanapatikana na ukizingatia na Chuo Kikuu cha SUZA tayari nao wameanza. Kwa hivyo Mheshimiwa juu ya hilo litolee wasiwasi.

Suala jengine ambalo pale linahitaji ufafanuzi ni suala lililoulizwa na Mhe. Panya Ali Abdalla ambae yeye alitaka kujua idadi ya wanafunzi waliofaulu darasa la sita na la saba. Naomba nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba jumla ya wananfunzi 25,861 wa darasa la sita walifanya mitihani kwa mwaka 2015. Kati yao wanafunzi 25,773 walifaulu katika ngazi mbali mbali za ufaulu

wakiwemo wanafunzi 44 wa vipawa maalum, 883 wa michepuo na 24,846 waliingia kidato cha kwanza katika skuli za kawaida.

Kwa upande wa darasa la 7 jumla ya wanafunzi 24,668 walifanya mitihani kwa mwaka 2015 kati yao 24,233 walifaulu katika ngazi mbali mbali za ufaulu wakiwemo wanafunzi 51 vipawa maalum, 621 michepuo na 23,563 waliingia kidato cha kwanza katika skuli za kawaida. Kwa hivyo tunaona kwamba ufaulu ambao ulitokezea kwa mwaka jana ulikuwa ni katika kiwango cha hali ya juu. Zaidi kwa wale wanafunzi wa darasa la sita ambao walifaulu vipawa maalum na michepuo, idadi yao ni kubwa zaidi ukilinganisha na wa darasa la 7.

Suala jengine ambalo Mhe. Panya alipenda kulijua ni kuhusu Chuo cha Kiislam alitaka kujua kwamba Chuo hiki kinafanya majukumu yake kama yalivyopangiwa awali. Napenda nimhakikishie Mheshimiwa kwamba Chuo hiki kinafuata muongozo na taratibu zote za serikali kupitia Wizara yetu ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Suala la michepuo ya kiislam ipo kama kawaida inaendelea katika Chuo cha Kiislam Mazizini, ambapo kwa sasa wanafunzi wale wamehamishiwa katika Skuli ya Kiembesamaki skuli mpya. Hii ni kutokana na kutoa fursa kwa Chuo kuweza kupata kuanzisha *course* nyengine mbali mbali. Lakini mchepuo bado upo na unaendelea.

Vile vile, kwa upande wa Pemba masomo hayo yanaendelea katika Vyuo vya Kiislam vya Pemba na wanafunzi hawa wanapomaliza masomo yao wanapata fursa ya kujiunga na vyuo vikuu, wengine wanakwenda katika Chuo cha Alsumait cha Chukwani ambacho tuko karibu nacho. Vile vile wako ambao wanaingia katika Chuo Kikuu cha Taifa cha SUZA na wengine pia wanaingia katika Chuo Kikuu cha Zanzibar. Kwa hivyo Chuo hiki kinafuata kama kawaida lile jambo ambalo limewekwa na serikali na vile vile wizara yangu itaendelea kuhakikisha kwamba malengo ya uanzishaji chuo hicho yanaendelea kuimarishwa na kulindwa kwa maslahi ya wananchi na nchi hii kwa ujumla wake.

Suala jengine lilizungumzwa na Mhe. Jaku Hashim Ayoub ambae yeye aliltaka kujua ukosefu vitabu vya Kingereza, Kiarabu na dini kwa darasa la kwanza mpaka la nne na tatizo hili limetatuliwa vipi. Napenda nimjibu Mheshimiwa kama ifuatavyo; ni kweli kwanza kuna tatizo la vitabu vya kingereza, kiarabu na dini kwa hayo madarasa ambayo tumeyataja. Lakini kwa sasa wizara yetu ya Elimu na Mafunzo ya Amali imefikia makubaliano na *Zanzibar Milele Foundation* juu ya kuchapisha vitabu vya somo la kingereza na vile vile kwa masomo ya Dini na Kiarabu vitachapisha na wizara kupitia ufadhili wa *global parntership for education.*

Kwa hivyo nimuhakikishie Mheshimiwa suala hili tayari sisi pia tumeliona na tunalifanyia kazi na muda si mrefu tu vitabu hivi navyo vitakuwa tayari ili watoto wetu nao waweze kupata fursa nzuri ya kujifunza.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo Mhe. Jaku ambalo Mhe. Jaku alilizungumza ni suala la lugha ya kufundishia, alihoji kwa nini lugha ya kingereza isitumike kama ambavyo inatumika katika skuli za binafsi kwa ngazi ya msingi.

Mhe. Spika, Sera ya Elimu ya Zanzibar ya mwaka 2007, imeelekeza kuhusiana na suala zima la lugha ya kingereza namna inavyotumika. Katika sera yetu ya elimu lugha ya kingereza inatumika kufundishia kuanzia darasa la tano na la sita. Kuanzia darasa la kwanza mpaka la nne tunatumia lugha ya kufundishia ya kiswahili, lakini darasa la tano na la sita tunaanza kufundishia kwa lugha ya kingereza isipokuwa tu kwa baadhi ya masomo. Masomo yenyewe ni kutokana na uhalisia wa masomo yenyewe likiwemo somo la Kiswahili, Kiarabu pamoja na dini. Masomo haya yanafundishwa kwa mujibu wa hizo lugha ambazo zinahusika. Somo la dini linafundishwa kwa lugha ya kiswahili, somo la Kiarabu kwa lugha ya kiarabu lakini somo la Kiswahili lenyewe linafundishwa kwa lugha ya kiswahili na yale masomo yaliyobakia yanafundishwa kwa lugha ya kingereza.

Suala jengine ambalo limezungumzwa na waheshimiwa wengi ni suala la mikopo ya elimu ya juu. Kwa kweli suala hili tayari limeshazungumzwa sana na hata Mhe. Waziri wa Fedha pale ametuhakikishia juu ya upatikanaji wa fedha kwa wanafunzi wetu. Zile changamoto zote ambazo zinajitokeza basi tumuamini Mhe. Waziri wa Fedha kwamba zitatatuka. Ni kwamba ni sawa na waheshimiwa wenzangu tuiamini sana serikali yetu. Serikali ipo kwa ajili ya wananchiwake wa Zanzibar. Kwa hivyo juu ya hilo tusiwe na wasiwasi wizara kupitia serikali kwa ujumla inatimiza wajibu wake.

Lakini katika hili kuna masuala madogo madogo ambayo walitaka kujua mbali ya yale masuala ya fedha, kuhusiana na ushirikishwaji wa wanafunzi katika Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Labda wajumbe niwataarifu tu kwamba miongoni mwa wajumbe 10 wa Bodi mjumbe mmoja anatokea katika Taasisi ya Elimu za Vyuo Vikuu. Kwa hivyo mwanafunzi huyu yeye anakuwa ni kiwakilishi cha wanafunzi wengine, kwa sababu hatuwezi kuchukua wanafunzi wote tukawaingiza lakini anakuwemo mmoja kama ni mwakilishi wao. Kwa hivyo mwanafunzi huyo yupo na hata kwa mwaka huu mimi binafsi yangu nishaandika barua ya kupelekwa huyu mwanafunzi, ili ashiriki katika vikao vya bodi. Tayari katika kikao ambacho kimefanyika kwa mara ya kwanza basi

mwanafunzi huyo ameshiriki na Mheshimiwa Mwakilishi pale nadhani atanisaidia Mhe. Abdalla Ali Kombo analifahamu zaidi juu ya suala hili.

Vile vile katika hapa ni kwamba Mheshimiwa anataka kujua idadi ya wanafunzi wanawake waliopatiwa mikopo katika 2015/16. Naomba nimuhakikishie Mheshimiwa kwamba kwanza katika utoaji wa mikopo wanawake wanapewa kipaumbele sana na katika mwaka 2015/2016 Bodi ilitoa mikopo kwa wanafunzi 1531 kwa wanafunzi wanawake. Wastani huu ni sawa na asilimia 50 ya wanafunzi ambao wanapatiwa mikopo kwa hivyo ni kwamba serikali inaliona hilo na kwa sababu tunaamini kwamba kumuelimisha mwanamke mmoja ni kuielimisha jamii nzima. Kwa hivyo kipaumbele kikubwa tunakitoa kwa hao wanawake kwa sababu na sisi wanawake tuna uwezo mzuri wa kusoma kwa bidii lakini vile vile kila pahala ambapo wanawake wanakuwa wanawekwa basi ufanisi wao wa kazi unakuwa ni mzuri zaidi, kwa hivyo serikali inaliona suala hilo. *(Makofi)*

Suala jengine ambalo Mhe. Naibu Spika, alitaka kujua lini Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu itafanyiwa marekebisho. Naomba nimuhakikishie Mheshimiwa kwamba suala hilo tayari limeanza kufanyiwa kazi. Suala la marekebisho ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, alitaka kujua muda wa urejeshaji wa mikopo, kwa hivi sasa mikopo inarejeshwa kwa kuanzia mwaka mmoja baada ya kumaliza masomo hadi miaka 30. Lakini tunaona kwamba muda huu ni mrefu sana na kutokana na urefu wake kwamba ile thamani ya pesa inakuwa haikidhiwi. Kwa mfano mwanafunzi ambaye amekopa mwaka 2013 analipa mkopo mpaka mwaka 2030, ile thamani ya fedha ambayo yeye alikopeshwa na ile ambayo yeye analipa na kwa kuzingatia ongezeko la ada za wanafunzi. Kwa kweli inakuwa iko juu sana. Kwa hivyo tungeomba sana wale ambao wote wanapata mikopo tulipe kwa wakati na tulipe tukiamini kwamba fedha zile ni za serikali, lakini lengo ni kuwasaidia wananchi wote wa Zanzibar. Kwa hivyo kila ambaye anapata ile fursa basi na yeye aone kwamba kuna mwengine nyuma yake anataka fursa kama ile. Kwa hivyo uzalendo tuweke mbele katika kurejesha mikopo hii ili na ndugu zetu na wao wapate nafasi ya kupata masomo kama ambavyo sisi tumepata. *(Makofi)*

Suala jengine ambalo Mhe. Hamza alitaka kujua ju ya hapa ni kwamba mikakati gani tuliyoipanga ya kuandaa vijana kitaaluma hasa kwenye sekta ya gesi na mafuta. Naomba nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba wanafunzi 30 mpaka sasa wanaendelea na masomo ya mafuta na gesi katika Chuo Kikuu cha Dodoma.

Vile vile kuna Vyuo Vikuu, China, Sudan, Malaysia, Oman na Uingereza pia wanasoma vijana wetu masomo haya ya mafuta na gesi. Lengo ni kwamba tuwe na wataalam wa sekta hii kwa hivyo serikali haijasahau hii sekta na wanafunzi hawa wanapata mkopo tuseme kwamba asilimia 100 ya mkopo wao wanakuwa wanaupata. Lengo ni kukuza hizo fani ili vijana wetu wahamasike kusoma zaidi na zaidi.

Suala jengine ambalo limezungumzwa na Mhe. Zulfa Mmaka Omar kuhusiana na mishahara ya wafanyakazi wenye uzoefu pia Mhe. Ali Khamis Bakari alilizungumzia. Wafanyakazi wenye uzoefu wa miaka 15 hadi 16 mpaka 29 na 30 vipi kuhusiana na suala zima la kuongezewa mshahara. Napenda nifafanue kama ifuatavyo:-

Suala la marekebisho ya mishahara kwa wafanyakazi wenye uzoefu wa miaka 15 na zaidi kutokana na maelekezo ya Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma yaliwahusu zaidi wale waliofikia muda wa kazi iaka 15 hadi kufikia Julai, 2015. Hata hivyo wizara yangu inajitahidi kufanya uhakiki na kuwagundua wale ambao kwa bahati mbaya labda walisahauliwa katika kuongezewa mishahara yao na kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi, Utumishi basi suala hili nalo wale ambao hawajapata basi tutalifanyia kazi.

Suala jengine ni suala la dakhalia ya Wete, Mhe. Shehe Hamad Matar alitaka kujua kuhusiana na wanafunzi ambao wanalala madarasani. Mhe. Mwakilishi, Mwenyekiti wetu wa Baraza napenda nikwambie kwamba suala la wanafunzi kulala madarasani wale ambao wanakaa dakhalia ni kwamba kwa wale wasichana wamekodiwa nyumba karibu na eneo la skuli, ila kwa wale wavulana wanabakia skuli lakini katika kile cha mitihani inapokaribia. Lengo ni kwamba kuwaweka wanafunzi karibu na mazingira ya Skuli ili kuepuka ule uchelewaji. Hata hivyo ni kwamba wizara yetu inajitahidi sana katika kuandaa miundo mbinu mizuri ambayo tutaweza kuongeza dakhalia lakini mipango ya baadae zaidi inshaallah. Kuandaa dakhalia nyingi, ili kuona kwamba vijana wetu wanapata muda mzuri wa kubakia ndani ya maeneo ya skuli. Ili kurejesha ile hali kama ambayo zamani tulikuwa nayo basi wizara *inshaallah* kwa hilo pia italifanyia kazi kwa kadri bajeti itakavyokuwa inaruhusu.

Suala la maktaba ambalo pia Mhe. Hamad Matari alitaka kuimarishwa kwa maktaba za Skuli za Kaskazini Pemba. Mhe. Mwakilishi shughuli za huduma za maktaba tayari limefungua tawi lake katika Wilaya ya Wete na lipo Wete mjini.

Shirika vile vile linatarajiwa kufungua tawi kama hilo Micheweni punde tu jengo litakapopatikana. Kwa hivyo Mhe. Mwakilishi labda yeye kama atakuwa na jengo ambalo lipo basi pia anaweza akaipa wizara ili tuweze kufungua hili tawi la maktaba.

Mhe. Rashid Shamsi; yeye alizungumzia suala zima la michezo alisema kwamba bajeti ndogo ya michezo ambayo inatolewa, wizara yangu imeandaa mpango wa kuibua vipaji na vile vile kuviendeleza vipaji vya watoto wetu mashuleni. Kwa hivyo ni kwamba mpango huu utakuwa na unahitaji zaidi ushirikiano baina yetu sisi lakini hata na wafadhili wa nje. Kwa hivyo ni kweli kwamba bajeti ni ndogo, ruzuku haitoshelezi lakini tukishirikiana kwa pamoja sote tunafahamu umuhimu wa michezo, michezo ni muhimu kwa afya lakini vile vile michezo ni muhimu kwa kukuza akili ya mtoto na hata ule ufahamu wa mtoto. Sambamba na hili kupitia Chuo Kikuu cha *SUZA* kimeanzisha kozi ya *diploma* ya michezo, lengo lake kubwa ni kuwaandaa walimu ambao wataweza kutoa mafundisho haya ipasavyo zaidi. Kwa hiyo, mheshimiwa ni kwamba kweli bajeti ya michezo ni ndogo, lakini kwa kushirikiana sisi Wizara ya Elimu, serikali kwa ujumla wake, viongozi majimboni na hata wale wafadhili wote ambao wanathini sana michezo basi tushirikiane kwa pamoja ili tuone kwamba michezo inakuwa maskulini.

Mhe. Nassor Ali Salum (Jazira) yeye alitaka kujua ujenzi wa Skuli ya Mwembeshauri utaanza lini na utamalizika lini?

Mhe. Spika, naomba nimjibu mheshimiwa kwamba ujenzi wa skuli hiyo upo katika hatua ya kutayarisha michoro ambayo inatarajiwa kukamilisha mwishoni mwa mwezi wa June, mwezi ambao tulionao 2016. Na taratibu za kumtafuta mkandarasi wa ujenzi utaanza mara tu baada ya michoro hiyo kukamilika, na ujenzi huo *in shaa Allah* unatarajiwa kuanza mwaka huu huu wa 2016, na kwa matarajio tunategemea kwamba 2017/2018 basi ujenzi wa skuli hii tayari uwe umekamilika. Kwa hiyo, tuiunge mkono serikali ili jambo hili liweze kufanikiwa kwa ufanisi zaidi.

Vile vile suala la kubadilishwa jina kwa skuli tatu za Rahaleo kama ambavyo Mhe. Rais amelitoa ombi hilo. Ombi hilo mheshimiwa limepokelewa na linafanyiwa kazi kwa mikono miwili na wizara yangu.

Mhe. Panya Ali Abdalla, alitaka kufahamu kuhusiana na suala zima la TUTU (Tucheze, Tujifunze) aliuliza kwamba muda ambao kipindi kile kinarushwa ndani ya redio ni muda wa saa mbili na nusu asubuhi je, lengo linafikiwa?

Napenda nimwambie mheshimiwa kwamba lengo kubwa la utoaji wa kipindi kile ni kwa ajili ya watoto na si kwa ajili ya watu wazima. Kwa hiyo, kwa muda ule wale watoto wanakuwa tayari wapo katika vile vituo vya mafunzo, na wanapokuwa katika vile vituo vya mafunzo wanapata wenyewe wao kufanya mazoezi ambayo yanakwenda sambamba na vile vipindi ambavyo vinarushwa na redio. Kwa hiyo, ni kwamba lengo linafikiwa sana na watoto wanafaidika sana na kile kipindi cha tucheze tujifunze. Lakini mbali ya watoto tu hata walimu ambao na wao wanafundisha wanafunzi wa maskuli mengine pia na wao wanafaidika. Kwa hiyo, lengo ni kuwafaidisha wale watoto na walimu wa TUTU, lakini wanafaidika jamii nzima kwa ujumla wake inapata faida. Kwa hiyo, kusema kwamba muda wa kipindi ni muda wa shughuli za kazi, ni kweli muda wa shughuli za kazi, lakini kwa muda ule walengwa wahusika wanakuwa wanafaidika na kile kipindi.

Mhe. Spika, vile vile Mhe. Panya alitaka kujua kwa nini walimu waliosemea Saateni wasiajiriwe kusomesha na kuondosha uhaba wa walimu katika madarasa?

Suala hili lipo chini ya Wizara ya Utumishi na tayari imelifikia na kwa wale ambao watakuwa wana sifa ule muda utakapofika kutangazwa nafasi za ajira basi pia na wao wataomba na kama wakipata kama sifa zinaruhusu na wao vile vile watafaidika.

Suala jengine Mhe. Ali Khamis Bakar alitoa ushauri kuhusiana na suala zima la kuviona vyuo vya madrasa na kuvijua, suala hili pia limezungumzia na Mhe. Nadiri Jimbo la Chaani.

Waheshimiwa ni kwamba suala la madrasa lipo chini ya Ofisi ya Mufti lakini kwa kushirikiana na wizara yangu tunazifuatilia madrasa hizi kupitia Idara ya Elimu Maandalizi na Msingi. Jumla ya madrasa zilizosajiliwa mpaka sasa kwa Unguja ni 1393 na kwa Pemba ni 893. Kwa hiyo, ni kwamba serikali inatambua uwepo wa hizi madrasa na wizara yangu inakuwa inasaidia katika kutoa mafunzo kwa walimu wale wa madrasa ili kuona namna bora ya ufundishaji, kwa sababu tukitaka tusitake ni kwamba madrasa nazo zinachukua nafasi kama ambavyo pengine skuli inachukua kwa elimu ya dunia lakini kule kwa elimu ya akhera. Kwa hiyo, wizara yangu inasaidia katika utoaji wa mbinu mbali mbali za ufundishaji kwa walimu wale.

Suala jengine ambalo limezungumzwa ni suala zima la taasisi ya elimu, suala ambalo limezungumziwa na waheshimiwa tofauti Mhe. Harous amelizungumza, Mhe. Choum vile vile, Mhe. Abdalla Diwani pia nae

amelizungumza suala la taasisi ya elimu na zaidi walitaka kuhusiana na somo la historia lirudishwe maskulini.

Napenda niwahakikishie wajumbe kwamba somo la historia linasomeshwa katika skuli zetu kuanzia darasa la tano na sita kwa ngazi ya msingi. Kwa upande wa sekondari kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita somo hili pia linafundishwa. Lakini kwa nini baadhi ya huwa hawasomi? Kuna baadhi hawasomi hili somo kutokana na *combination* ya masomo yao. Kwa mfano, mwanafunzi ambaye anaingia kidato cha tano kutokana na *combination* yake inategemea anachukua masomo gani. Kwa hiyo, anaweza akalichukua somo la historia hutegemea na yale masomo husika. Lakini kwa ngazi za huko chini somo hilo linafundishwa, lakini wizara itahakikisha yale mambo muhimu ambayo yanatakiwa yawemo ndani ya somo la historia hasa kuielewa ile historia yetu ya Zanzibar wapi tumetoka, basi itafanya kazi kuhakikisha kama vitu hivyo havipo basi vinaendelezwa zaidi.

Mhe. Zaina alitaka kufahamu suala zima la elimu ya maandalizi kwa watoto wenye mahitaji maalum. Mhe. Mwakilishi suala hilo linafanyiwa kazi na kwa sasa wapo wanafunzi wanaopitia skuli au madrasa ya maandalizi yaliyopo katika vituo ambavyo wanapokea wanafunzi wenye mahitaji maalum. Kwanza kabisa Skuli ya Mwanakwerekwe “H”, Mwanakwerekwe “F” na Mwanakwerekwe “E”. Vile vile Skuli ya Jang’ombe msingi “A”, Kisiwandui msingi, Mwembemakumbi, Pondeani, Michakaeni na skuli ya binafsi ya *ZOP*. Skuli hizi zinachukua wanafunzi hawa ambao nao pia wana mahitaji maalum.

Kuhusiana na vifaa vya kufundishia wanafunzi wenye mahitaji maalum nadhani suala ambalo tayari tushalizugumza kama alivyoliuliza Mhe. Mwantatu aliuliza. Kwa hiyo, ni kwamba serikali ipo katika huo mchakato wa kununua hivyo vifaa na *in shaa Allah* karibu vifaa hivyo vitapatikana. Lakini kuhusiana na suala zima la Baraza la Mitihani kuzingatia wanafunzi wenye ulemavu wa akili katika utungaji wa mitihani.

Suala hili linafanyiwa kazi na litaweza kutekelezwa vizuri zaidi pale sera yetu ya elimu mjumuisho itakapokamilika ambayo ipo mboni kukamilika na kuanza kutumika.

Suala la upungufu wa walimu limezungumzwa kwa sana, waheshimiwa wengi wamelizungumza na tayari tumeshalizungumza suala hilo. Mhe. Jaku vile vile alizungumzia suala la tetesi ya Chuo cha Kiislamu kuunganishwa na *SUZA* na anaomba kibaki kama kilivyo.

Mhe. Spika, kwa sasa wizara inafuata na kuheshimu sera ya elimu ya 2006 ambayo inavitaka vyuo vyote viwe chini ya Chuo Kikuu cha *SUZA*, na tayari Chuo cha Benjamin cha Pemba kiko chini ya *SUZA* na wakati wowote kuanzia sasa *SUZA* itapeleka wanafunzi katika kile chuo. Hata hivyo, suala lako wizara italizingatia na ombi hili tunalichukua tutalifanyia kazi zaidi.

Mhe. Ali Suleiman (Shihata) alitaka kufahamu kuhusiana na Chuo cha Ualimu cha Nkurumah ambacho kilifundisha walimu wa kiwango cha cheti cha ualimu na walimu wale mpaka leo anasema kwamba hawajapata ajira.

Ni kweli kuwa tangu mwaka 2006 hadi 2010 walimu wengi walimaliza masomo yao, wizara inafuata taratibu za maombi ya ajira na kibali kitakapokuwa tayari wataajiriwa kwa mujibu wa sifa zao. Hivyo wizara inawapongeza waliojiunga na kozi ya *diploma* na kwamba itakuwa ni rahisi kwao kuweza kupata ajira, kwa sababu bahati mbaya sana kuna wale ambao walimaliza kwa miaka hiyo hawajajiendeleza, lakini baadhi wamejiendeleza na mpaka kuna wengine wamemaliza mpaka elimu yao ya *degree*. Kwa hiyo, sisi tunawapongeza sana wale ambao wamepata sifa ya ziada na *inshaallah* Mhe. Haroun kupitia wizara yake itakapotangaza nafasi za ajira tuna imani kwamba na hawa nao watakuwa ni miongoni mwa ambao wataomba, na nadhani sifa madhali wanazo basi nao wataweza kuajiriwa.

Vile vile alitaka kujua ni skuli ipi ambayo imepatiwa usajili wa kudumu. Skuli hiyo ni *Karibu Nursery and Primary School* iliyopo Bububu Kijichi. Hiyo skuli imepata usajili wa kudumu.

Vile vile Mhe. Mohammed Said (Dimwa) aliuliza kuhusiana na wanafunzi ambao wanadahiliwa kupitia *CAS*. Mhe. Spika, naomba niwaeleweshe waheshimiwa ni kwamba huu ni uamuzi wa serikali na kwa upande wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar *CAS* ni mfumo wa TEHAMA ambao huchagua waombaji na kuwagawa kwenye vyuo bila ya kujali wanakotoka. Serikali ilishauri *SUZA* kujitoa kwenye *CAS* mpaka pale ambapo *SUZA* itakuwa na uwezo wa kuwapatia wanafunzi mabweni ya kukaa hasa kwa wanafunzi kutoka Tanzania Bara, kwa sababu wanafunzi wengi ambao wanakuja hapa hawana jamaa. Kwa hiyo serikali imeshauri *SUZA* kujitoa katika udahili huo. Hata hivyo, ni kwamba udahili unafanywa kwa kufuata vigezo ambavyo vimewekwa na Kamisheni ya Vyuo Vikuu pia na kamisheni ndio inayohakiki kupitia majina wanaodahiliwa chuoni. Kwa ufupi orodha wanayodahiliwa *SUZA* hupitishwa na kudhibiti na *TCU* hata kama chuo hakifuati mfumo wa udahili wa *CAS*. Nadhani mheshimiwa atakuwa amelielewa vizuri sana.

Suala jengine ni suala la Mhe. Miraji Khamis Mussa ambae alitaka kujua kuhusiana na mfuko wa bandari ambao unachangia madawati. Aliuliza ni kiasi gani kilichopatikana hadi sasa kutoka katika mfuko huo. Naomba nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba mfuko huo kwanza ulianza mwaka 2013 na jumla ya Tanzania shilingi 3,452,662,465 hadi sasa zimeshapatikana, na jumla ya madawati 2,370, meza 1,730 na viti 1,730 yamenunuliwa na kusambazwa katika skuli za msingi Unguja na Pemba.

Vile vile, alitaka kufahamu ni utaratibu gani unaotumika katika kununua madawati. Ununuzi wa madawati unafuata utaratibu za ugavi na ununuzi za serikali. Lakini suala hili nadhani Mhe. Haroun alilizungumza vizuri sana na kwa sababu serikali tayari hili suala imeliona na inalifanyia kazi. Labda niwaombe waheshimiwa kwamba tuwe wastahamilivu kidogo tu niliisikia kauli ya serikali juu ya suala hili. Lakini katika hilo niwaombe sana waheshimiwa kwamba itakapokuja hii kauli sisi basi tuwe wa mwanzo kuunga mkono juu ya hili suala.

Mhe. Yussuf Hassan alichangia kwa maandishi alitaka vile vile kuuliza kuhusiana na suala la elimu ya mikopo ya juu. Suala hili tayari tumeshalizungumza sana na vile vile alitaka kujua ujenzi wa Skuli ya Pangawe.

Je, skuli ya msingi inayotaka kujengwa Pangawe ni hiyo inayofadhiliwa na Wachina. Mheshimiwa ni kwamba suala la ujenzi wa Skuli ya Pangawe ndio hiyo hiyo ambayo inafadhiliwa na Wachina, na nadhani itakuwa ni skuli ambayo itasaidia sana lile wimbi la wingi wa wanafunzi.

Halafu vile vile Mhe. Yussuf alitaka kujua kuhusiana na Baraza la Mitihani, uvujaji wa mitihani ya darasa la saba na kidato cha pili hili suala likoje. Mhe. Spika, naomba niwajibu waheshimiwa kwamba mwaka 2014 kulikuwa tuhuma tu lakini hakukuwa na uthibitisho wowote, kwa mwaka 2015 hakukuwa na tuhuma yoyote hata hivyo wizara yangu italifuatilia na kuchukua hatua stahiki na hasa kwa wale ambao watakutikana na jambo hili. Vile vile katika hili niwaombe sana waheshimiwa kwamba pale ambapo tunaona kwamba kuna tatizo linajitokeza basi tusilinyamaze tukasubiri mpaka tuje katika kikao. Wizara ya Elimu milango yako ipo wazi lengo ni kujenga elimu yetu na tukizingatia kauli yetu ya elimu bora kwanza, ili tuweze kufikia kauli yetu mbiu ile ni kwamba tunaomba sana waheshimiwa tushirikiane katika kunyanyua maendeleo ya elimu. Tuwe wazalendo zaidi, uzalendo wetu ndio ambao utanyanyua elimu yetu, lakini tukisubiri kila kitu serikali, ni kwamba serikali ni sisi na sisi ndio serikali. Kwa umoja wetu sote tutaweza kuzimaliza changamoto za sekta ya elimu.

Mhe. Spika, napenda nikushukuru sana kwa kunipa fursa hii, lakini nimalize kwamba kwa kuwahakikishia waheshimiwa kwamba Mhe. Rais hakufanya makosa kumteua Mhe. Riziki Pembe Juma kuwa Waziri wa Elimu, lakini vile vile hakufanya makosa kumteua Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri kuwa Naibu wa Waziri wa Elimu. Kwa nini nasema hivi? Nasema hivi kwa sababu nyote ni mashuhuda kwamba sisi tumetoka katika sekta ya elimu, tuna uchungu sana wa sekta ya elimu, lakini ni matarajio yetu makubwa kuona kwamba elimu yetu inakuwa zaidi ya hapo ambapo imekuwa. Kwa pamoja tunaweza kulifanikisha suala hilo, "elimu bora kwanza inawezekana". Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Mhe. Waziri naomba utoe hoja, hapo hapo ulipo.
Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza lako tukufu limejadili…

Mhe. Spika: Bado mheshimiwa hatujafika huko, ulipomaliza ulikuwa useme kwamba unaomba kutoa hoja ili niweze kulihoji hili Baraza.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Samahani Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri.

Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa sasa naomba hoja iamuliwe, wale wote wanaounga mkono hotuba ya Mhe. Waziri ipitishwe wanyanyue mikono yao, wale wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja imetolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri kabla sijakuita tena sasa kwa ajili ya shughuli inayoendelea labda kwanza nitoe matangazo mawili madogo. Kwanza Mhe. Waziri ulisahau katika orodha yako ya waliochangia Mwenyekiti wa Kamati nae ni mchangiaji halali, kwa hiyo kwenye *hansard* ionekane hivyo Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame nafikiri na yeye mwenyewe atafahamu kukaa hapo mambo yanakuwa mengi unaweza ukapitikiwa, kwa hiyo alichukulie hivyo kwamba *hansard* itatambua mchango wake.

Waheshimiwa Wajumbe, kuna matangazo mawili madogo. Tangazo la kwanza ni linatoka kwa Mhe. Hamza kwamba tutakapomaliza hizi shughuli hapa leo waheshimiwa sote tubaki kuna maelekezo yanataka kutolewa kuhusiana na *issue* nafikiri ya bima, ataeleza mwenyewe baadae tutakapokuwa tumemaliza.

Tangazo jengine ni la wajumbe wa CCM kwamba mnatakiwa baada ya kuahirishwa hili Baraza leo tukutane ukumbi wa juu kuna maelezo kidogo kutoka kwa Mwenyekiti wa Wawakilishi wa CCM. Baada ya hapo sasa naomba nimuombe Mwanasheria Mkuu kwa sababu ya muda tulionao na hii hatua ambayo tunataka kuingia, basi tunaomba kidogo tutambue mheshimiwa.

Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kutoa hoja ya kutenga kando kanuni kwa sababu ya muda wenyewe ulivyo na kwa vile tunataka kwenda sasa kwenye mafungu. Sasa naomba kwa heshima kabisa nitoe hoja ya kutenga kando kanuni ya muda ya 23, fasili ya (4) ili Baraza lako tukufu likae kwenye kamati na liendelee mpaka hapo ambapo tutamaliza kupitisha mafungu ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa naomba sasa niwahoji wale wote wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Mwanasheria Mkuu wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi, ili kupitisha vifungu vyote vya matumizi ya wizara yangu.

KAMATI YA MATUMIZI

Mhe. Spika: Kabla hatujaanza wale watendaji wa Mhe. Waziri wa Elimu tungewaruhusu wakakaa nyuma kule ili kuweza kumsaidia kwa karibu, mnaweza mkateremka mkakaa nyuma kwa ajili ya kuja kumsaidia Mhe. Waziri wa Elimu.

FUNGU K01	**WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI**	
Fungu K0101	Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	38,320,000
	Jumla Kuu ya Fungu	**38,320,000**

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

FUNGU K01 WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

Fungu K0101 Programu Kuu ya Elimu ya Maandalizi na Msingi
Kifugu SK010101

Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa): Mhe.Mwenyekiti, nakushukuru. Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia michango yangu nilieleza sana na kufurahishwa na kuwapa pongezi Wizara ya Elimu kwa kuweza kuweka darasa la maandalizi katika Skuli yangu ya Migombani. Lakini nikaelezwa kuchukizwa kwangu sana na hali iliyokuwa mbaya katika madarasa yale nikasema basi kama wako tayari tununuwe mabusati kwa pamoja kama Serikali haina uwezo, sikupata jibu lolote naomba nipewe jibu.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, labda nimuombe samahani kidogo Mhe. Mwakilishi kwamba hilo suala sikulisema inawezekana kutokana na wingi wa makaratasi nimeliacha. Ni kwamba naomba nimuhakikishie kwamba Wizara yangu katika hiyo kutokana na suala zima la madawati basi na skuli yake ya Migombani nayo pia itaingia.

Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa): Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu sana Mhe. Waziri na madamu ameonesha *commitment* zake, tuendelee.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe.Mwenyekiti, na mimi nachukuwa fursa hii kukushkuru sana kunipa nafasi, lakini mimi kwa kuwa swali langu nilichangia mchango wangu kwa maandishi na haukujibiwa wala haukutajwa. Kwa kuwa katika Jimbo langu Skuli ya Mkia wa Ng'ombe, skuli ya Mkia wa Ng'ombe ni skuli iliyoko nje ya mji ambayo mfano wake kama kisiwa na nilipeleka swali langu hili kwenye maandishi halikutajwa kabisa, kwamba ina shida nyingi pamoja na shida kubwa ni ya mahitaji kwamba skuli hiyo haina hata maji.

Sasa nilitaka kujua haina maji, maji yanatoka pale usiku usiku na nilitoa ushauri wa kuwekewa *tank* angalau la lita elfu mbili ili usiku itakapotokea maji kutoka yaweze kuingizwa kwenye *tank* wanafunzi waliopo pale wapate angalau kunawia maji na kwenda chooni wakapata maji ya kujisaidia wakati wakenda haja. Kwa hiyo namuuliza Mhe. Waziri, lini tatizo hili la skuli ya Mkia wa Ng'ombe litatatuliwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsatne sana Mmhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kumjibu suala la nyongeza la Mhe. Omar wa Jimbo la Konde. Ni kwamba

Wizara inahakikisha kwamba itapata fursa ya kutembelea eneo la skuli hiyo na kufanya tathmini inawezekana, litakalogundulikana hapo Wizara itashirikiana na Mwakilishi wa Jimbo hilo kuweza kutatua tatizo hilo, ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, namshukuru kwa jibu hilo, lakini mimi nilitaka *commitment* yake ni kwamba lini tutatafuta safari, maana yake labda hajaamini kwamba hilo tatizo liko, lini baada ya kikao hiki tutakwenda mimi na yeye tufuatane ende akalione ili kuweza kulitatua tatizo hilo kwa haraka.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali napenda kumjibu kama ifuatavyo. Ni kwamba mara tu baada ya kikao cha Baraza tutapanga siku ya kwenda Pemba. *(Makofi)*

Mhe. Omar Seif Abeid: kwasababu ya *commitment* tayari nimeipata tuendelee.

Mhe. Ali Khamis Bakari: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi hii kuweza kuchangia. Wakati nilipokuwa nikichangia hii hotuba Mhe. Waziri, nilimwambia kwamba walimu wetu wa tutu wale ambao tunawawezesha kuwapa zile pesa au posho elfu thalathini nikasema kwamba ni ndogo kuna haja ya kuonekana kuona kwamba tuangalieni watu ambao wanapewa semina tu kwa ajili ya mafunzo fulani labda pengine ya mwani, siku ile wataondoka pale pengine na shilingi elfu ishirini, maji ya *drop*, kababu sijui kitu gani. Sasa kwa hiyo mimi nilikuwa nauliza tu ni lini watu hawa ukilinganisha kwamba mishahara yao au posho lao ni dogo ni lini sasa wataongezewa angalau ile hela yao na wao kidogo wajisikie kulinganisha na hali tunayokwenda nayo, watoto wetu ni wadogo tunawapeleka pale wakiwa hata kuvaa nguo wengine hawajui, kazi walionayo ni kubwa.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, napenda nimjibu Mhe. Ali Khamis Bakari (Doholo) kama hivi ifuatavyo. Suala la posho kwa walimu ni suala ambalo nimezungumza na walimu wengi na waheshimiwa wengi samahani, natokea uwalimu kwa hiyo naomba mnisamehe kwa hilo. Nimezungumza na waheshmiwa wengi lakini kwamba Wizara ya Elimu itaangalia katika upatikanaji wa bajeti yake kwa sababu hatuwezi kuji-*commit* kusema kwamba tutawaongezea na hali upatikanaji wa fedha kama ambavyo sote tunavyoelewa. Lakini naomba nimuhakikishie Mhe,. Muwakilishi kwamba kadiri ya hali ya fedha itakapokuwa ni nzuri basi hata

haya maposho ya walimu watutu na hata walimu wengine basi yataimarika zaidi. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Ali Khamis Bakari: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri, pia nilipeleka kwa maandishi mchango wangu kwamba hawa walimu wanaosomesha hizi tutu kule nyuma mimi nashukuru kwa sababu na mimi natokea huko huko nilipewa vyeti, lakini sasa hivi wale ambao wapo bado vyeti vyao hawapo, ningelitaka

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa hoja nyengine sasa inakuja he!

Mhe. Ali Khamis Bakari: hoja nyengine he! basi tuendelee

Kifungu SK010101	Programu ndogo ya Elimu ya Maandalizi na Msingi	35,880,459,000
	Jumla	**35,880,459,000**

Kifungu PK01

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabla ya yote nichukuwe fursa hii kumpongeza kwa dhati kabisa Mhe. Waziri wa Elimu alivyoonesha uwezo wake na utaalamu wake kujibu hoja za Wajumbe wa Baraza hili. Ni miongoni katika mawaziri bora wa Dkt. Ali Mohammed Shein na yeye yumo. Hoja yangu ilikuwa Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa maslahi ya nyumba za walimu wa skuli ninakotokea Jimbo la Paje, nyumba ziko Jambiani nyumba tano, nyumba hizo hali yake haziridhi na ni kipindi cha muda mrefu. Nataka aniambie tu lini wala sina nia ya kuzuia fungu, anambie lini hizi nyumba ni muda, nyengine hazina paa na usalama wa walimu wanaosomesha pale hauko salama.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda nimshukuru sana Mhe. Jaku, lakini naomba nimjibu kwamba kwasababu Wizara yangu inafanya ziara katika maskuli mbali mbali na kwasababu skuli zetu ni nyingi sana ni kwamba katika kufanya ziara kwetu inawezekana pengine tumeenda upande mwingine na upande mwengine hatujaenda. Lakini naomba nimuhakikishie Mhe. Jaku kwamba binafsi yangu nitafanya ziara katika Jimbo lake la Paje na katika ziara hiyo mbali ya kuzungumza na walimu kujua changamoto za walimu, lakini hata changamoto kama hizo ambazo zipo basi tutazifanyia kazi, naomba nimuhakikishie, *inshallah*.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, mimi nimshukuru tena Mhe. Waziri, lakini aniambie tu muda wenyewe ni lini? muda unaweza ukasubiri kesho, kesho kutwa baada ya mwaka miaka miwili ni muda vile vile, aniambie tu baada ya Ramadhani kwisha au baada ya sita anieleze lini tu.

Mhe. Mwenyekiti: Baaada ya bajeti, kwasababu sitamruhusu Waziri aende na wewe pia mkaacha shughuli za Baraza, kwa hiyo muende baada ya bajeti.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mheshimiwa sina tatizo lakini utakuwa kama ulomjibia yeye angejibu yeye mwenyewe Mhe. Mwenyekiti, ungeomba radhi kwa hilo, angepata *commitment* ili *Hansard* zikakaa sawa huko.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante Mwenyekiti, kunipa nafasi hii na mimi. Na mimi katika mchango wangu nilizungumzia suala zima la ahadi ya muda mrefu la ukuta au fence katika skuli ya Jang'ombe ya Sekondari, imefikia hatua sasa hivi lile eneo linavamiwa na kuna ubadhirifu wa vifaa vya shule, sijui lini Mhe. Waziri, hujanijibu unaniambiaje katika suala hilo.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, naomba nimjibu Mhe. Abdalla Maulid Diwani kama ifuatavyo; suala la ukuta kwanza ni swali ambalo haliko katika skuli ya Jang'ombe peke yake lipo katika skuli nyingi na sisi Wizara tunafanya tathmini ya skuli mbali mbali ya skuli mbali mbali hasa zile ambazo zina changamoto nyingi kama ambavyo skuli ya kwake ili kuona ni kiasi gani kitaweza kutumika kwa ajili ya kujenga uzio ndani ya skuli hizo. Kwa hiyo naomba nimuhakikishie Mheshimiwa kwamba tutakapomaliza bajeti yetu hii katika ile ziara yetu hasa kutembelea hasa kwa kila skuli zetu tutaangalia katika kila skuli na kuona samani ambayo itahitajika na Serikali peke yake kwa kweli haiwezi kufanya lakini kwa kusaidiana na wazalendo kama yeye mmoja wapo mwanamapinduzi, lakini vile vile kwa kusaidiana na wafadhili wetu basi suala hili tutalifanyia kazi *in shaa Allah*, ahsante.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante; pamoja na majibu mazuri sana Mheshimiwa nashkuru ukitilia maanani wewe ni mpya katika Wizara hii basi naomba tuendelee.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na wakati mimi nachangia pia nilizungumzia kuhusiana na suala la watoto wetu kuharibiwa kwa kutokana na maovu ya kupata mimba wakati wako mashuleni, wakati wanasoma jambo ambalo linaathiri familia, vijana wale watoto na kuharibu

maisha yao; sasa hakuna majibu niliyopata ya kuridhisha ningependa kufahamu kwanini?

Mhe. Mwenyekiti: hoja ipi? hebu nenda *specific*

Mhe. Simai Mohammed Said: naomba nirudie tena, kwa kuwa watoto itakapotokea kwamba wamepata mimba mashuleni wakati ni wadogo hasa wa sekondari pamoja na *primary* na hili linakuwa ni janga na linaathiri familia na nguvu kazi ya maisha ya kesho pamoja na watoto wenyewe, sasa sijapata maelezo ambayo ya kuonesha kabisa na ni hatua gani za kisheria za kinithamu zinafanywa sijui kuna *policy* gani za kuwalinda watoto ningependa nifahamu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, ngojea wa-*communicate* na Waziri wa Kazi labda anaweza akasaidia.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mwenyekiti, kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, napenda kumjibu Mhe. Simai swali lake kama ifuatavyo: Ni kwamba suala hili sisi katika Wizara pale tumeanza kulifuatilia kwa undani ili kujua ukubwa wake lakini tuliwahi kuzungumza na Mhe. Waziri anayeshughulikia wanawake na watoto na yeye pia kufanya utafiti kwa upande wake, ili kulijua hilo tatizo ukubwa wake. Sasa tatizo ambalo sisi katika elimu tunalipata kwamba ni la kuwepo ushirikiano mdogo kwa wazazi, wakati wakipata habari tukifuatilia basi mzee anasema ata! keshaolewa na hichi hapa cheti cha ndoa.

Mhe. Mwenyekiti, Kwa hiyo ni kwamba sisi tutakapopata ushahidi wa ukubwa wa tatizo basi tutapeleka hoja yetu Serikalini ili kuona tunachukuwa hatua gani zaidi wakati suala likiwa kubwa, likiwa dogo tutaendelea kuchukuwa hatua za kisheria zilizopo, ziko wazi kabisa sheria ile ya elimu iko wazi, kwamba anayempa ujauzito mwanafunzi, yeye aliyepata ujauzito na aliyehusika kupata ujauzito wote sheria itachukuwa mkondo wake, lakini kwa sasa kwa kweli nikuhakikishie kwamba tunafanya utafiti ili kuujuwa ukubwa wa tatizo lake. Maana yake sasa ukisikia mitaani unaambiwa tatizo ni kubwa lakini ukifanya utafiti pengine likawa dogo, kwa hiyo Wizara ya Elimu inafanya uchunguzi ili kuona ukubwa wa tatizo halafu baadaye hatua zinazohusika zinachukuliwa.

Mhe. Simai Mohammed Said: ahsante Mwenyekiti, pamoja na swaumu lakini naona haya majibu niliyopata kwbasababu hili tatizo lipo na ni kubwa na linajulikana na Wizara na limekuwa kama linafichwa chini kwa chini ili lisitoke. Ni sahihi kweli wazee wanachukuwa hatua za kuficha lakini katika masuala yangu niliuliza juu ya *preventing measures* ni hatua gani, kwasababu

yeye amenijibu kwamba hapa tatizo limeshatokezea unakwenda wazee wanatoa vyeti vya ndoa, wakati hapo tayari mtoto ameshapokea ujauzito. Nimesema ni hatua gani ambazo wao tayari, wanasema wapo kwenye utafiti, lakini hili tatizo lipo na linaendelea na tayari watendaji wake wanalifahamu ndani ya Wizara. Sasa hapa tulipo sasa hivi ananiambia wanaanza utafiti, utafiti huo labda nimuulize anahitaji watoto wapate mimba ngapi ili utafiti ukamilike.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, napenda kumjibu Mhe. Simai kama ifuatavyo. Ni kwamba kauli zilizopo kwamba tatizo hili ni kubwa, lakini utafiti mpaka sasa hauoneshi hivyo, tunapokwenda katika data zetu tulizonazo Wizara ya Elimu na nina hakika na Wizara ya Wanawake bado *data* ni chache, ndio tukasema kwamba lazima tufanye utafiti wa kina ili kulijuwa ukubwa wake suala hili. Lakini hata hivyo ni kwamba suala hili wakati tutakapobaini ukubwa ukubwa wake, lakini hata tusibaini ukubwa wake ni kwamba suala hili liko mikononi mwetu sote wananchi, ni suala mtambuka linatuhusu Wizara ya Elimu inamuhusu Muwakilishi inawahusu wazee.

Kwa hivyo vile vishawishi vinavyosababisha tatizo hilo basi inabidi lazima tuchukuwe hatua za pamoja ili kujikinga, hiyo ndiyo hali halisi, vyenginevyo ni kwamba ni muhimu kufanya maamuzi yetu kwa ushahidi tunaita *evidence based decision* kwa hiyo tunakusanya utafiti ili kuweza kutoa maelekezo na ushahidi, ahsante.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, mimi naweza kukubali kwa njia moja ili kifungu kiendelee hapa kwa kusaidia hapa Baraza, ni kwamba nipate ahadi kutoka Wizara husika kwamba mimi naamini wao wanasema hawana taarifa za kutosha, mimi naamini taarifa zipo za kutosha na zipo taasisi ambazo zinafanya kazi na haya mambo yapo nje na ripoti pia katika Shehia na maeneo watu tafauti. Sasa ili tuondoke hapa aniahidi kwamba atatayarisham, *prevention measures* ya hili suala la *child policy* kutoa elimu na kufanya kampeni za pamoja juu ya kulinda hawa watoto wetu ili wasiharibike. Je, hiyo ahadi ninaweza kupata kutoka kwake.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa *with all respect* lakini nafikiri hili swali kama ni la Wizara yaani kuna Wizara maalumu ambayo *portfolio* yake inahusiana na suala hilo, hata kama litakuwa limetokezea katika Taasisi za Elimu, bado Wizara ambayo itatakiwa kuli-*engage* suala hili ni Wizara ambayo inashughulika na masuala ya Wanawake, Jinsia na vitu kama hivyo. Kwa hiyo Waziri wa Elimu kwa kweli sifikirii kama atakuwa na msaada mkubwa sana

zaidi ya hapo. Mhe. Waziri wa Kazi, tafadhali. Mhe. Simai, naomba urudi kwenye kiti chako *please*.

Mhe. Maudline Cyrus Castico: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kabisa nashukuru kusema kwamba suala hilo alilolisema Mhe. Simai, ni suala ambalo linatugusa wote na kwa sasa hivi Wizara zote mbili Wizara ya Elimu na hasa Wanawake na Watoto ambayo ni Wizara inafanya jitihada za kila namna kuhakikisha kwamba jambo hili linapatikana. Lakini kwa kuanzia angetusaidia sana kama Mwakilishi atuletee hizo taarifa alizonazo tuanze nazo ili tuendelee kufanya kazi hii.

Kwa upande mwengine nataka kusema kwamba suala hili si la Wizara ya Elimu ni jamii nzima na hasa kwa wanaume, wanaume ambao nasema baba ambae hajachukua nafasi yake inavyostahiki. Wanaume wanapofika kwenye *adolescence age* wanajaribu kila kitu, lakini bado nimegundua kwamba wanaume hawajafanya kazi, *role* ninayowapata kama wazazi wa kiume kuwaambia mwanangu wa kiume ukianza kuona ndevu zinaota, kifua kinapanuka kwa watoto wa kiume, unaota ndoto za ajabu usimsogelee mtoto wa kike. Kwa sababu katika kipindi hicho kwa vyovyote vile ukigusana na mtoto wa kike utampa mimba, kitu ambacho wazazi wa kiume tunawahitaji sana. Wanawake tunafanya upande wetu lakini katika hili mhusika mkuu ni mzazi wa kiume na viongozi wa dini katika imani zote. Namuomba sana Mheshimiwa awe karibu na sisi, atupe taarifa alizonazo ili tuanze nazo. Ahsante sana.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti ahsante, japo kuwa na upya wangu lakini haya majibu yamenipiga kisiasa kidogo. Kwa sababu swali nililouliza mimi nasema ni matarajio yangu kwamba niko tayari tuendelee, lakini nahitaji iwekwe *policy* katika Wizara ya Elimu katika kulinda maslahi ya wanafunzi katika skuli. Kwa sababu katika vitendo vinavyofanyika hatuwezi kujua vinafanyika kati ya wanafunzi wanaume na wa kike au pengine unaweza kusema ni baina ya walimu pia vinatokezea. Sasa *by then* tunapotoka tunampeleka katika wizara husika tunaingia katika jamii ambayo *just a social side* sawa, ambapo yule mtoto itabidi ahitaji malezi yake, kumlea, kumpa ushauri, pale ndipo tunakwenda kwa Mheshimiwa. Lakini *policy* gani Wizara ya Elimu itakuwa nayo kumlinda na wizara zote na katika serikali zote.

Ulaya ukienda Kenya, South Africa wanazo *policy* ndani ya Wizara ya Elimu; *child support, child protection,* mwanamke, mwanamme. Sasa mimi nataka hiyo *policy* ndani ya Wizara ya Elimu je, kwa muda wa kutoka sasa hivi na

tunakokwenda mbele Mhe. Waziri atakuwa yuko tayari kuweka hiyo? Kama atashirikiana na wizara husika mimi sina tatizo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nimesikiliza kwa makini sana hoja ya Mhe. Simai Mohammed Said na nadhani tumuelewe anachokusudia ni kitu gani. Kuna mambo mawili ambayo anayazungumza Mhe. Simai, la kwanza sijui anamaanisha kwamba sera au sheria katika namna ya kumlinda mtoto ambae anasoma skuli. Lakini iwe hivyo ama iwe kwa maana ya kwamba sheria au sera, zote mimi naamini serikali imefanya jitihada kubwa sana. Lengo lake kubwa analozungumza Mhe. Simai Mohammed ni namna ya kumlinda ili kuwa salama katika mkondo mzima wa masuala ya kusoma.

La kwanza serikali imetunga sheria ya kumlinda mtoto, madhumuni yake kumlinda huyo huyo mwanafunzi pia.

La pili, serikali ina sheria inayohusiana na masuala mazima ya wanafunzi imemlinda mtoto na imemlinda mwanafunzi huyo huyo.

La tatu, serikali ina Sheria Nam. 7 nadhani ya mwaka 2004 ya Makosa ya Jinai, mtoto humu amelindwa kwa nguvu zote. Kwa hiyo, mimi nimuombe Mhe. Simai Mohammed kwamba jambo hili ambalo analizungumza ni *cross cutting issue*, kwa maana ya suala mtambuka, halina lazima tu kwamba litungiwe sera katika Wizara ya Elimu linalindwa na serikali kwa ujumla wake kwa kupitia wizara yoyote katika mnasaba ule wa kuhakikisha kwamba mwanafunzi ama mtoto anakuwa salama katika utaratibu mzima wa kusoma, pamoja na kulindwa haki zake mpaka pale ambapo umri utakapomruhusu kuwa na maamuzi yake yeye mwenyewe binafsi kwa mujibu wa sheria na kwa mujibu wa katiba ya nchi. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, nasema mimi nataka tuendelee, lakini nataka tuendelee katika njia ambayo ya matumaini, siyo ya kunipa mimi matumaini ya kuwapa hawa wazee ambao ni waathirika juu ya watoto wao ambao wanapokea hizi mimba na ni wanafunzi. Sasa japo kuwa hili jambo kama alivyosema Mhe. Waziri kwamba linagusa maeneo mengi lakini lazima wizara husika kuna vitu vingi inatakiwa ivifanye, kuna masuala ya *resources, training,* kutoa elimu, kufanya *message campaign*, ndani ya hilo kwa sababu mwisho wa siku watu wanakaa masaa 10 mpaka manane pamoja ndani ya skuli. Kwa hivyo, lazima hizo *policy* ziwe ndani ya hizo skuli baina ya mwalimu na wanafunzi, watoto, *engagement* zote.

Sasa mimi nataka kauli ya waziri husika ataweka hizo *policy* za kumlinda mtoto ndani ya wizara husika? Kama atashirikiana na wizara hiyo ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto mimi sina tatizo nataka kauli ya waziri.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa sheria inayohusiana na masuala haya ipo sasa unataka iletwe *policy* juu ya sheria. Sheria nafikiri ni *stronger* kuliko sera. Mhe. Mwanasheria Mkuu hebu tusaidie.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na nachukua fursa hii pia kumshukuru Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa ufafanuzi mzuri ambao ameutoa. Anachosema Mhe. Simai Mohammed tayari kimeshashughulikiwa, katika moja ya jambo ambalo serikali hii ililishughulikia katika awamu yake ya kwanza ni kutunga Sheria Nam.6 ya Mwaka 2011, Sheria ya Mtoto ambayo ndani yake inaelezea mengi ambayo Mhe. Simai Mohammed ameyazungumza ni sheria kubwa kidogo.

Sheria ile inatokana na Mkataba wa Kimataifa wa *CRC* ambapo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania uliridhia na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania likakubali mkataba ule wa Kimataifa kutumika Tanzania. Sisi kama Zanzibar *role* yetu ilikuwa sasa ni kutunga sheria ya ku *domesticate* ile *convention* ambayo imetoka. Sasa mengi yameelezwa mule ndani ya sheria ile.

Vile vile kuna sheria ya kulinda wari, wajane na mengi yameelezwa kule ambayo yanatakiwa *maintenance* yafanywe, lakini pia kumpa fursa yule mtoto kuendelea na masomo yake pale ambapo kuna matukio hayo yatamkuta. Sasa mengi yamefanywa mimi nilidhani hoja ya Mhe. Simai kama kuna zaidi ya haya ambayo tufanye hiyo nadhani ndio ingekuwa hoja ya kutushauri, lakini sheria zipo nzuri, sheria zinaeleza vizuri sidhani kama kuna zaidi ya hapo ambalo *commitment* inaweza kutoka kwa Wizara ya Elimu.

Mimi nadhani Mhe. Simai aisome vizuri ile sheria halafu kama kuna jambo ambalo anaona tuliongeze basi tushirikiane naye katika kulifanyia kazi. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ah, nimepigwa na watu wanne basi tuendeleeni Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Sio basi bwana, yaani tuendelee tu Mheshimiwa.

Mhe. Simai Mohammed Said: Nakubali kushirikiana.

UTARATIBU

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa kidogo nataka utaratibu kwa sababu nafikiri Kanuni zetu zinatutaka kwamba Mheshimiwa hoja yake apate maelezo kwa waziri mara tatu ikizidi hapo ina maana ipigwe kura. Lakini kwa kulisaidia hili mimi nadhani Mhe. Simai unajua ndio huo ugeni, ndio maana tukataka hizi semina. Tatizo la Mhe. Simai yeye ni mgeni lakini vile vile inavyoonesha yeye alivyokuwa anataka utekelezaji wa hii sheria yenyewe. Sheria zipo nzuri tu za kumlinda mtoto na hata ukisikia malalamiko kwenye vyombo vya habari watu wanalalamika katika vile vyombo vya kutoa hukumu zinapokuja hizi kesi.

Kwa hivyo, mimi nafikiri Mhe. Mwenyekiti hoja ya Mhe. Simai ilikuwa ni *right* lakini yeye alikuwa anatetea kwamba anaona mbona haya mambo yanafanyika lakini hatua hazionekani, ndio maana akaona kwamba hakuna sheria zinazowalinda watoto. Lakini sheria zipo tumezipitisha, mimi nafikiri tuitake serikali hivi vyombo tulivyovipa mamlaka wachukue hatua za kisheria. Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana nakushukuru sana na ninawashukuru mawaziri wote waliotoa maelezo na pia naomba nimshukuru Mhe. Hamza Hassan Juma kwa maelezo ya sasa hivi na naomba niweke *hansard* iwe sahihi ili serikali isiwekwe *at a weak point*. Kwa hiyo, *hansard* hiyo iwekwe sahihi.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara yangu ya Afya ndio inayoshughulika kisheria na masuala yote ya watoto akilawitiwa, akinajisiwa, akifanya jambo lolote analetwa kwanza kabisa katika huduma ya Mkono kwa Mkono kwangu mimi. Kwangu mimi sio kama mimi, katika Wizara ya Afya na pale ndipo *enforcement agency* zote. Hili naomba nilitolee maelezo, ikiwa mwanafunzi yuko skuli akiwa wakati wa skuli ama hata nyumbani kwao au nyumbani kwa wazee wake, akiwa ameshapitia Wizara ya Wanawake na Watoto ama hajapitia analetwa pale kwa ajili ya *medical approval.* Pale sasa hivi muongozo tuliopewa kisheria lazima na askari awepo ndio maana tumeanzisha vile vituo vya Mkono kwa Mkono ambapo askari anakuweko pale *24 hours* na huenda *very soon* tukafungua vituo hasa ndani ya hospitali zetu katika vituo vya Mkono kwa Mkono askari anakuwepo.

Sasa ninachotaka kumwambia Mhe. Hamza Hassan Juma kwa maelezo yake ya ziada aliyotoa ni mazuri kabisa pamoja na Mhe. Simai. Nitatoa mfano wa kesi

moja ambayo mimi mwenyewe nimeishiriki kuipokea na nimeshiriki katika *process* jumla ya kujifunza.

Kesi hiyo imemtokezea mtoto sheria za kumlinda mtoto zipo, sheria za *enforcement agency* yaani polisi na vyombo vyengine vya ulinzi na usalama ipo, daktari husika yupo amesha-*prove* yule mtoto amefanyiwa kitendo hiki na mimi mwenyewe nipo nimeliona hilo, tukasema hili lichukuliwe hatua.

Mhe. Mwenyekiti, tulipotaka kulichukulia hatua ndio narudi kwenye ile hoja ya Mhe. Hamza mama mtu kaingilia kati sisi hospitali nzima na wafanyakazi wetu na askari na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali walikuwepo sote kama kikundi kizima pamoja na *Save the Children* hii kesi imo katika *Save the Children* wameirikodi wanaipeleka ulimwenguni kutoa taarifa hizo. Pale mama mtu kasema hapana, sitoweza kuendelea na kesi hii tukambembeleza mama yule tafadhali turuhusu twende nayo mbele.

Kwa hiyo, mara nyingi kesi hizi katika rekodi na kwa ajili ya rekodi ya Mhe. Simai na kwa ajili ya Mhe. Hamza ni wazee wanaoingilia kati, hata utafiti gani ukifanyika ni wazee wanaoingilia kati kusema isiendelee. Mhe. Mwenyekiti, likaja kugundulikana kumbe kesi ile ilifanywa na mjomba wa yule mtoto ambae ni kaka yake mama mzazi. Kwa hiyo, ndio maana mama yule akatuomba sisi haiwezekani mimi nilikuweko kwenye hilo akasema Mheshimiwa nakuomba tafadhali hii ni aibu yetu sisi kifamilia isiendelee mbele tutalitatua zaidi.

Kwa hiyo, hata tuchukue takwimu gani mara nyingi sisi tunashindwa kufanya kazi yetu ku-*enforce* kwenda mbele kwa sababu wale watoaji ushahidi wanakuwa wanakataa na hii ni kutokana na mila, silka, tamaduni na desturi zetu tulizokuwanazo katika familia. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu PK0102	Program Kuu ya Elimu ya Sekondari	
Kifungu SK010201	Program ndogo ya Elimu ya Sekondari	47,301,328,000
	Jumla ya Kifungu:	47,301,328,000

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu PK0103 Programu Kuu

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini pia Mhe. Waziri pamoja na naibu wake katika kipindi kifupi

wameonesha uwezo mkubwa sana katika kusimamia masuala ya wizara yao. Nawaomba sana waendelee na moyo huo na sisi tutajitahidi kuwasaidia katika kutekeleza majukumu yao. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi hoja yangu moja tayari Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango aliijibu vizuri sana kuhusu suala la madai ya walimu, malimbikizo na hata wale waliostaafu aliahidi vizuri na Mhe. Naibu Waziri pia ameeleza vizuri. Kwa hivyo, hilo naliacha sasa nakuja katika suala la Elimu Mjumuisho.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri alinijibu vizuri pale, lakini pia nilikuwa nataka msaada kidogo wa ufafanuzi. Unajua walimu wangu wameongezeka humu ndani maana yake na Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali na yeye pia ni mwalimu wangu kanisomesha; sasa nauliza kwa nidhamu sana. Suala langu nataka kujua kwamba *SUZA* wameanzisha *diploma* ya Elimu Mjumuisho na tatizo walilokuwanalo kama suala langu nilivyoeleza kwa maandishi wana uhaba wa walimu na walimu wanachukua kutoka katika maeneo mengine. Sasa kwa nini hiki Chuo cha *Muslim* ambao wao wameanzisha mafunzo ya *certificate* katika hii ngazi ya Elimu Mjumuisho, kwa nini na wao wasiruhusiwe wakaanzisha hii ngazi ya *diploma.* Kwa sababu wao tayari wana walimu wa kutosha ili kuweza kusaidia ili wale wanafunzi wakapata elimu kule mpaka *SUZA* wakishakuwa na walimu wa kutosha na wao wakaendelea nao.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante naomba nimjibu Mhe. Hamza Hassan Juma kwamba, kuhusu suala la kuanzishwa *diploma* ya Elimu Mjumuisho katika Chuo cha Kiislamu, Mazizini labda naomba nimwambie kwamba suala hilo tayari Taasisi ya Elimu inaandaa mtaala maalum wa Vyuo vya Ualimu. Kwa hiyo, katika mtaala huo suala hilo pia la uanzishwaji wa *diploma* ya Elimu Mjumuisho ndani ya Chuo cha Kiislamu pia lipo. Kwa hiyo, namuomba awe bukheri kuwa suala hilo tayari linafanyiwa kazi.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, ama kweli Mhe. Waziri mtaalamu wa Kiswahili mana amenambia nikae bukheri, yaani *bukheiri wa hamsa wa ishiriin*. Kwa hiyo, kama nilivyosema kwa kweli kutokana na ufuatiliaji wao kwa kifupi hii wizara naona tutakwenda vizuri sana tuendelee Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti nikushukuru, nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa sababu amekuwa akitugonga gonga kidogo. Lakini hata hivyo, nilipokuwa nikichangia nilieleza kukerwa kwangu na Bodi ya Elimu, kwanza niliipongeza sana lakini kukerwa kwangu kulikuwa zile *living*

expenses, pesa za kujikimu kwa wale wanafunzi zinachelewa na hazifiki kwa wakati watoto wanalalamika wanakwenda katika hali ambayo siyo. Naomba *commitment* ya serikali hapa.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kuhusiana na suala zima la Bodi ya Mikopo kama Ofisi ya Wizara ya Elimu tumelifafanua, lakini vile vile nikikariri kauli ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango pia amelifafanua vizuri. Suala la ucheleweshaji wa pesa zile za kujikimu unatokana na ucheleweshwaji wa pesa kuingia ndani ya wizara yetu, lakini kwa sababu tayari Wizara ya Fedha imetuahidi hapa kwamba fedha hizo zitaingia kwa wakati na hasa kuzingatia changamoto nyingi ambazo zinajitokeza, labda watoto wetu wanawake hasa wanawake kudhalilika na Wizara ya Fedha tayari hili suala imeliona na kupitia wizara hiyo itahakikisha, kwamba fedha hizi zinaingia kwa wakati. Sisi Wizara ya Elimu mara tu pesa hizi zinapoingia basi tutakuwa tayari kuzipeleka kwa wanafunzi husika.

Kwa hivyo, naomba nimhakikishie Mhe. Mwakilishi hili kwamba wizara yetu kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha mara tu pesa hizi zinapokuwa zimeingizwa katika wizara yetu basi tutakuwa sisi hatuzicheleweshi. Ahsante sana.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu sana Mhe. Waziri kwa maneno yake aliyosema, lakini inaonesha vipi serikali haiko makini kwa suala la wanafunzi. Anasema Wizara ya Fedha haiingizi fedha Waziri wa Fedha leo yupo atwambie atawaingizia lini, wanafunzi wanapata tabu walioko nje na ndani ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, hili tujue Waziri wa Fedha yupo atwambie *commitment* gani serikali itapeleka na lini itawapelekea pesa, hatuwezi kuliacha hivi hivi. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mohamed Said Dimwa, kwanza nataka nimhakikishie kwamba serikali hii iko makini sana na yote yanayofanywa yanafanywa kwa mujibu wa maslahi ya wananchi wa nchi hii. Nilichokisema kwenye maelezo wakati natoa mchango wangu ni kwamba serikali itajitahidi kwa sababu serikali yetu inategemea mapato na bajeti yetu ni *cash budget*. Kwa hivyo, pesa tutakapozipata nilisema kwamba zitaingizwa kwa wakati ili kuwaondoshea usumbufu wanafunzi wetu. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mwakilishi ndugu yangu akubali hilo aachie wizara hii kwa maana ya kifungu hiki kiendelee kwa

sababu bado sisi tuko makini watendaji, mawaziri, manaibu mawaziri, serikali kwa ujumla tuko makini na hili tutalifanyia kazi kikamilifu.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu sana kaka yangu Waziri wa Fedha lakini kutokana na kuwa nimezowea sana kujibiwa kisiasa serikali iko mbioni, serikali haijafika, hili linaudhi sana katika wanafunzi wetu. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru lakini nimshukuru sana Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa) kwa kusimamia hoja yake kikamlifu na kwa kusema kweli kanifilisi, ilikuwa hoja yangu ni hii hii mie. Namshukuru sana.

Kifungu PK0103 Programu kuu ya Elimu ya Juu

Kifungu SK010301 Program Kuu ya Elimu ya Juu 13,542,552,000
Kifungu PK 0104 Program Elimu Mbadala ya Mafunzo ya Amali
Kifungu SK010401 Program

Mhe. Nadir Abdul- latif Yussuf Al- Wardy: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri wa Elimu kwa kuja kulitembelea jimbo langu nilisahau kumsifu, nampongeza sana yeye na wizara yake nzima. Kwa kuja kufanya ziara ya jimbo langu kukagua skuli, namshukuru sana.

Katika hoja yangu niliyochangia nilichangia walimu wa masomo ya dini kwa maana kwamba Chuo Madrasa. Kwa kuwa ninavyofahamu mimi Wizara ya Elimu. Elimu kuna elimu ya dunia na elimu ya akhera. Lakini sasa alichojibu wakati walipokuwa akitoa hoja yake kwamba hawa walimu wa chuo wanatambulikana na Mufti Mkuu.

Sasa mimi suala langu liko moja kama ni elimu Wizara ya Elimu wakati pia Madrasa ni elimu lakini ni elimu ya Akhera kwa nini wao hawawatambui kama Wizara inatambuliwa na Afisi ya Mufti na lini itawatambua wizara hii walimu wa chuo.

Mhe. Mwenyekiti: Swali lako moja tu Mheshimiwa la pili hilo hatulijibu.

Mhe. Wazri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma: Namshukuru Mhe. Nadir Abdul- latif Yussuf Al- Wardy kwa swali lake zuri sana na niwashukuru wote waliochangia hoja hii. Lakini Mheshimiwa nimkumbushe tu kwamba jambo hili tulilizungumza hapa hapa na tukalimaliza

na tukatoa ufafanuzi na nilisema mimi kwamba Afisi ya Mufti inalifanyia kazi suala hili na mimi nimesema mwenyewe, kwamba nitafanya kila njia kutafuta wahisani ili kusaidia njia gani kuwasaidia walimu wetu wa Madrasa. (*Makofi*)

Mhe. Nadir Abdul- latif Yussuf Al- Wardy: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, unajua anazungumzia suala hili angalau tupate thawabu tuingie peponi. Naomba tuendeelee, nilisahau.

Mhe. Ali Khamis Bakari (Doholo): Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti na mimi kunipa nafasi hii kwa mara nyengine tena.

Mhe. Mwenyekiti nilipokuwa nikichangia nilimuuliza Mhe. Waziri kwamba upungufu wa walimu ni kipingamizi kikubwa cha kueleta maendeleo ya elimu katika majimbo yetu na serikali au nafasi nchi nzima kwa ujumla.

Mimi kwa ushahidi nilionao ndani ya Wilaya yangu ya Micheweni walimu 12 hawa walistaafu kiufupi na miongoni mwa hao 12 mmoja wapo alifariki. Wizara kwa kipindi hiki ilisitisha kwa kupitia serikali uajiri wa walimu. Sasa je, serikali kwa kupitia wizara hii ni lini itaajiri walimu hawa kwa kuweza ku-*cover* walimu hawa nafasi zile ambazo walikuwa wanafunzi wanazipata. Kwa sababu sasa hivi ni mwaka huu wanafunzi wamekaa na tukizingatia kwa walimu wengi walikuwa wa Sayansi, *Art* na pamoja na kwamba ni sehemu tafauti ya ndaji ya majimbo.

Kwa kweli ni changamoto kubwa sasa nimuombe Mhe. Waziri ni lini kwa kupitia serikali wataajiri walimu hawa ili kuondosha haya matatizo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma: Mheshimiwa nimesimama hapa kuendelea kutoa ufafanuzi kidogo suala hili na naomba nimjibu Mhe. Ali Khamis Bakari wa Tumbe suala lake muhimu sana.

Nataka nitoe ufafanuzi kwamba serikali haijafuta ajira imesimamisha kwa muda tu tena ajira zote sasa hivi kutokana na mipangilio tuliokuwa nayo kiserikali. Lakini kwa walimu wale ambao wanachukuwa Sanyansi wote wanapewa *priority* iwe ngazi ya Diploma, Digrii ni walimu wale wa masomo ya *Art* kidogo ndio kulikuwa na mtihani kidogo. Hata hivyo pale inapotokea haja katika maeneo mengine serikali haishindwi kutoa *priority* katika eneo lile.

Kwa hivyo, tutaliangalia vizuri kusaidiana na Wizara ya Elimu sisi watu wa Utumishi ili kushirikiana nao ili kuonesha kwamba tunatoa kila aina ya

msukumo kuhakikisha kwamba suala hilo tunalitekeleza na kuwasaidia. Pale ambapo pana upungufu basi serikali itachukuwa hatua za haraka kabisa.

Mhe. Ali Khamis Bakari (Doholo): Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba tuendelee, lakini waliangalie suala hili kwamba ni mtihani sana. Hasa ukizingatia suala la jimbo langu hali ni nzito.

Kifungu SK010401	Program ya Elimu Mbadala na Watu wazima	14,744,579;000
Kifungu SK010402	Program ya Elimu ya Mafunzo ya Amali	1,228,010,000
	Jumla	**15,972,589,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

Kifungu PK 0105 Programu kuu ya Ubora wa Elimu
Kifungu SK0105

Mhe. Mwenyekiti: Nitawapa Waheshimiwa wapya wawili Mhe. Panya Ali Abdalla na Mhe. Miraji Khamis Mussa. Halafu Mhe. Hamza Hassan Juma mara moja kwa hiyo nitakupa wewe. Nilikupa mara mbili Mheshimiwa lakini moja ukasamehe.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru na pia nitoe shukurani zangu za dhati kwa Mhe. Waziri na Naibu Waziri kwa majibu mazuri kabisa ambayo yanatuonesha mwanzo mzuri kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilizungumzia kuhusu suala la wakaguzi. Mhe. Mwenyekiti, ubora wa walimu ni pamoja na kuwa na wakaguzi watakaofanya kazi vizuri na nikaishauri serikali, kwamba wakaguzi hawa tuwapate kiwilaya ili kuwapunguzia yale masafa waweze kufanya kazi zao vizuri.

Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti, sikuwahi kulipata jibu nilikuwa naomba Mheshimiwa na nasisitiza tena ukaguzi ule wa jumla jumla hatufikii malengo ya kupata hiyo elimu bora. Naomba ukaguzi huu ufanyike kiwilaya ili ile elimu bora ambayo tunakusudia tuweze kufanikiwa naomba nipate jawabu.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Mwakilishi wa viti Maalum suala lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa mama angu mpenzi ni kwamba ni kweli alizungumza hili suala na tayari nilikuwa nimeliweka lakini kwa bahati mbaya nimekosa kulisoma. Lakini kwamba suala ambalo nimelizungumza la kuweka suala ambalo nimelizungumza la kuweka, vituo vya ukaguzi ndani ya wilaya hili suala tayari, sisi Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali tayari tumeshaliweka na kumuhakikishia hili, ni kwamba kwa matumizi ya Wilaya tunatumia vile vituo vya Walimu *TC* kwa ajili ya kuweka pale Ofisi za Ukaguzi.

Kwani ni suala ambalo lipo katika yaani sio mipango ya muda mrefu ni suala ambalo tayari lipo na ndani ya muda mfupi tu *inshaallah* suala hili litakuwa tayari na kila Wilaya itakuwa na wakaguzi kupitia katika vile vituo vya *TC* vya walimu afisi zao zitakuwa hapo. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naridhika sana na majibu ya Mhe. Waziri na kwa kuwa wameonesha mfano mzuri ambao utatupelekea kwenda katika hiyo Elimu Bora ambayo tunaitegemea Mheshimiwa tuko tayari kutoa mashirikiano kwa viongozi wetu hawa, ili ile elimu bora tunayoikusudia iweze kupatikana. Mheshimiwa tuendelee.

Mhe. Miraji Khamis Mussa(Kwaza): Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu mazuri katika suala langu nililomuuliza la mchango kwa wasafiri kutoka miundo mbinu.

Mhe. Mwenyekiti amenitaja *figure* ya milioni tatu na ametaja *figure* ya madawati kwa maana ya viti na meza lakini bila ya kujua gharama na bilioni tatu kwa kawaida ni nyingi sana na kwa namba ya viti na meza alizozitaja.

Ningependa kujua kwa uhalisia viti vimegharamika kiasi gani na meza hizi zimegharamika kiasi gani ili tujue bilioni tatu hizi zipo au zimetoka ngapi au zimeisha zote. Kwa sababu ni jambo kubwa sana la kuwachangisha watu na matumizi yake yakawa hayaeleweki. Sasa nataka *figure* kamili.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba nimjibu Mhe. Miraji Khamis Mussa (Kwaza) kama ifuatavyo:-

Ni kweli nilimjibu hiyo idadi ya ambayo nimemjibu ya madawati pamoja na viti na meza. Lakini naomba nimwambie tu fedha za Mfuko huu wa Bandari hizi bilioni tatu mbali ya kuchonga madawati ambayo tumechonga na meza lakini vile vile tumezitumia pesa hizi kwa kulipia madeni. Madeni ambayo tulikuwa tayari tumeshachongesha vile vifaa ya kwamba madawati pamoja na meza na tulikuwa kwa bahati mbaya hatujalipia zile gharama.

Kwa hivyo, baada ya kupata fedha zile na kwa vile fedha zile zilikuwa maalim kwaajili ya madawati basi tulichukuwa kiwango cha pesa kulipia madeni yale madawati na kiwango kilichobakia ndicho ambacho tumetengeneza madeski haya. Ahsante sana, nadhani itakuwa nimemridhisha Mheshimiwa.

Mhe. Miraji Khamis Mussa (Kwaza): Mhe. Mwenyekiti, bado hoja yangu naendelea kuizuia na tunaweza kupiga kura.

Nataka kujua madeni ya serikali kwenye madawati ilikuwa ni kiasi gani, ili serikali hapa tujue ililipa kutoka bilioni tatu zilizokusanywa na madawati waliochonga baada ya ukusanyaji wa hizi fedha kwa namba ya viti vingapi, meza ngapi ili tuunganishe. Kwa sababu hii fedha wanachangishwa wananchi wa nchi hii na huduma lazima iende kwa utaratibu mzuri kama matarajio yao ya kuchangia katika mfuko huu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri sijui una majibu ya Mheshimiwa au;

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Mwakilishi kama ifuatavyo:-

Kwa bahati mbaya ni kwamba hatuna zile hesabu yaani vile ambavyo anataka yeye moja kwa moja kwamba kiasi gani zimetumika kwa ajili fulani na kiasi gani zimetumika kwa ajili fulani. Hesabu ambayo tumechukuwa sisi hii hesabu ipo si kama haipo lakini kwa bahati mbaya hapa hatuko nayo. Lakini ni kwamba hiyo hesabu ipo kiasi gani kimetumika kwa ajili gani.

Naomba tu nimwambie kwamba apitishe hili fungu ili hayo madawati lakini na vile vile vifaa nyengine tunavipata kama ambavyo serikali ina nia na wajibu wa kufanya hivyo.

Kwa ushirikiano wa pamoja kati yetu sisi na yeye Mheshimiwa basi nadhani hili linawezekana sana. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Miraji Khamis Mussa (Kwaza): Mhe. Mwenyekiti, bado sijaridhika kwenye eneo hili na nimuombe tu Mhe. Waziri na Mawaziri wengine. Kama ulirithi madeni waliyatafuta wenzio. Lazima nijue deni tulilolilipa na tulichotumia sasa.

Pia Mhe. Mwenyekiti, niiambie serikali kunako mambo makubwa kama haya ambayo wananchi wana matarajio makubwa kuja ndani ya chombo hiki tukawa hatupati majawabu yenye muelekeo kwa kujenga nchi yetu ni tatizo. Naomba .....

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Miraji Khamis Mussa (Kwaza), nafasi zako zote utakuwa umeshazitumia, nafasi tatu na bado hujaridhika kanuni inatutaka tuende kwenye kura na Mhe. Waziri nadhani katika majibu yake amekwambia kwamba ile takwimu hapa hana lakini ipo na ameahidi kwamba utaweza kuipata.

Sasa naomba kama utaridhika utaipata baadae au tupige kura hapa sasa hivi ili tuendelee.

Mhe. Miraji Khamis Mussa (Kwaza): Mhe. Mwenyekiti, Kabla ya utaratibu huo anaotaka kuusema Mhe. Hamza Hassan Juma Waziri katika majibu yake hajaniahidi kama atanileta kwa maandishi na mimi kwenye hili kama sijaahidiwa maana jambo kubwa kama hili....

Mhe. Mwenyekiti: Kasema mtashirikiana mie nimemsikia uzuri kwamba baadae mshirikiane, nafikiri ndio maana yake mje mpate hayo majibu yaliyo sahihi.

Mhe. Miraji Khamis Mussa (Kwaza): Mhe. Mwenyekiti, ushirikiano mzuri ainuke aahidi kwamba kwa Baraza hili atatuletea kwa maandishi haya tuliomuhoji.

Mhe. Mwenyekiti: Haya Mhe. Waziri mridhishe.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba nimridhishe Mheshimiwa wangu katika jimbo la dhahabu kwamba nitamletea taarifa hii kwa maandishi *in shaa Allah,* ahsante sana.

Mhe. Miraji Khamis Mussa (Kwaza): Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, mimi hoja yangu hapa niliandika kwa maandishi lakini kutokana na muda wa Mhe. Waziri hakuwahi

kuitolea ufafanuzi. Niliuliza kwamba serikali baada ya kuzuia michango kwa wananchi suala hili kidogo wananchi limewachanganya sana kwa sababu michango ilikuwa ya aina nyingi, kulikuwa na michango wa ada ya mitihani, kuna michango mingine sasa kuna baadhi ya shule kuna ile michango inasaidia katika kuboresha yale mambo mengine ambayo pengine serikali haikuweza kuyafanya kwa wakati katika zile shule ile walimu waweze kusomesha vizuri.

Sasa sijapata jawabu na kwa mfano mzuri wenzetu Bara kule serikali, baada ya kuzuia michango kuna mafungu ingawa kule wenzetu Wizara hizi za Elimu kuna zile serikali za mitaa kuna fedha zilipelekwa kusaidia mambo mbali mbali. Lakini hapa kwetu pako kimnya. Sasa nilikuwa nataka kupata ufafanuzi tu kwa serikali je, michango ya aina gani ambayo imezuiliwa.

Je, ile michango ya kuboresha mambo madogo madogo ya kuendeleza skuli zetu hii iko vipi na kama ile pia imezuiliwa je, serikali kuna fungu gani ambalo inatoa kupeleka kule maskuli ili kusaidia wale walimu kuboresha yale baadhi ya mambo ambayo hayako sawa.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii kumjibu Mhe. Hamza Hassan Juma mwanafunzi wangu kama ifuatavyo:-

Ni kwamba kuzuia michango kumekwenda kwa mujibu wa ngazi, katika ngazi ya skuli ya Msingi mchango wa aina yoyote unapigwa marufuku badala yake serikali inagharamia baadhi ya mambo ya msingi ya kuendeshea skuli yote yanagharamiwa na serikali.

Kwa upande wa Sekondari bado baadhi ya michango inaendelea lakini pia nayo imewekewa miongozo maalum si kwamba wafanye wanavyotaka. Nakumbuka kama Sekondari baina ya ishirini na ishirini na tano isizidi hapo ikizidi hapo ni kosa kwa mujibu wa maelekezo ya wizara. Ahsante.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, unajua siku hizi wanaposimama walimu wangu huwa kidogo Mhe. Hamad Rashid aya yake kidogo inanitisha.

Unajua nilikuwa nataka tu nijue kwa sababu kama ni walimu walikuwa wakichangisha kulikuwa na baadhi ya huduma wanaboresha kule maskulini. Lakini baada ya kuzuiliwa ile michango ina maana zile fedha hazipatikani. Sasa ndio maana nilitaka kujua je, kuna fedha gani za ziada ambazo toka

kusimamishwa hii michango zimepelekwa kule kwenye Shule za Msingi ili kuziba lile pengo ambalo wananchi walikuwa wakichangishwa.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba nimjibu Mhe. Hamza Hassan Juma kama ifuatavyo:-

Kwanza namshukuru Mhe. Naibu Waziri pia kwa kulifafanua vizuri hili suala ni kwamba serikali imefuta hii michango. Lakini nia na madhumuni ni kusaidia wananchi wake na hasa kwa sababu ya kuona kwamba wanafunzi wengi walikuwa hawaandikishwi ipasavyo hasa Msingi na Maandalizi.

Kutokana na kufutwa huku haina maana kwamba serikali haitoi msaada. Msaada upo ingawa hatujaonesha hapa kwamba ni kiasi gani tunapeleka lakini Wizara ya Elimu ni kwamba tunakuwa tunapeleka msaada ikiwa unahitajika na zaidi kwa mfano katika Skuli za Maandalizi, kuna suala la watoto kupikiwa chakula kama uji.

Kwa hiyo, wizara kwa kushirikia na wafadhili wetu tunakuwa tunafanya hicho kitu. Kwa hiyo, yote ni katika kuona kwamba michango imeondoshwa lakini zile huduma zinaendelea. Lakini vile vile linapokuja suala la mitihani ikiwa ya majaribio na mitihani mingine, wizara ndio inabeba jukumu lile. Lakini katika hatua hiyo ni kwamba Wizara ya Elimu kwa sasa inajaribu kwenda katika ule mfumo mpya ya kuwa wabunifu zaidi na tunapokwenda kwa walimu wetu wakuu, lakini kupitia Maafisa Elimu wa Wilaya na Mikoa tunakuwa tunashajiisha skuli ziwe na ubunifu

Ubunifu wenyewe mmoja wapo ni kuandaa miradi hasa ile midogo midogo ndani ya maskuli yetu na kwa baadhi ya skuli tayari hili suala limeshaanza. Kuna baadhi ya skuli wanalima mboga mboga. Mboga mboga zile zinakuwa zinauzwa na zinapouzwa ni kwamba tayari zile pesa zinasaidia maendeleo ya skuli. Haina maana kwamba wazee ndiyo watoe bali ni kwamba mchango ule unakuwa unasaidia.

Ninadhani nimemjibu vya kutosha Mheshimiwa. Ahsante sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, mimi ninafikiri labda niwape muda hili walifanyie kazi, wajipange zaidi, kwa sababu tatizo hapa tunaogopa hii elimu bora baada ya kwamba ikikosa zile huduma za haraka sana. Maana yake mboga hata ikishalimwa, ikishaota, huku mambo yanaharibika. Sasa tunataka kile kiwango tunachokitaka kifikiwe. Lakini kama nilivyosema kwa sababu hii hoja yangu ya tatu, nilikuwa naomba tuendelee lakini naomba Mhe.

Waziri akalifanyie kazi ya ziada ili kujua namna gani huko mbele tunakokwenda.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea.

Kifungu SK 010501	Programu Ndogo ya Ubora wa Elimu	Shs.2,407,216,000/-
	Jumla Kuu	**Shs.2,407,216,000/-**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

Kifungu KK 0106 Programu Kuu ya Uongozi wa Elimu

Mhe. Mwenyekiti: Wa kwanza ni Mhe. Miraji Khamis Mussa halafu utakuja Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Wardy, halafu tutamalizia Mhe. Mohamed Said Mohamed.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilimuuliza Mhe. Waziri kuwa kuna kampuni iliyowahi kuruhusiwa na baadhi ya viongozi wa Wizara ya Elimu kukusanya fedha *Majengo Auction Mart* za wanafunzi kwa ajili za kuwatafutia vitambulisho, kwa kuwaandalia usafiri wa kuwahi maskulini. Lakini mpaka sasa hakuna mwendelezo wa hilo na pesa hawa wanafunzi baadhi yao wa skuli za Unguja na Pemba wameshachangia.

Ni nini hatma ya serikali kwa wanafunzi hawa waliochangishwa fedha zao na hizi fedha ukizingatia ni fedha za wakulima sikupata majibu. Naomba nipate majibu na hapa ndipo panapo fungu la utawala na waliohusika ni viongozi.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mhe. Miraji Khamis Mussa akiwa katika jimbo la dhahabu la Chumbuni kwa suala lake.

Kwa kweli nina masikitiko kidogo kwamba hiyo habari kwangu mimi bado ni mpya. Lakini naomba nimuombe Mhe. Mwakilishi kwamba hiyo habari nimeichukua na tutaifanyia kazi. Na naomba aniamini kwa hilo kwamba hapa kazi tu, tutafanya kazi yake. (*Makofi*)

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Wardy: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri tena kwa kuwa vifungu vyake vimeshamaliza anakaribia kufunga daftari.

Lakini mimi suala langu dogo nililiuliza kwenye hotuba yangu kwamba wale wazee wengi sana wenye uwezo mdogo huwatuma watoto wadogo kwenda na ng'ombe wakati wa skuli kupakia maji kuuza, kuuza maandazi, samaki, njugu wakati wa skuli. Je, wizara inachukua hatua gani kwa wazee kama hawa wanaowakosesha watoto elimu badala yake kuwafanyisha kazi ambazo haziwahusu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya Mhe. Waziri napenda kumjibu Mhe. Nadir kama ifuatavyo.

Hili kama ulivyosema ni suala mtambuka. Ni suala ambalo linakwenda katika wizara au sehemu nyingi. Hili ni suala la ajira ya watoto kwa hivyo litafika kwenye wizara nyengine. Lakini hata hivyo sisi kwetu Wizara ya Elimu kwa kweli tunafanya mikutano ya kuwahamasisha wazazi kuwapeleka watoto wao skuli kujifunza. Na hili tunalifanya mara kwa mara katika mikutano, kwenye matembezi yetu kuona kwamba wazazi wanahamasika na kuwapeleka watoto skuli.

Kimsingi kama nilivyosema awali kuwa suala la ajira watoto linashughulikiwa na wizara nyengine, lakini kama serikali tunafanya kazi kwa pamoja. Kwa hivyo tunawaelimisha wazazi.

Kwa mujibu wa Sheria ya Elimu ya mwaka 1982 mzazi akishindwa kumpeleka mtoto wake skuli ni kosa kubwa kwa kweli. Ninafikiri nitakuwa nimemjibu Mhe. Mwakilishi na atakuwa yupo radhi.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Wardy: Mhe. Mwenyekiti, ninampongeza sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake lakini ningeomba wizara hizi mbili zishirikiane kuwapa elimu wazee wote Unguja na Pemba kwa ujumla. Ahsante sana tuendelee.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilionesha furaha yangu sana kwa Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kipindi cha miaka sita imejenga zaidi ya skuli ishirini na moja za ghorofa.

Lakini suala langu lilikuwa kwenye Skuli ya Kibuteni. Kipindi kirefu sana na kwenye hotuba yao wametwambia imejengwa kwa asilimia kama 42, lakini *physically* tukenda pale tunakuta kama asilimia 30 au 20. Sasa nilikuwa ninataka kujua kwa sasa amepewa mkandarasi gani na hasara gani iliyopata serikali kwa kipindi chote ambacho skuli hii ilikuwa imalize.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya Mhe. Waziri ninapenda kumjibu Mhe. Mohamed Said Mohamed kama ifuatavyo.

Ni kweli mimi binafsi nilifanya ziara ya kutembelea skuli ile na maneno anayosema Mhe. Mwakilishi ni sawa. Na tulipofika kwa mara ya mwanzo tulimuagiza mkandarasi kufika Ofisini, ilikuwa ni siku ya Alhamisi tulimuagiza afike ofisini siku ya Jumatatu.

Alipokuja kule akazungumza na watendaji wangu na mkandarasi aliyepewa anaitwa *United Builder* na bado hajahamisha, kazi zake anaendelea, lakini kwa pole pole sana. Sasa kuna mambo ambayo baada ya sisi Wizara kutoridhika tukapeleka taarifa kwa Mwanasheria Mkuu kushauriana hatua gani tuzichukue dhidi ya mkandarasi yule katika hatua hii tuliyofanya.

Kwa kweli hapo mwanzo alionesha ufanisi mkubwa katika kazi kiasi ya kwamba wizara ilishangaa kwa kasi, lakini baada ya muda akaanza kuzorota. Sasa baada ya kuzorota, sasa hali hiyo ya kuzorota inaendelea hadi hii leo. Siku nyengine apeleke mifuko mitano, siku nyengine hamsini lakini pale katika *site* bado hajahama yupo. Kwa hivyo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inashauriana na Mwanasheria Mkuu ili kujua hatua gani za kuchukua dhidi ya mkandarasi huyo.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, nilizungumza mapema sana kuwa serikali haipo makini. Na kwa sababu hiyo basi pesa hizi ni pesa za wananchi za walipa kodi na pesa za *BADEA* zimeendelea kukaa. Mpaka leo tunaendelea na mashauriano.

Hebu atwambie Mwanasheria Mkuu ni kitu gani kinafanyika ili kuweza kuiondoa, aidha tuweze kuukatisha ukandarasi wake labda tutapata hasara kiasi gani. Lakini kama inawezekana kwa nini tusiweze kukatisha mkataba huu na mkandarasi ili skuli hizi na wananchi wakafaidika kwa haraka zaidi.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru na kama ambavyo Mhe. Naibu Waziri wa Elimu amejibu. Ni kweli skuli hii yule

mkandarasi ambae amepewa amechukua muda mrefu kujenga na kumaliza ile skuli ukitilia maanani wale ambao waliingia nao *contract* pamoja na wengi walimaliza na yeye amekuwa akisuasua. Jambo ambalo tumefanya na tumekubaliana serikalini ni kutafuta sasa utaratibu wa kuvunja naye mkataba na hilo ndiyo jambo ambalo sasa lipo mezani kwetu.

Of course unapofanya mambo haya Mhe. Mwenyekiti, kuna *liability* unapovunja mikataba ambazo na sisi kama serikali lazima tuzi-*manage*. Ni kweli lipo Ofisini kwetu tunalishughulikia na pale ambapo tutamaliza basi tutatoa taarifa ya jinsi ambavyo tumelishughulikia. Ni kweli ninalijua na tunalishughulikia.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, sasa nimeona *concern* yangu ipo wapi na ule umakini unaotakikana upo wapi. Lakini madhali Mwanasheria Mkuu ameshasema basi tuendelee.

Fungu KK 0106 Programu Kuu ya Uongozi wa Elimu

Kifungu SK 010601 Programu Ndogo ya Uongozi na Utawala Shs.2,253,889,000/-
Kifungu SK 010602 Programu Ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Omar Seif Abeid na Mhe. Simai Mohammed Said.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, na mimi ninashukuru tena kunipa tena nafasi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Skuli ya Maandalizi ya Konde. Skuli hii haina uzio, haina mlinzi na skuli hii ni hivi karibuni tu iliibiwa kila kitu chake kilichomo humo ikabakishwa viti na meza tu, mpaka vyombo vya kupikia vya wale watoto wa chekechea viliibiwa. Na kwamba wizara Pemba inajua suala hili...

Mhe. Mwenyekiti: Samahani Mheshimiwa. Jambo unalohoji hebuaangalia na hicho kifungu. Hicho kifungu unachokizuia ni cha Mipango, Sera na Utafiti.

Mhe. Omar Seif Abeid: Eeh! kupanga na kusimamia kazi za wizara.

Mhe. Mwenyekiti: Hichi cha chini ninadhani ndiyo kinakuhusu wewe au vipi.

Mhe. Omar Seif Abeid: Cha chini eeh! Kwa hivyo ninakaa Mhe. Mwenyekiti, lakini ikifika zamu yangu unipe.

Mhe. Mwenyekiti: Wewe kaa mheshimiwa. Mhe. Simai Mohammed Said. *(Kicheko)*

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi wakati ninachangia nilihoji juu ya ukurasa wa 91 na 92 na ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya matumizi ya milioni thamanini na tisa na arobaini na tatu elfu pamoja na milioni sita kwa Kampuni ya *Facima General Traders* juu ya malipo haya yaliyofanyika.

Sasa sijapata maelezo yoyote. Ahsante.

Mhe.Mwenyekiti: Mheshimiwa ripoti ya *PAC* imekuja hapa. Maana yake nina wasi wasi haijafanyiwa kazi.

Mhe. Simai Mohammed Said: Nimezungumza juu ya matumizi katika kitabu cha ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hichi ni cha 2013 ninafikiri lakini naona kama inajumuisha....

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa hiyo ni *current.*

Wajumbe: Tuendelee.

Mhe. Simai Mohammed Said: Hawa wananichanganya sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Aah! wewe zungumza na mimi. Jaalia hawapo hao Mheshimiwa. Tuendelee.

Yaani nilikuwa ninakuuliza hiyo ripoti ni hii ambayo *current* imekuja au vipi? Hiyo ripoti ya mwaka huu au vipi.

Mhe. Simai Mohammed Said: Hizi ni ripoti ambazo tunaletewa kama Wawakilishi tumezipitia.

Mhe. Mwenyekiti: Ripoti ya *PAC* mpaka mwezi wa Machi, yaani mpaka waifanyie kazi kamati.

Mhe. Simai Mohammed Said: Lakini hapa hatuwezi kuwapata kabisa.

Mhe. Mwenyekiti: Hapo utawaonea Mheshimiwa. Tunaendelea.

Kifungu SK 010602	Programu Ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti	Shs.2,065,502,000/-
Kifungu SK 010603	Programu Ndogo ya	

Mhe. Mwenyekiti: Haya ni Kuratibu Shughuli za Kielimu Pemba. Mhe. Omar Seif Abeid na Mhe. Suleiman Sarahan Said.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ninashukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kunirejeshea tena nafasi yangu. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Skuli yangu ya Maandalizi katika Jimbo langu la Konde haina uzio wala haina mlinzi. Na ni hivi karibuni Mhe. Mwenyekiti, skuli hiyo wezi waliweza kuingia ndani wakaweza kuiba kila kitu kilichomo hapo ndani ya skuli hiyo mpaka masufuria, wakabakishiwa viti tu.

Na kwa kuwa hii Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inalijua kwa sababu ripoti tayari imefika. Je, wizara ina mpango gani wa dharura wa kuiwekea skuli hiyo uzio pamoja na mlinzi ili ulinzi wa skuli hiyo upatikane ukitilia maanani kwamba skuli hiyo ipo nje kidogo ya makaazi ya watu.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana. Mhe. Waziri kabla sijakupa Mhe. Omar Seif Abeid umetumia ujanja kwa sababu Skuli ya Mkia wa Ng'ombe hoja ilikuwa hiyo hiyo. Sasa hiyo umeitafutia na hii. Yaani ungeweza hoja yako ingekuwa ya uzio ukazitaja hizo skuli mbili lakini sasa umeitafutia pahala. Lakini wacha Waziri akujibu.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, ninadhani kama ambavyo Mhe. Mwakilishi kakiri kwamba hili suala tayari tumeshalijibu. Lakini hata hivyo bado tutaendelea kumjibu tena kwamba kama nilivyomjibu awali kuwa wizara yangu tayari kwamba inafanya tathmini ya gharama ya ujenzi wa uzio, zikiwemo skuli mbali mbali hata hii ambayo ameitaja.

Lakini kwa muda huu ambapo anasema kwamba skuli imeibiwa. Mimi ninadhani yeye Mhe. Mwakilishi akiwa ni kiongozi wa ile sehemu basi tushirikiane kwa pamoja tujue nini tunafanya kudhibiti hali ya wizi wa ile skuli.

Lakini katika kushirikiana vile vile na jamii nzima, walimu wenyewe na yeye kiongozi na viongozi wengine basi tuone kwa namna gani sisi wenyewe tunaanza katika kudhibiti vile vitu vyetu ili visidhurike.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Omar Seif Abeid tena utakubaliana na mimi kwamba hata jawabu ya Mhe. Waziri haina tofauti na ile ya mwanzo.

Mhe. Omar Seif Abeid: Sawa Mhe. Mwenyekiti, ninakubaliana naye kwa majibu mazuri lakini sina tatizo nalo nitamtaka tu Naibu Waziri atekeleze yale aliyoniambia. Ahsante tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante tunaendelea. Mhe. Suleiman Sarahan Said.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Ninashukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi leo sikupata bahati ya kuzungumza kwa mdomo lakini pia nilipata kwa maandishi, lakini pia Mhe. Waziri alinisahau lakini ninamsamehe siyo vibaya sana.

Lakini mimi kutokana na kadhia yangu niliyokuwa nayo Chake Chake. Mimi na muda wa kufutari unakaribia na sala, lakini kwa hivyo ningemuomba Mhe. Waziri au Naibu Waziri kwa kuchangia kwa yote ni kwamba ninamtaka kwa muda wa siku mbili aseme tu aje Chake Chake nimuoneshe matatizo yangu ya Chake Chake kwa Wizara ya Elimu basi.

Ninashukuru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said (Sele Manga) wa Jimbo la Chake Chake.

Ninachukua ahadi hiyo na tutaonana inshaallah.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Ahsante sana, ninashukuru.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea.

Kifungu SK 010603	Programu Ndogo ya Kuratibu Shughuli za Kielimu Pemba	Shs.20,766,931,000/-
Jumla Kuu		**Shs.140,188,395,000/-**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ahsante sana Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya fedha ya wizara yangu bila ya mabadiliko. Sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza likubali makadirio hayo.

Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Sasa naomba nichukue nafasi hii kuwahoji wale wote ambao wanakubaliana na hoja ya makadirio haya wanyanyue mikono yao, wanaokataa, Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe ninalo tangazo jengine moja na hili safari hii linakuja kufuta lile tangazo moja la awali kati ya yale mawili ambayo nimeyatoa. Kikao cha Waheshimiwa Wajumbe wa CCM kimeahirishwa mpaka litakapotoka tangazo jengine.

Kwa hivyo lile jengine linabaki kwamba Wajumbe mupate maelekezo na baada ya matangazo hayo na kwa kuwa shughuli zetu zimemalizika za siku ya leo, naomba sasa niahirishe shughuli za Baraza la Wawakilishi mpaka kesho siku ya Jumanne saa tatu barabara za asubuhi.

(Saa 9.58 jioni Baraza liliahirishwa hadi
tarehe 14/06/2016 saa 3.00 asubuhi)